# HARAKATI ZA USHAIRI WA KISWAHILI KATIKA UJENZI WA JAMII YENYE MABADILIKO: MFANO WA DIWANI YA KARNE MPYA

**GACERI MARTHA**

**C50/CE/34860/2016**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine.

Sahihi................................. Tarehe 2/5/2025...........

GACERI MARTHA

C50/CE/34860/2016

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii:

Sahihi........................................ Tarehe 2/5/2025...............

**DKT.EDWIN MASINDE**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES
KENYATTA UNIVERSITY

## SHUKURANI

Imekuwa safari ndefu sana yenye changamoto tele. Ni safari iliyohitaji nguvu na uvumilivu mwingi kuikamilisha. Ningependa kuwashukuru wengi sana ambao wamechangia kufanikisha kazi hii ambayo kwa hakika ni mojawapo ya mafanikio yangu maishani.

Kwanza, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa wazo la kufunga safari hii. Zaidi kwa kuniwezesha kuvuka viunzi vyote nilivyokumbana navyo hadi tamati.

Pili, shukurani za dhati zimwendee msimamizi wangu Dkt.Masinde kwa ushauri mwafaka pamoja na kunitia moyo nilipoonyesha dalili za kukata tamaa. Mola ammiminie baraka daima.

Tatu, ningependa kuwashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa mafundisho ya kufana katika kozi zote ambazo ziliwezesha kufanikisha kazi hii.

Vile vile, ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu, hasa Hellen, Jannet, Angeline, Mercy, na Jacob kwa mchango wao; hasa kunitia moyo na kunihimiza kukamilisha safari. Asanteni sana na Mungu awajalie mema.

Hatimaye, ningependa kuwashukuru wazazi na ndugu zangu kwa kunitia moyo na kufuatilia hatua za kazi hii kila mara. Mungu awazidishie baraka.

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu Charity Gaiti na Simon Murega. Mmekuwa nguzo imara kwangu.

## YALIYOMO


**UNGAMO** ........ **ii**

**SHUKURANI** ........ **iii**

**TABARUKU** ........ **iv**

**IKISIRI** ........ **x**

**ABSTRACT** ........ **xi**

**MAELEZO YA ISTILAHI** ........ **ix**

**YALIYOMO** ........ **v**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1Usuli wa Mada ........ 1

1.2 Suala la Utafiti ........ 4

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 5

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 6

1.6 Upeo na Mipaka ........ 7

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 8

1.8.0 Misingi ya nadharia ya Uhistoria Mpya ........ 12

1.8.1 Mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya ........ 14

1.9.0 Mbinu za utafiti ........ 15

1.9.1 Muundo wa utafiti ........ 15

1.9.2 Mahali pa utafiti ........ 16

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 16

1.9.4 Ukusanyaji wa Data ........ 17

1.9.5 Uchanganuzi wa Data ........ 17

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ........ 17

1.9.7 Maadili ........ 18

1.9.8 Kiishilio ........ 18

**SURA YA PILI ........................................................................................................ 19**

**MIKTADHA ILIYOIBUA HARAKATI ZA KULETA MABADILIKO KATIKA JAMII** .......................................................................... 19

2.1 Utangulizi ........................................................................................................ 19

2.3 Muhtasari wa Diwani ya Karne Mpya............................................................ 19

2.4 Miktadha iliyoibua harakati za kuleta mabadiliko katika jamii ....................... 20

2.4.1 Miktadha ya kisiasa ........................................................................................ 20

2.4.1.1 Vipindi vya uchaguzi na siasa ...................................................................... 21

2.2.1.2 Ukoloni mamboleo ........................................................................................ 23

2.2.1.3 Ufungwa ........................................................................................................ 26

2.2.1.4 Uongozi Mbaya ............................................................................................. 30

2.2.2 Miktadha ya kijamii........................................................................................ 33

2.2.2.1 Utabaka........................................................................................................... 33

2.2.2.3 Ndoa za Mapema ........................................................................................... 36

2.2.2.4 Matumizi Ya Dawa Za Kulevya.................................................................... 38

2.2.2.5 Maradhi.......................................................................................................... 39

2.2.2.6 Ubaguzi.......................................................................................................... 42

2.2.2.7 Ukengeushi .................................................................................................... 44

2.2.3 Miktadha ya kiuchumi.................................................................................... 47

2.2.3.1 Umaskini........................................................................................................ 47

2.2.3.2 Ubepari na Dhuluma za Kibepari ................................................................. 50

2.5 Kiishilio .......................................................................................................... 52

**SURA YA TATU ..................................................................................................... 55**

**MBINU ZA KUJENGA JAMII YENYE MABADILIKO KATIKA DIWANI YA KARNE MPYA ...................................................................... 55**

3.0 Utangulizi ........................................................................................................ 55

3.1 Kuhimiza Kumbukumbu za Historia.............................................................. 55

3.2 Kuhimiza Umakinifu wa Wananchi ............................................................... 57

3.3 Kuhimiza Umoja, Ushirikiano, Bidii na Uzalendo ........................................ 60

3.4 Kuhimiza Ushirikiano Katika Kupiga Vita Matumizi ya Mihadarati .............. 63
3.5 Kuonya Viongozi Dhidi ya Dharau .............................................................. 64
3.6 Kuhimiza Uvaaji wa Mavazi ya Heshima ...................................................... 65
3.7 Kuhimiza Maskini Kutia Bidii ..................................................................... 66
3.8 Kuwasuta Mabepari ....................................................................................... 67
3.9 Kukashifu Ndoa za Mapema .......................................................................... 68
3.10 Kukashifu Ukoloni Mamboleo na Ubaguzi wa Kimataifa ............................ 69
3.11 Kuhimiza Tahadhari Dhidi ya Ukimwi ......................................................... 69
3.12 Kuhimiza Haki na Usawa wa Kijinsia .......................................................... 71
3.13 Kiishilio ........................................................................................................ 72
**SURA YA NNE ......................................................................................................... 73**
**UMUHIMU WA HARAKATI ZA UJENZI WA JAMII YENYE MBADILIKO KATIKA JAMII YA SASA .......................................... 73**
4.0 Utangulizi ......................................................................................................... 73
4.1 Uzindushi .......................................................................................................... 74
4.1.1 Kuelewa Unafiki wa Viongozi ....................................................................... 74
4.1.2 Kujuza Kuhusu Unafiki wa Mataifa Yaliyoendelea ..................................... 74
4.2 Uwajibikaji ....................................................................................................... 75
4.2.1 Kudumisha historia ......................................................................................... 75
4.2.2 Kumaliza Mihadarati Shuleni ....................................................................... 77
4.2.3 Kudumisha Utamaduni wa Afrika ................................................................. 77
4.2.4 Kumaliza Udhalimu na Ubepari .................................................................... 78
4.2.5 Kupiga Vita Maradhi ....................................................................................... 78
4.2.6 Kumaliza Uzembe na Utegemezi .................................................................. 79
4.3. Usawa ............................................................................................................... 80
4.3.1 Usawa wa Kitabaka ......................................................................................... 81
4.3.2 Usawa wa kijinsia ........................................................................................... 82
4.4 Kiishilio ............................................................................................................. 83

**SURA YA TANO** ........................................................................................ **85**
**HITIMISHO NA MATOKEO YA UTAFITI** ................................................ **85**
5.0 Utangulizi ........................................................................................ 85
5.1 Muhtasari ........................................................................................ 85
5.2 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................ 87
5.3 Changamoto za utafiti ........................................................................................ 92
5.4 Umuhimu wa utafiti ........................................................................................ 93
5.5 Mapendekezo ........................................................................................ 93
**MAREJELEO** ........................................................................................ **94**
**VIAMBATISHO:** ........................................................................................ **97**
Mashairi teule ........................................................................................ 97
Kibali cha NACOSTI ........................................................................................ 122

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Jamii yenye mabadiliko:** Kauli hii ilitumika kurejelea jamii isiyo na matatizo yaliyoshuhudiwa mara tu baada ya uhuru nchini Kenya.

**Jamii ya sasa:** Jamii ya karne ya ishirini na moja.

**Harakati:** Kwa mujibu wa utafiti huu, neno harakati lilitumiwa kwa maana ya mikakati ya kuibadilisha jamii inayodhihirika katika mashairi teule yaliyo katika *Diwani ya Karne Mpya*.

**Muktadha** Ni hali ambayo hujumuisha mazingira ya tukio au mazungumzo na ambayo husaidia katika uelewekaji wa jambo. Hali hii inaweza kuwa ya kiuchumi, kisiasa. kijamii au kihistoria

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Mashairi yaliyorejelewa ni yaliyo katika *Diwani ya Karne Mpya* (2007). Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha miktadha iliyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko, kueleza harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika diwani teule, pamoja na kuonyesha umuhimu wa harakati hizo katika jamii. Utafiti huu uliongozwa na baadhi ya mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya. Nadharia ya Uhistoria Mpya ina misingi yake katika mawazo ya Raymond Williams (1977) na Michel Foulcault (1972, 1977, 1997). Nadharia hii huangalia uhusiano uliopo kati ya historia na fasihi. Hivyo, kazi ya fasihi haiwezi kutengwa na historia inayohusika nayo. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Utafiti ulifanywa maktabani na mitandaoni. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kimakusudi na data ikakusanywa kwa kusoma kwa kina mashairi teule na kunukuu sehemu ambazo zina data iliyokidhi mahitaji ya utafiti husika. Mtafiti pia alisoma vitabu, majarida, tasnifu na machapisho mbalimbali yaliyohusiana na mada. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia iliyoongoza utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari na utoaji mifano. Utafiti huu ulibaini kuwa harakati mbalilmbali za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko, zimeibuliwa na miktadha mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Isitoshe, harakati hizi zina mnachango muhimu katika jamii ya sasa. Inatarajiwa utafiti huu utachangia katika uhakiki wa fasihi kinadharia. Aidha, utaifaa jamii hasa katika kuelewa harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko na manufaa yake. Tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia utagulizi, usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada nadharia iliyoongoza utafiti huu pamoja na mbinu za utafiti. Sura ya pili imeshughulikia miktadha iliyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Sura ya tatu imeshughulikia harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Sura ya nne imeshughulikia umuhimu wa ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Sura ya tano imeshughulikia hitimisho, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

## ABSTRACT

This research investigated the role of Swahili poetry in developing a changed society. The poems referenced are from the anthology *Karne Mpya (2007)*. The objectives of this study were to identify the contexts that inspired Kiswahili poetry into developing a changed society, to explain the role of Kiswahili poetry in developing a changed society and to demonstrate the significance of this role in the society. This research was guided by some principles of the New Historicism theory, which is based on the ideas of Raymond Williams (1977) and Michel Foucault (1972, 1977, 1997). This theory examines the relationship between history and literature, suggesting that literature cannot be separated from the history it's associated with. The study adopted a descriptive design and was conducted in libraries and online search. A purposive sampling method was used to collect data by thouroughly studying the selected poems and quoting sections that provided relevant information for the research. The researcher also reviewed books, journals, theses, and various publications related to the topic. Data was analyzed based on the research objectives, guided by the tenets of New Historicism Theory. The findings of this study were presented through descriptive explanations and giving suitable examples. This research identified that various movements for developing a changed society have emerged from different economic, political, and social contexts. Furthermore, these movements play a significant role in contemporary society. It is expected that this study will contribute to theoretical literary criticism and will be beneficial to society in understanding the best means of creating a changed society and their significance. This thesis is divided into five chapters. The first chapter addresses the introduction, background of the topic, research problem, research objectives, research questions, reasons for choosing the topic, scope and limitations, existing literature on the subject, the guiding theory of this research, and the research methodology. The second chapter discusses the contexts that inspired the need for developing a changed society. The third chapter focuses on the role of Swahili poetry in developing a changed society. The fourth chapter addresses the importance of developing a changed society. The fifth chapter concludes with the research findings, challenges encountered, and suggestions for future research.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii, mambo yafuatayo yalijadiliwa: Usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na hitimisho.

## 1.1 Usuli wa Mada

Kipindi cha mwisho wa karne ya kumi na tisa kilishuhudia ongezeko la idadi ya wageni wa mataifa ya Kimagaharibi waliongia barani Afrika. Christopher (1984) anasema kuwa ujio wa mataifa ya Ulaya barani Afrika, ulihusisha mataifa mbalimbali yaliyokuwa katika ushindani kati ya moja na jingine. Awali, lengo kuu la mataifa haya lilikuwa shughuli za kibiashara. Baadaye, mataifa haya yalianza kung'ang'ania rasilimali za bara la Afrika; hali iliyosababisha haja ya kuligawa bara la Afrika. Kuligawa bara la Afrika kirasmi kulifanyika katika mkutano wa Berlin mwaka wa 1884 (Kiruthu, Kapiyo na Kimori, 2011). Hata hivyo, ugawaji huu licha ya kuwa wa manufaa kwa wakoloni, ulihasiri bara la Afrika. Kulingana na Thuranira (2017), harakati hizo za kuligawa bara la Afrika ziliendeleza dhuluma na ukandamizaji kwa wenyeji.

Kipindi cha ukoloni barani Afrika kilishuhudia matatizo chungu nzima miongoni mwa Waafrika. Matatizo haya yalikuwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kichumi, wakoloni walihimiza ubinafsi ulioambatana na unyanyasaji. Kijamii, wakoloni walipuuza tamaduni za Waafrika. Aidha, kisiasa utawala wa kikoloni uliathiri miundo ya utawala ya

Kiafrika.Wakishadidia hili, Wilfred na Martin (1970) wanasema kuwa masuala kama vile ushuru, ajira ya kulazimishwa na unyakuzi wa ardhi kwa matumizi ya wakoloni, ndio uliokuwa msingi wa upingaji wa utawala wa kikoloni katika miongo miwili ya kwanza ya ukoloni barani Afrika.

Hatimaye, mataifa ya Afrika yalipopata uhuru, viongozi na wananchi walikuwa na hamu ya kuwa na jamii isiyokuwa na matatizo waliyoshuhudia katika kipindi cha ukoloni. Hata hivyo, baadhi ya mambo yaliyotakiwa kutekelezwa hayakutekelezwa. Ni mazingira kama haya ya kihistoria, kisiasa na kijamii ambayo huathiri mtunzi kifani na kimaudhui. Akishadidia hili, Masinde (1992) anasema kuwa mtunzi hupata tajriba yake kutokana na maisha yake pamoja na mazingira yake.

Hatimaye, mataifa ya Afrika yalipopata uhuru, viongozi na wananchi walikuwa na hamu ya kuwa na jamii isiyokuwa na matatizo waliyoshuhudia katika kipindi cha ukoloni. Hata hivyo, baadhi ya mambo yaliyotakiwa kutekelezwa hayakutekelezwa. Ni mazingira kama haya ya kihistoria, kisiasa na kijamii ambayo huathiri mtunzi kifani na kimaudhui. Akishadidia hili, Masinde (1992) anasema kuwa mtunzi hupata tajriba yake kutokana na maisha yake pamoja na mazingira yake.

Madhumulla (1988) anaeleza kwamba matukio fulani hujitokeza zaidi kuliko mengine katika kila kipindi cha maisha. Baadhi ya matukio haya, huigusa jamii kwa uzuri au ubaya. Tukio linapokuwa hivyo, huwa mada kuu na muhimu kwa miaka mingi baadaye.

Katika kushadidia kauli ya hapo juu, Mlacha (1984) anaeleza kwamba historia ya kipindi fulani cha utunzi ni muhimu katika utunzi wa kazi ya kifasihi ukiwemo ushairi. Akirejelea taifa la Tanzania, Nasimiyu (2016) anabainisha kwamba sera zilizobuniwa baada ya

uhuru, hususa Azimio la Arusha la 1967, zililenga kuvunja nguzo za ukoloni za ubepari na kujenga ujamaa, kuondoa utabaka, unyonyaji na dhuluma kwa kujenga Tanzania kiuchumi na kisiasa ili kukomesha uonevu, ukanadmizaji, utumwa na umaskini. Aidha, lengo kuu lilikuwa kujenga Tanzania mpya yenye usawa na haki na isyo na utabaka Hivyo, watunzi wa Tanzania katika miaka ya 1970 na kuendelea walitunga kazi zao kwa njia ya kuhakiki na kutathmini kufaulu kwa malengo ya Azimio la Arusha.

Washairi wa Kiswahili wana nafasi mbalimbali katika jamii, kama vile kukashifu uovu. Wametambua kwamba maisha si jana na leo tu, bali pia kuna kesho ambayo lazima ifanyiwe matayarisho kwa kutumia leo. Hamu ya mtunzi ni kuiumba jamii mpya kulingana na namna anavyoyaona matatizo yanayoikumba jamii yake (Mlacha 1984). Kwa vile fasihi ni kama kioo cha jamii na ushairi kama taswira au vivuli vyetu kwenye taswira hiyo, utunzi humulika ule urazini wa jamii husika katika kipindi husika.

Mshairi wa Kiswahili amekuwa na uhusiano wa aina mbalimbali na jamii yake. Hivyo, kumetokea washairi wenye kuelezea uhusiano huu, pamoja na matarajio ya jamii zao katika nyakati tofauti (Masinde, 2003). Kwa mfano, katika shairi *Jipu* kwenye diwani ya *Sauti ya Dhiki*, Abdalla *(1973)* anaeleza kuhusu dhiki anayoipitia kutokana na jipu. Neno jipu limetumika kijazanda kumaanisha matatizo ya kisiasa hasa kutokana na juhudi zake za kupinga utawala wa kipindi hicho uliojaa udhalimu. Katika shairi hili, anaendelea kueleza imani na matarajio yake kuwa ipo siku ambayo jipu hilo litatobolewa. Kwamba itakuwa siku ya furaha. Katika shairi la *Bara Jingine* katika *Diwani ya Bara Jingine*, Mberia (2001) anaeleza matarajio yake ya kupata bara jipya lilioendelea kiuchumi. Hata hivyo, anawalaumu viongozi hasa wabunge ambao baada ya kuchaguliwa na wananchi,

wanatumia nafasi hiyo kujitajirisha na kupuuza maslahi ya wananchi. Anawafananisha na genge la nzige ambao kwa kawaida wanajulikana kama wadudu waharibifu ambao hula bila kusaza. Hivyo, hakuna fasihi ulimwenguni ambayo imechimbuka katika ombwe tupu. Huwa imepata uhai wake, miongozo na hata maudhui yake kutokana na hali ya kitamaduni, kisiasa na kiuchumi ya jamii hiyo

Hamu ya utafiti huu ilitokana na sababu kwamba kila kazi ya fasihi inaweza kuelezwa katika muktadha wa utunzi ambapo inakita katika kipindi maalumu cha historia. Aidha, watunzi katika kipindi fulani cha historia hushughulikia masuala ya aina fulani na huongozwa na thamani za aina moja pamoja na sababu kuwa huwa na sifa za kipekee (Peck na Coyle.1984:2). Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu ulishughulikia harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko.

### 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya*.Utafiti ulijikita katika utanzu wa ushairi kwa kuwa ni utanzu mkongwe ambao umetumikia jamii kwa njia mbalimbali katika nyakati mbalimbali za kihistoria. Aidha, utanzu huu ni maarufu katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, katika jamii ya sasa, ushairi unatumika katika nyanja kama vile tamasha za mziki shuleni, utumbuizaji katika sherehe mbalimbali, hukaririrwa katika vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii. Kutokana na umaarufu huu, utanzu wa ushairi wa Kiswahili umeweza kuwa njia muhimu katika harakati za kuleta mabadiliko katika jamii.

Aidha, utafiti huu ulichochewa na sababu kwamba utungo wa fasihi huwa na chanzo chake katika maisha ya binadamu katika mazingira yake maalumu ya kihistoria, kiuchumi

na kijamii. Masinde (2024) anaeleza kwamba msanii kwa mara nyingi huzoa mawazo kutoka jamii anamoishi. Washairi wa Kiswahili wamesawiri masuala ya jamii zao tofauti kubainisha mielekeo ya jamii zao na mtarajio pia.

Kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu suala la kubadilisha jamii. Kwa mfano Kimeu (2016) alichunguza Maudhui ya ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti. Naye Ndung'u (2019) alichunguza usawiri wa vijana katika ujenzi wa jamii mpya katika riwaya teule ya Kiswahili. Kadri mtafiti ajuavyo, hakuna utafiti ambao umeshughulikia harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko kwa kutumia diwani teule, malengo, maswali ya utafiti, mbinu za utafiti na mkabala ambao umetumika katika utafiti huu.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni :

*a)* Kubainisha miktadha iliyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya.*

b) Kueleza harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya.*

c) Kuonyesha umuhimu wa harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko kwa jamii ya sasa.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

*a)* Ni miktadha ipi iliyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya?*

*b)* Je, ni harakati zipi za kujenga jamii yenye mabadiliko zinazodhihirika katika *Diwani ya Karne Mpya?*

c) Harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko zina umuhimu gani kwa jamii ya sasa?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Hamu ya mtunzi wa kazi ya kifasihi huwa ni kuiumba jamii yake upya kufuatana na jinsi anavyoona matatizo yanayoikabili. Kwa mujibu wa King'ei (2000), fasihi nzuri ni ile ambayo huhimiza, huboresha au kuimarisha ujenzi wa jamii imara. Hivyo basi, kuna haja ya kuchunguza namna ushairi wa Kiswahili unavyotimiza dhima hii ya kazi za fasihi.

Mazingira ya mtunzi huwa ni muhimu katika utunzi wa kazi yake. Huwa ni malighafi ya kusawiri ujumbe kwa njia ya ubunifu. Katika utunzi wake, mtunzi huwa na nia ya kuichora jamii yake jinsi ilivyo. Hivyo, kuna haja ya kuchunguza miktadha ambayo mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* yametungiwa kwa lengo la kujenga jamii yenye mabadiliko.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa jamii nyingi za Afrika Kenya ikiwemo, zimekumbwa na matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii baada ya kupata uhuru, na hasa

katika Karne ya ishirini moja. Kwa hivyo, kuna haja ya kuchunguza matatizo haya na kuyaweka wazi pamoja na kuangazia harakati za kupambana na matatizo haya kwa lengo la kujenga jamii yenye mabadiliko.

Aidha, mtunzi huishi katika jamii na huwa na wadhifa fulani wa kutekeleza katika jamii hiyo. Anaweza kuchambua matatizo halisi ya jamii yake katika kipindi fulani, kuonyesha chanzo cha matatizo hayo, kupendekeza suluhisho kwa kuwa na msingi wa uadilifu (Kiango, 1993: ix).Kwa hivyo, kuna haja ya kuchunguza umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya* baada ya kuchunguza matatizo yanayoikumba jamii pamoja na miktadha iliyoibua matatizo hayo.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulishughulikia harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Mashairi yaliyotafitiwa ni yaliyo katika *Diwani ya Karne Mpya*. Aidha, ni mashairi ya watunzi kutoka nchi ya Kenya. Mashairi haya ni 'Kumekucha', 'Tazama', 'Niguse', 'Msitu ni Ule Ule', 'Tujenge Nti Wananti', 'Kuno Kunena', 'Mchochole', 'Kilio cha Afrika' 'Mihadarati Shuleni', 'Kesho Yangu', 'Mtu na Utu', 'Muwerevu Hajinyoi', 'Ajali Ikidhihiri', 'Mavazi', 'Elimu Adhimu', 'Kuteleza Siku Hizi', 'Kwenda Mbio Si Kupata,' 'Tutakula Nini?', 'Kila Mpenda Haramu', 'Jikanye', 'Mkesha wa Mwaka Mpya,' 'Siolewi', 'Kibaruwa' 'Ngoma za Leo', 'Ndoto Mbaya,' 'Limwengu tofauti', 'Amani', 'Watuonavyo', 'Kijiji cha Mauji', 'Mwanangu Nakuusia', 'Hofu za Binadamu', 'Nilipokuwa Tajiri' na 'Moyo Iwa na Subira'. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa ushairi kwa sababu ya umaarufu wa matumizi yake hasa katika jamii ya sasa. Utafiti ulishughulikia miktadha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyoibua harakati za

ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Aidha, uliangazia harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko katika diwani hii pamoja na umuhimu wa harakati hizo.

*Diwani ya Karne Mpya* iliteuliwa kimakusudi kwa kuwa na data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti huu. Diwani hii ni ya hivi karibuni.

Utafiti huu ulijikita nchini Kenya. Hii ni kwa sababu nchi ya Kenya imeshuhudia matukio mbalimbali ya kihistoria baada ya kupata uhuru na matukio hayo yameathiri utunzi wa mashairi kimaudhui.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu suala la kuibadilisha jamii. Miongoni mwa wale ambao wametafiti kuhusu suala hili ni Manoti (2012). Alishughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika *Upotevu.* Manoti anaainisha makundi kadhaa ya uovu ambayo ni pamoja na uovu wa kimatendo, uovu wa kiadili, uovu wa kimetafizikia, uovu wa mwonoulimwengu na uovu wa kijamii. Anaendelea kuweka aina hizi zote za uozo katika makundi mawili ambayo ni uozo wa kiadili na uozo kiasilia. Anabainisha athari kadhaa zinazowakumba wanajamii kutokana na aina hizi za uovu. Uchanganuzi wa uozo na athari zake katika utafiti wa Manoti ulifaa utafiti huu katika kuelewa miktadha hasi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyochochea harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika mashairi teule kwenye *Diwani ya Karne Mpya*. Utafiti wa Manoti unatofautiana na huu kimalengo. Hii ni kwa sababu kando na kuchunguza miktadha hasi inayoghasi wananchi, utafiti wa Manoti ulichunguza harakati za kujikomboa ambazo ndizo harakati za kuijenga jamii yenye mabadiliko kwa mujibu wa utafiti huu. Utafiti wa Manoti umetumia Nadharia ya Maadili ambayo hulenga kuchanganua sababu ya matendo

kuonekana mema au maovu. Hii ni tofauti na utafiti huu ambao ulitumia nadharia ya Uhistoria Mpya ambayo huchunguza uhusiano uliopo kati ya historia na jamii. Utafiti wa Manoti pia umetumia utanzu wa riwaya ilhali huu ulijikita katika utanzu wa ushairi.

Kiongera (2012) alichunguza mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia teule. Katika utafiti wake, alionyesha maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayozua migogoro na yanayohitaji kubadilishwa. Uchanganuzi wa maovu haya ulifaa utafiti huu katika uelewekaji wa miktadha ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iliyochochea harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Aidha, mikakati iliyotumika na vijana katika kukabiliana na maovu haya, ilisaidia utafiti huu katika ubainishaji wa harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko zinazodhihirika katika mashairi teule katika *Diwani ya Karne Mpya*. Utafiti wa Kiongera (2012) ulijikita katika utanzu wa tamthilia ambapo alihakiki tamthilia nne teule zilizochapishwa katika mwongo wa kwanza wa Karne ya ishirini na moja. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu huu ulijikita katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili.Utafiti wa Kiongera pia ni tofauti na huu kinadharia, kimalengo na hata kiupeo.

Njoroge (2014) alichunguza viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatiah: *Vipanya vya Maabara* na *Majira ya Tufani*. Anasema kuwa viongozi ndio husababisha matatizo yanayozikumba jamii za leo. Viongozi anaowarejelea ni wa nyanja zote za kisiasa, kiuchumu na hata kijamii. Anaendelea kusema kwamba japo wengine hawakufaulu, wananchi katika jamii za *Vipanya vya Maabara* na *Majira ya Tufani* walijitetea kwa kukaidi. Utafiti wa Njoroge (2014) ulisaidia huu katika kuchanganua matatizo yanayozikumba jamii. Aidha, ulifaa katika kubainisha harakati za

kujikomboa dhidi ya matatizo hayo katika mashairi teule. Utafiti wa Njoroge unatofautiana na huu kimada. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulichunguza harakati za ushairi za kujenga jamii yenye mabadiliko chanya ilhali utafiti wa Njoroge ulichunguza mchango wa viongozi katika kuleta mabadiliko hasi katika jami

Osango (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alishughulikia ukombozi wa kisiasa na kiuchumi katika *Mkamadume*. Lengo lake lilikuwa kudhihirisha hali za wananchi kiuchumi na kisiasa na ndoto zao baada ya uhuru wa bendera visiwani Zanzibar na Pemba. Anasema kuwa hali ngumu za kiuchumi na kisiasa ndizo zinazowafanya Waafrika kuamua kupigania uhuru wao wakiwa na matarajio kuwa hali ingebadilika na kuwa nafuu. Aidha, anaeleza harakati za ukombozi zinazotumiwa na Waafrika katika shughuli ya ukombozi. Utafiti wa Osango (2015) ulisaidia huu katika kubainisha miktadha ya kiuchumi na kisiasa iliyochochea hamu ya kutaka mabadiliko katika jamii. Aidha, ulisaidia katika uchanganuzi wa harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko zinazobainika katika mashairi teule katika *Diwani ya Karne Mpya*. Utafiti wa Osango unatofautiana na huu kwa kuwa umetumia mihimili ya Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ilhali huu uliongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uhistoria Mpya. Isitoshe, utafiti wa Osango (2015) umejikita katika riwaya ilhali huu ulijikita katika ushairi. Utafiti wa Osango pia unatofautiana na huu, kimada, kimalengo na hata kiupeo.

Nasimiyu (2016) alichunguza athari za mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Dhifa*. Anaeleza kwamba chanzo cha utungo wa fasihi ni maisha ya binadamu pamoja na mazingira yake maalum ya kihistoria, kiuchumi na

kijamii. Aidha, anaeleza namna mabadiliko ya kijamii na kihistoria yalivyoathiri utunzi wa mashairi kifani na kimaudhui. Maudhui anayoyashughulikia katika mazingira mbalimbali ni ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Utafiti wa Nasimiyu ulifaa huu katika uchanganuzi wa miktadha kijamii, kiuchumi na kisiasa. Utafiti wake pia umetumia Nadharia ya Uhistoria Mpya ambayo ilitumika katika utafiti huu. Hili lilifaa utafiti huu katika uelewekaji na utumizi wa nadharia ya Uhistoria Mpya. Hata hivyo, kimalengo utafiti wa Nasimiyu unachunguza kwa ujumla maudhui yanayoibuliwa na mazingira mbalimbali ya kihistoria na kijamii katika diwani ya *Dhifa*. Kwa upande mwingine, utafiti huu ulijikita katika namna miktadha halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii inavyochochea harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya*.

Ndung'u (2019) alichunguza usawiri wa vijana katika ujenzi wa jamii mpya katika riwaya teule ya Kiswahili. Lengo lake kuu lilikuwa ni kuonyesha mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii ya *Kidagaa Kimemwozea*. Aidha, ametumia nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii.Utafiti wa Ndung'u ulifaa huu katika kubainisha mabadiliko chanya yanayohimizwa na mashairi teule katika *Diwani ya Karne Mpya*.Utafiti wa Ndung'u (2019) ni tofauti na huu kimada, kimalengo, kinadharia, upeo na hata kiutanzu.

Ndung'u (2022) alibainisha kuwa, matukio ya kihistoria yameathiri waandishi wa riwaya za *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba* katika uwasilishaji wa maudhui ya kazi zao. Matukio haya ya kihistoria yanajumuisha miongoni mwao masuala kama vile uongozi, siasa na vita vya baada ya uchaguzi nchini Kenya. Alibainisha namna matukio hayo halisi

yalivyoathiri kazi za watunzi wa *Nyongo Mkalia Ini* na *Mafamba*. Aidha, amebainisha juhudi za wananchi za kujikomboa dhidi ya masuala kama vile usaliti wa viongozi na uongozi mbaya. Utafiti wa Ndung'u ni muhimu kwa utafiti huu katika uchanganuzi wa /matukio halisi katika miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia, utafiti wa Ndung'u umeongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya ambayo ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Hili lilichangia katika uelewekaji wa misingi na mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya. Utafiti wa Ndung'u ni tofauti na huu kimada, kimalengo, kiupeo na kiutanzu.

Kutokana na mapitio ya tafiti za awali, ni dhahiri kuwa kadri mtafiti ajuavyo, tafiti za awali hazijalenga namna miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa inavyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadilko katika diwani teule. Hivyo, palikuwa na pengo lililohitaji kuzibwa na utafiti huu.

### 1.8.0 Misingi ya nadharia ya Uhistoria Mpya

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya. Nadharia ya Uhistoria Mpya ni mojawapo ya matapo mawili ya Uhistoria (Uhistoria Mkongwe na Uhistoria Mpya). Tofauti na Wana-uhistoria Mkongwe, Wana-uhistoria Mpya husawiri matukio ya wakati uliopita katika muktadha wa wakati uliopo. Kwa upande mwingine, Wana-uhistoria Mkongwe husawiri matukio katika wakati uliopita. Nadharia ya Uhistoria Mpya iliasisiwa na Stephen Gleeblatt katika miaka ya 1980 na kushika kasi katika miaka ya 1980. Kwa mujibu wa Gleenblatt (1980) mahitaji ya kijamii na kisiasa huathiri utoaji na upokezi wa kazi za kifasihi. Kwa hivyo, kipindi ambacho kazi ya fasihi iliandikwa ni

muhimu. Aidha, kipindi anachoishi mhakiki wa kazi ya fasihi kina umuhimu katika uhakiki wa kazi hiyo.

Nadharia ya Uhistoria Mpya ina misingi yake katika mawazo ya Raymond Williams na Foulcault (1972, 1977, 1997). Wahakiki hawa wanatambua umuhimu wa muktadha wa kihistoria katika kazi za kifasihi. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhistoria Mpya, kazi zote za fasihi na zisizo za fasihi zina mzunguko wa kimwingiliano. Nadharia hii pia hutazama kipengele cha jamii pamoja na utamaduni wake. Kulingana na Veeser (1989), kazi zote za fasihi ni sawa. Kwa hivyo, hakuna kazi bora zaidi ya nyingine. Hii ni kwa sababu waandishi na wahakiki wa kazi za fasihi huwa wameathiriwa na mazingira yao. Nadharia ya Uhistoria Mpya imekuwa na mchango mkubwa katika kueleza miktadha ya fasihi ya kihistoria. Tunaweza kuzielewa kazi za kifasihi kwa kuangalia hali na athari za mabadilishano ya kitamaduni ambayo huzaa kazi hiyo (Wamitila, 2003). Hii ni kwa sababu matukio ya kihalisia ama ya kijamii, kisiasa, kihistoria au kiuchumi ndiyo ambayo huzalisha fasihi. Isitoshe, jamii ndiyo hujenga mazingira ya usomaji na uhakiki wa kazi ya fasihi.

Kwa mujibu wa Nasimiyu (2016), Nadharia ya Uhistoria Mpya hushughulikia umuhimu wa muktadha katika utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi. Aidha, nadharia hii huweka mkazo kwenye njia ambazo zinaweza kutumiwa kuijenga au kuisawiri tena jana au historia. Wana-Uhistoria Mpya huhimiza uchunguzi juu ya jamii halisi inayozalisha fasihi katika mazingira na wakati maalum. Maelezo haya yalisaidia katika kuchunguza miktadha ambayo imeibua mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya*. Mazingira ya mtunzi huathiri utunzi wake na hivyo athari hizi huwa zinajitokeza katika kazi yake. Akishadidia

hili, Mlacha (1984) anasema kuwa utunzi wa kazi za kifasihi huathiriwa pakubwa na historia ya kipindi cha utunzi wa kazi hizo. Kwa hivyo, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kazi ya fasihi na muktadha wa kijamii. Hii ni kwa sababu kazi hiyo imetokana na muktadha wa kijamii bali haitoki katika ombwe tupu.

Kimsingi, nadharia ya Uhistoria Mpya hueleza uhusiano uliopo baina ya fasihi na historia, Aidha, hutambua kuwa kazi za fasihii huathiriwa na mazingira ya kihistoria na kiutamaduni. Pia kazi hizo huathiri mazingira hayo kwa njia mbalimbali. Isitoshe, kazi hizi hujenga na kubadilisha historia. Ni kutokana na maelezo haya ambapo baadhi ya mihimili ya nadharia hii imetumika katika utafiti huu.

### 1.8.1 Mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya

Mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya ni kama ifuatayo :

1. Kazi zote za kubuni zina miktadha ya kijamii ambayo ina mahusiano yanayoingiliana. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza miktadha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa iliyochochea utungaji wa mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya.*

2. Kazi za kifasihi hazitokani na ubunifu wa mwandishi peke yake bali ni matokeo ya uhusiano changamano wa mwingilianomatini. Mhimili huu ulikuwa muhimu katika uchanganuzi wa mashairi katika Diwani ya Karne Mpya, kama zao la watunzi wa jamii mahususi ambapo pana uchangamano wa maendeleo ya fasihi, utamaduni, masuala ya kihalisia ya kijamii pamoja na ya kihistoria.

3. Kusudi la mwandishi wa fasihi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria ya kazi inayohakikiwa pamoja na jamii husika. Mhimili huu ulisaidia kuhakiki na kubainisha harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko kama unavyobainika katika mashairi teule katika *Diwani ya karne Mpya* pamoja mbinu zinazotumika katika harakati za kuleta mabadiliko katika jamii

4. Muktadha na chimbuko la kazi ya fasihi huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi. Mhimili huu ulitumika katika kuonyesha vitengo mbalimbali vya umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko kutokana na uhakiki na ufasiri wa mashairi teule katika *Diwani ya Karne Mpya.*

5. Suala la miktadha na utamaduni wa kijamii lazima liangaliwe upya. Hii ni kwa sababu ujumi, mielekeo, maongozi, urazini na thamani za jamii hubadilika kulingana na maendeleo ya jamii. Mhimili huu ulitumika kuhakiki na kuonyesha umuhimu wa harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko

### 1.9.0 Mbinu za utafiti

Sehemu hii imeshughulikia ; muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo

### 1.9.1 Muundo wa utafiti

Kombo na Tromp (2006) wanasema kuwa muundo wa utafiti hurejelea aina ya utafiti utakaofanywa. Utafiti huu utachukua muundo wa kimaelezo. Muundo huu ulitumika kuelezea miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ambamo mashairi katika *Diwani ya*

*Karne Mpya* yametungiwa. Aidha, ulitumika katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi, pamoja na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti

### 1.9.2 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na mtandaoni. Maktabani mtafiti alisoma vitabu, majarida, makala na tasnifu mbalimbali kwa lengo la kufanikisha utafiti wake. Aidha, machapisho yanayohusiana na mada yalisomwa kwa lengo la kuimarisha suala la utafiti huu. Tasnifu zilisomwa kwa lengo la kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu suala la kujenga jamii yenye mabadiliko. Vilevile, vitabu vilisomwa kwa lengo la kuweka upeo na mipaka ya utafiti. Mtafiti pia alisoma vitabu na makala yanayohusiana na nadharia iliyotumiwa katika utafiti. Mashairi katika diwani teule yalisomwa na kuchanganuliwa ili kubainisha miktadha na harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko pamoja na umuhimu wa harakati hizo katika jamii ya sasa. Mtandaoni, tovuti zilizohusiana na mada ya utafiti zilisakuriwa na data kusomwa na kuchanganuliwa ili kupata data mwafaka kuhusu miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa iliyoathiri untunzi wa mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya*.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya utafiti huu ilteuliwa kimakusudi. Kulingana na Orodho (2005), usampulishaji wa kimakusudi ni ambapo mtafiti hufanya uteuzi wa moja kwa moja wa idadi ndogo iliyo na sifa zinazohitajika katika utafiti wake. Mashairi thelathini na matatu katika *Diwani ya Karne Mpya* yaliteuliwa kimakusudi kwa misingi kuwa yametungwa na watunzi kutoka nchi ya Kenya katika miongo tofauti na kwamba, mashairi hayo yalikuwa na data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Data iliyotumiwa katika utafiti huu, ilikusanywa kwa kusoma kwa kina mashairi katika diwani teule na kunukuu sehemu ambazo zilikuwa na data iliyohitajika kulingana na malengo ya utafiti. Aidha, mtafiti alisoma na kuyahakiki majarida, vitabu, tasnifu na machapisho yanayohusiana na mada. Mtafiti pia alisakura kwenye tovuti kwa lengo la kupata data iliyohusiana na utafiti huu.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Kabla ya kuichanganua, data ya utafiti huu ilipangwa kimfumo kwa kuzingatia malengo ya utafiti kisha data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa kuzingatia mashairi yaliyodhihirisha miktadha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Aidha, utafiti ulizingatia mashairi yaliyoangazia harakati za kuijenga jamii yenye mabadiliko pamoja na umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Uchanganuzi uliongozwa na malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, pengo lililonuiwa kuzibwa na utafiti na mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari pamoja na utoaji wa mifano mwafaka.

Utafiti huu unatarajiwa kuchangia katika uhakiki wa fasihi kinadharia. Pia, unatarajiwa kuifaa jamii katika kuelewa harakati mwafaka za kuleta mabadiliko chanya katika jamiii na manufaa yake.

### 1.9.7 Maadili

Utafiti huu umezingatia taratibu mwafaka za maadili. Mtafiti alipata ruhusa ya kufanya Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta. Aidha, mtafiti alipata kibali cha kufanya Utafiti kutoka kwa NACOSTI.

### 1.9.8 Kiishilio

Sura hii ilishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti yaliyoanfikwa kuhusu mada misingi na mihimili ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti. Sura inayofuata ilishughulikia miktadha iliyoibua harakati za kuleta mabadiliko katika jamii.

# SURA YA PILI

# MIKTADHA ILIYOIBUA HARAKATI ZA KULETA MABADILIKO KATIKA JAMII

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilijadili miktadha ambayo iliibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhistoria Mpya, matukio ya kihalisia ama ya kijamii, kisiasa, kihistoria au kiuchumi ndiyo ambayo huzalisha fasihi. Kwa hivyo, sura hii ilichunguza miktadha halisi ya kijamii, kihistoria na kisiasa ambayo iliibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya*. Sura hii iliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya Uhistoria Mpya. Kwamba, kazi zote za kubuni zina miktadha ya kijamii ambayo ina mahusiano yanayoingiliana. Mhimili wa pili ni kuwa, kazi za kifasihi hazitokani na ubunifu wa mwandishi pekee bali pia ni matokeo ya uhusiano changamano wa mwingiliano matini. Sura hii pia ilionyesha namna watunzi katika *Diwani ya Karne Mpya* wameshughulikia masuala ya kihalisia yanayoingiliana. Aidha, ilionyesha namna watunzi hawa walivyoathiriwa na mazingira yao katika utunzi wa kazi zao. Kabla ya kujadili miktadha halisi iliyoibua harakati za kuleta mabadiliko katika jamii, muhtasari wa *Diwani ya Karne Mpya* ulishughulikiwa.

## 2.3 Muhtasari wa Diwani ya Karne Mpya

*Diwani ya Karne Mpya* ni mkusanyiko wa mashairi; mengi yakishughulikia masuala ya kimamboleo. Masuala haya yanahusu maisha ya binadamu hasa ya baada ya uhuru wa mataifa ya Afrika. Masuala haya ni pamoja na siasa, elimu, ukengeushi, umaskini,

utabaka, ukoloni mamboleo, uongozi na ufisadi. Mashairi haya yametungwa na watunzi kutoka nchi mbili za Afrika Mashariki (Kenya na Tanzania). Ni watunzi ambao wameathiriwa na mazingira walimojipata na hivyo kusawiri masula halisi katika jamii. Ingawa diwani hii ina mashairi ya watunzi kutoka nchi mbili, mashairi yaliyochanganuliwa katika utafiti huu, ni yale yaliyotungwa na watunzi wa Kenya katika kipindi cha Karne ya ishirini na karne ya ishirini na moja. Mashairi haya yalihaririwa na Ken Walibora na kuchapishwa katika *Diwani ya Karne Mpya* mwaka wa 2007.

### 2.4 Miktadha iliyoibua harakati za kuleta mabadiliko katika jamii

Kwa mujibu wa Wana-Uhistoria Mpya, kazi ya fasihi haitokani na ombwe tupu. Manoti (2012) anasema kuwa kazi za kifasihi hutungwa katika muktadha wa jamii maalumu ili kuonyesha welewa na utambuzi wa mitagusano na matukio ya jamii. Mtunzi hutunga kutegemea namna anavyosawiri mazingira yake. Sanja (2012) anasema nguvu za kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kidini humwathiri msanii na ndiyo maana hushawishika kuandika. Miktadha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyojadiliwa katika sehemu hii, ilisaidia kubainisha namna watunzi mbalimbali walivyoathiriwa na hali mbalimbali za jamii. Aidha, ilionyesha namna watunzi walivyomulika na kuelewa uhalisia katika jamii zao.

#### 2.4.1 Miktadha ya kisiasa

Miktadha ya kisiasa iliyobainika katika mashairi ya watunzi mbalimbali ni: Vipindi vya uchaguzi na siasa, ukoloni mamboleo, ufungwa na uongozi mbaya

#### 2.4.1.1 Vipindi vya uchaguzi na siasa

Baada ya nchi ya Kenya kupata uhuru kutoka kwa Waingereza mwaka wa 1963, kumekuwepo na chaguzi mbalim vbali. Vipindi vya chaguzi hizi vimeshuhudia patashika ambazo zimeathiri utunzi wa kazi za sanaa mojawazo ikiwa ni ushairi. Baadhi ya mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* yametungwa katika muktadha huu. Mfano ni shairi *Kumekucha* (uk.24) la Adilatif Abdalla. Mtunzi wa shairi hili anadhihirisha furaha na matumaini yake baada ya uchaguzi. Licha ya kupata uongozi mpya, anawahimiza wananchi kukumbuka hali mbaya ya hapo awali ili wasije wakasahau na kurudi katika hali hiyo. Anasema:

> *Kumekucha! Imengiya asubuhi! Kumekucha! Siku imepambazuka!*
> *Kumekucha! Wote umma tufurahi, miale ya juwa yamulika*
> *Kumekucha! Itwambae ikirahi, na nyoyo ziwe kutukunduka*
> *Kumekucha! Mbingu zapiga siyahi, na ardhi nayo piya yatibwirika!*
> *Kumekucha! Kwanukiya njema rihi, si ya ule uvundo wenye kunuka*
> *Kumekucha! Mwishowe 'metanabahi, giza limetishika na kutimika!*
> *Kumekucha! Ni kwamba 'mekosa zihi, Jogoo leo limeshindwa kuwika!*

Mtunzi anaonyesha kufurahia jamii mpya kiutawala baada ya kipindi kirefu cha utawala wa kiudhalimu. Mtunzi anatumia kauli "kumekucha" kwa maana ya mapambazuko mapya. Aidha, ametumia maneno *rihi* na kauli kama vile 'uvundo wenye kunuka' katika mshororo wa tano kuashiria hali ya kuvutia kinyume na ya hapo awali iliyojaa uovu. Kulingana na Ndwiga (2013) katika muktadha huu, rihi ni sitiari ya hali mpya na nzuri ya kisiasa nchini iliyotarajiwa kuleta mabadiliko mema katika taifa. Anaendelea kusema kuwa uvundo wenye kunuka ni sitiari ya uozo na udhalimu uliotambulisha utawala wa chama husika. Mtunzi ametumia kauli hizi mbili kujenga taswira ya hali ya utawala unaoondoka na ile ya utwala unaoingia. Pia amezitumia kulinganisha vipindi viwili vya

kiutawala. Mtunzi anasema “giza limetishika na kutimika” kwa maana kuwa kipindi cha utawala mbaya kimetamatika. Kwa mujibu wa Walibora (2007), shairi hili lilitungwa baada ya uchaguzi mkuu wa Kenya (Disemba2002) ambapo Wakenya waliupigia kura kwa wingi muungano wa vyama vya upinzani, NARC. Kutokana na kitendo hicho, chama cha KANU, ambacho kilikuwa kimetawala kwa miaka 40 kilishindwa. Kutokana na maelezo haya, ni haki kusema kuwa mtunzi wa shairi hili alichochewa na muktadha wa kisiasa hasa kabla na baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchi Kenya.

Katika shairi ‘Msitu ni ule ule ‘(uk.29) la Omar Babu (Abu Marjan), mtunzi anaangazia siasa potovu ambazo huendelezwa na viongozi hasa wakati wa kampeni za uchaguzi. Anasema:

*Vigogo waumbuane, matayo pasi sumile*
*Na mara watukanane wapigizane kelele*
*Eti kisa twondokane, na ya uhasama ndwele*
*Bado mwitu ule ule, na fisi ni wale wale*

*Sikuye wapapurane, maguvu waamilile*
*Muda wasisemezane, ja mhasimu wa kale,*
*Wakae wasikizane, warejee pale pale*
*Kwani mwitu ni ule ule, na fisi ni wale wale*

Katika beti hizi mtunzi anaonyesha namna viongozi hutenganisha wananchi wakati wanajitafutia uongozi. Wakishapata uongozi, viongozi hao huungana kuwanyanyasa wananchi kwa kuongozwa na tamaa bali si kuwatumikia wananchi. Kwa mfano, anasema,” Eti kisa twondokane, na ya uhasama ndwele.” Mtunzi anarejelea hali ya uhasama kama ndwele kwa kuwa ni hali ambayo inaishia kuwasababishia wananchi maafa. Mtunzi pia anasema, “wakae wasikizane, warejee pale pale,” kwa maana kuwa hatimaye viongozi huungana na kuendeleza uovu dhidi ya wananchi kama awali. Huu ni unafiki na usaliti wa hali ya juu.

Beti hizi zinapiga mwangwi maelezo ya, Ajulu (1998) anaposema:

> *"Kwa hivyo kulingana na matendo yao ya kisiasa kwa miaka saba ambayo imepita, viongozi wa upinzani wamedhihirisha kuwa hawana tofauti na KANU ambacho ndicho shina ambalo vyama vyote vimeibuka" (Tafsiri yetu)*

Ajulu (1998) anashadidia kauli ya mtunzi kuwa, "mwitu ni ule ule, na fisi ni wale wale" kwa maana kuwa japo wakati wa kutafuta kura viongozi wa upinzani hutaka kuonekana kuwa bora, hawana tofauti na wale viongozi wa chama tawala. Wote wametoka katika chama kuu kimoja na hivyo matendo yao ni sawa. Mtunzi anawafananisha viongozi hawa na fisi anaposema, "na fisi ni wale wale". Kwa kawaida fisi hufahamika kwa tamaa yake.

**2.2.1.2 Ukoloni mamboleo**

Katika kipindi cha ukoloni nchini Kenya, wakoloni waliwanyanyasa na kuwadhulumu Waafrika hasa kwa kuwatumikisha. Kulingana na Mwiribua (2014), ukoloni mamboleo ni aina ya mfumo wa kisiasa unaoendelezwa na nchi zenye nguvu katika nchi maskini. Nchi zenye nguvu huingilia mifumo ya nchi maskini. Kisiasa, kiuchumi na hata kitamaduni. Hali hii inadhihirika nchini Kenya kwa kuwa hata baada ya kuondoka, wakoloni waliendeleza mfumo wao. Waliendeleza mfumo huo kupitia kwa viongozi waliochukua usukani baada ya uhuru nchini Kenya. Hivyo, ikawa hakuna tofauti kubwa kati ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Tofauti iliyoko ni kwamba wanaouendeleza ukoloni ni Waafrika ambao wanatumika kama vibaraka wa nchi zilizoendelea (Ndung'u, 2013). Aidha, viongozi wa Afrika huwadhulumu Waafrika wenzao kwa kutumia njia zilezile tu za kidhalimu zilizotumiwa na wakoloni. Baadhi ya

mashairi katika *Diwani ya karne Mpya* yametungwa katika muktadha huu wa ukoloni mamboleo. Katika shairi 'Kilio cha Afrika' (uk.36) la Alamin Mazrui anasema:

*Tazameni miji ikinyongeka*
*kwa magugu ya ubepari*
*na madhila yakituzika*
*yapita yakijikariri.*

Katika mshororo wa pili, mtunzi ametaja 'magugu ya ubepari' kwa maana ya hali ya uzungu weusi unaoendelezwa na viongozi wa Afrika waliochukua uongozi baada ya kuondoka kwa wakoloni. Viongozi hawa wanaendeleza utawala ule ule wa udhalimu na unyanyasaji kwa Waafrika.Thuranira (2017) akishadidia hoja hii anasema:

> ''Kabla ya mkoloni kuondoka, alijiundia tabaka la wenyeji lilikokuwa na mwelekeo na tabia kama zake ili kuendeleza kuendeleza ukoloni mpya."

Katika kipindi cha ukoloni, wakoloni waliendeleza dhuluma na unyanyasaji dhidi ya Waafrika kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, walinyakua mashamba ya Waafrika na kuwalazimisha Waafrika kufanya kazi katika mashamba hayo kwa mshahara duni. Aidha, waliendeleza ubaguzi wa rangi dhidi ya Waafrika. Manoti (2012) anasema kuwa serikali ya kikoloni iliwatendea Waafrika maovu kwa kutumia mabavu na vitisho kama njia ya kuwafanya raia wake kutenda mambo. Tabia hizo za kuwadhulumu Waafrika ndizo zilizoendelezwa na waafrika waliochukua uongozi. Ndiposa katika ubeti wa tatu mtunzi anasema, "na madhila yakituzika, yapita yakikariri." Kwa maana ya matatizo mengi yasiyokwisha yanayowakumba wananchi. Matatizo haya bila shaka yanaendelezwa na viongozi waliochukua uongozi baada ya uhuru.

Katika shairi ‘Watuonavyo!’(uk.119) la Paul Nabiswa, mtunzi anaeleza uhusiano uliopo kati ya nchi za Afrika na Wazungu. Anasawiri uhusiano huu kama wa dharau, matusi na kejeli. Anaonyesha kukerwa na kuchukizwa na mtazamo wa Wazungu kuhusu Waafrika. Katika ubeti wa tatu mtunzi anasema:

*Taswira ya huku kwetu, kwao ni bara jeusi*
*Waongeza utukutu, kudai yetu meusi*
*Waona tunayo kutu, nyingi kupita kiasi*
*Ama kwetu kila kitu, ni nduli kama kisasi.*

Katika ubeti huu, mtunzi analalamikia hali ya Wazungu kudharau na kudunisha Waafrika.Mtunzi anasema. “Taswira ya huku kwetu, kwao ni bara jeusi.” Kumaniisha kuwa kulingana na Wazungu, Afrika ni bara la wajinga. Aidha,”waona tunayo kutu nyingi kupita kiasi,”kumaanisha kuwa wanaona Waafrika wakiwa wenye upumbavu mwingi kupindukia. Huku ni kudharau Waafrika hali ambayo imechangiwa na kasumba za kikoloni. Mtunzi anaendelea kusema, “Ama kwetu kila kitu ni nduli kama kisasi,” kumaanisha kuwa, kulingana na Wazungu kila kitu cha Waafrika ni kibaya. Kulingana na Ndwiga (2013), Wazungu huwaona Waafrika kama wakaazi wa bara jeusi. Yaani bara lilojaa ujinga na kuwa nyuma kimaendeleo. Kauli ya Ndwiga inalingana na mawazo ya Hegel (1975) anayedai kuwa bara la Afrika halijasonga wala kudhihirisha maendeleo. Huu ni ufahamu mbaya kuhusu tamaduni na asasi mbalimbali za Waafrika. Ni dhahiri kuwa mawazo yake yalichochewa na kasumba za kikoloni dhidi ya bara la Afrika.Katika ubeti wa tano wa shairi hili, mtunzi anasema:

*Mmetutia unyama, kusema sisi tumbili*
*Siku nyingi mmesema, sisi hatuna akili*
*Mwatuchukulia kama, hatuwezi uwakili*
*Ndiposa ninawauma, kwa matatu na mawili.*

Ubeti huu unaonyesha kiasi ambacho Wazugu waonavyo Waafrika. “Kusema sisi tumbili,” kumaanisha kuwa Waafrika hawana tofauti na tumbili. Yaani Waafrika ni kama wanyama kwa kuwa hawana akili. Kwa maana kuwa ni wajinga. Aidha anasema, “hatuwezi uwakili,” kumaanasha kuwa Waafrika hawana uwezo wa kutathmini wema na uovu.

Kulingana na Hegel (1975), Mwafrika ni mfano wa mtu mnyama kulingana na hali yake ya ushenzi na utovu wa sharia. Kauli kama hizi zinadhihirisha dharau na udunishwaji wa Waafrika. Pia ni kauli potovu kwa kuwa hata kabla ya ujio wa wakoloni, Waafrika walikuwa wamejiendeleza katika asasi mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na hata kijamii.

#### 2.2.1.3 Ufungwa

Baada ya Wakenya kupata uhuru mwaka wa 1963, walitarajia kuwa hali ya maisha yao ingeimarika. Hali ilienda kinyume na matarajio yao na ndiyo sababu baadhi wakaanza kuikosoa serikali. Juhudi hizi zao zilipelekea baadhi yao kufungwa chini ya utawala wa Rais mwanzilishi wa taifa Mzee Jomo Kenyatta na Rais wa pili wa taifa Kenya Daniel Arap Moi. Muktadha huu wa ufungwa ndio uliochochea baadhi ya watunzi kutunga. Ingawa walifungwa, hali ya ufungwa haikufifisha juhudi zao (Hamadi, 2017). Mmoja wa watunzi hao ni Alamini Mazrui. Katika shairi ’Niguse’ (uk.28) anasema:

*Nitokapo kizuizini*
*Nitamwomba yeyote mwendani*
*Aniguse*
*taratibu*
*polepole*
*lakini*
*kwa yakini*
*Niguse tena*
*Unijuze tena*
*Unifunze tena*
*maisha yalivyo*
*maisha yaonjavyo*
*ladha ilivyo*

Katika mshororo wa kwanza ubeti wa kwanza mtunzi anasema "Nitokapo kizuizini" kumaanisha kuwa ni mfungwa. Alamini Mazrui alifungwa katika kipindi cha utawala wa Moi.Alifungwa pamoja na wenzake sita kwa kosa la kuwafundisha wanafunzi umuhimu wa wananchi wazuri. Hamadi (2017) anasema kuwa, Alamini Mazrui akiwa gerezani, kwa ujasiri na usiri wa hali ya juu na kwa kutumia Biblia na kalamu alitoa hasira zake dhidi ya udhalimu uliopo. Kando na kutoa hasira zake, alieleza matumaini yake ya kufunzwa tena kuhusu maisha pindi atokapo kizuizini kama inavyodhihirika katika shairi lake,'Niguse'.

Shairi 'Kuno Kunena' (uk.34) la Abdilatif Abdalla, ni mojawapo ya mashairi yaliyo katika diwani yake ya *Sauti ya Dhiki.* Abdilatif Abdalla aliandika mashairi yaliyo katika diwani hii akiwa kizuizini. Sababu ya kufungwa kwake ni kuwa aliunga mkono chama cha KPU kilichopinga utawala wa Rais Jomo Kenyatta na kuandika Makala iliyoitwa *Kenya: Twendapi?* Anasema:

> *"Sababu ya kufungwa ni kwamba nilipatikana na 'hatia' ya kuchochea watu kuipindua serikali ya Kenya kwa kutumia silaha baada ya kuiandika, kuichapisha na kuisambaza, kwenye miji kadha wa kadha ya Jimbo la Pwani la Kenya, karatasi niliyoiitwa Kenya: Twendapi?"(Abdilatif, 2012)*

Katika ubeti wa kwanza wa shairi 'Kuno Kunena', mtunzi anasema:

> *Kuno kunena kwa nini, kukanikomeya kuno?*
> *Kwani kunena kunani, kukashikwa kani vino?*
> *Kani sio na kiini, kuninuniya mno*
> *Kanama nako kunena, kwaonekana ni kuwi*

Kwa mujibu wa ubeti huu inadhihirika kuwa mtunzi alikuwa anashangaa kwa nini kunena kwake kukaonekana ni kubaya kiasi cha kumtia mashakani. Kunena anakorejelea ni harakati zake za kisiasa, hasa kuandika makala ya *Kenya: Twendapi,* pamoja na nyinginezo zilizosababisha kufungwa kwake. Anaweka wazi hali ilivyokuwa katika kipindi cha utawala uliokuwepo. Hali hii inaonyesha kuwa kuwa Rais Moi aliendeleza mfumo wa kiudikteta ambao haukukubali mawazo yalioelekea kupinga serikali. Akishadidia hili, Manoti (2012) anasema kuwa wazo jipya katika uongozi usiojali maslahi ya wengi huchukuliwa kuwa ni uzushi na ukiukaji wa sheria. Kwa mujibu wa ubeti ulionukuliwa hapa, mawazo ya Abdlilatif Abdalla ndiyo yaliyopelekea kufungwa kwake. Yalipoonekana kuwa ni uzushi na uchochezi. Ni katika muktdha huu wa kufungwa ndipo alipotunga ili kueleza hisia zake kupitia ushairi.

Shairi 'Moyo iwa na subira' (uk.133) ni jingine ambalo Abdilatif Abdalla alitunga akiwa kifungoni. Katika shairi hili, mtunzi kupitia kuunenea moyo wake, anabainisha dhiki anazozipitia pale kifungoni; baadhi zikiwa ni upweke na huzuni. Ni dhiki hizi ambazo zinaufanya moyo wake kulia na hivyo anautuliza kuunasihi uwe na subira.

Katika ubeti wa nne anasema:

*Usiwe kama mkiwa, moyo wangu changamka*
*Kwani myonge ukawa, na matama kujishika*
*Ng'ara mfano wa juwa, uwate kuhuzunika*
*Sijiuwe kwa mashaka, zidi kuwa na subiri.*

Katika ubeti huu, mtunzi ambaye ndiye mfungwa, anaukanya moyo wake kuwa na upweke wala kujiuhurumia. Badala yake anauhimiza kuchangamka. Aidha, anauhimiza kutojiua kutokana na dhiki ambazo unazipitia. Ni ubeti unaodhihirisha kuwa hali ya pale gerezani ilikuwa ya kuhuzunisha na kukatiza tamaa. Mtunzi anasema:

*Moyo kwamba halikuwa, ulilolitarajiya*
*Lisikupe kuingiwa, na simanzi na kuliya*
*Hivyo ndivyo mambo huwa, ni kama lumbwi duniya*
*Shika n'nalokwambiya, zidi kuwa na subira*

Kwa kusema, "halikuwa ulilolitarajiya", mtunzi anamaanisha kuwa kupitia machapisho yake ya Kenya: *Twendapi*, alitarajia kuwa serikali ingeona ukweli wala si kumfunga jela. Anaendelea kuuhimiza moyo wake kutoingiwa na huzuni kwa kuwa dunia ndivyo huwa. Kwamba, dunia hubadilika kama vile kinyonga. Utarajialo silo ambalo huwa.

Katika ubeti wa kumi na mbili, mshororo wa kwanza mtunzi anasema, "Huwezi kuligeuza, lililolekeya kuwa." Hii ni sauti ya kutuliza moyo ili asiendelee kusononekea hali yake. Ndiyo maana katika mshororo wa tatu ubeti huo huo anasema, "Ufaalo kufanyiza, omba uwe na afuwa." Kwamba la maana sasa ni kuomba awe na afya kwa kuwa hakuna jingine la kufanya. Muktadha wa kufungwa ndio uliochochea shairi hili linalosawiri hali na dhiki apitiayo mfungwa pale gerezani; kwa sababu ya harakati za kupigania mabadiliko.

#### 2.2.1.4 Uongozi Mbaya

Uongozi mbaya ni hali ya viongozi kutotumia mamlaka ipasavyo. Njoroge (2014) anasema kuwa, sifa za uongozi mbaya ni kinyume na sifa za uongozi mzuri. Anaeleza baadhi ya sifa za uongozi mzuri kuwa ni uwezo wa kutovumilia wanaotumia uwezo wao kiholela pamoja na kugundua na kukabiliana na ufisadi pasipokujali umaarufu na cheo cha wenye hatia.

Uongozi mbaya hudhihirika kwa namna mbalimbali kama vile ufisadi, tamaa, udhalimu, unyanyasaji na ubadhirifu wa mali ya umma. Tungo kadhaa katika *Diwani ya Karne Mpya*, zimetungwa katika muktadha huu wa uongozi mbaya wa utawala wa viongozi watatu wa kwanza tangu uhuru nchini Kenya. Kwa mfano, katika shairi la ‘Kila Mpenda Haramu’ (uk.62) la Muchai Bin Chui, mtunzi anasema:

*Namba nanyi mlo wima, mliopewa jukumu*
*Mlioajiri umma, kupenda kutudhulumu*
*Kuna siku ya kiyama, ameipanga Rahimu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

Katika ubeti huu mtunzi anawalenga viongozi ambao baada ya kupewa mamlaka waliwadhulumu wananchi. Katika mshororo wa kwanza mtunzi anasema, “Namba nanyi mlo wima, mliopewa jukumu” kumaanisha ananena na walionavyo hasa waliopewa nafasi za uongozi. Anaendelea kuwaonya kuwa ipo siku iliyopangwa na Mungu nao mabaya yatawapata. Mtunzi, alizaliwa mwaka wa 1970. Ameshuhudia kwa ukamilifu utawala wa viongozi wawili (Rais Daniel Arap Moi na Rais Mwai Kibaki) kabla ya uchapishwaji wa *Diwani ya Karne Mpya.* Utawala wa viongozi hawa pia haukuwa na tofauti kubwa na ule wa Rais wa kwanza, Jomo Kenyatta. Ulijaa ufisadi, usaliti, dhuluma

na unyanyasaji miongoni mwa maovu mengine. Akirejelea uongozi wa Moi, Mohamed (2015) anasema kuwa uongozi wa Moi ulitawaliwa na mapuuza, ukingaji wa wahalifu kwa sababu za kisiasa pamoja na uundaji wa makundi haramu na ya kibinafsi ya usalama. Anaendelea kusema kuwa, hata baada ya utawala wa Rais Moi, serikali ya Rais Kibaki haikufanikiwa kutatua tatizo la ardhi. Maelezo ya Mohamed yanaonyesha kuwa baadhi ya matatizo yaliyoshuhudiwa katika utawala wa Moi, bado yalikuwepo katika utawala wa Kibaki.Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa muktadha huu wa uongozi mbaya ulichochea utunzi wa shairi 'Kila Mpenda Haramu.'

Katika shairi 'Tazama' (uk.25) la Wamitila ubeti wa tatu mtunzi anasema:

*Tazama tena, kisha utaona*
*Wanasiasa wanaojisifia kwa maendeleo*
*Mawaziri wanaorereja sifa za sera za nchi yao*
*Wanadini wanaoimba kwa kupagawa*
*Na kiongozi anayejisifia kipaji cha kuona mbele.*

Katika ubeti huu, mtunzi anakashifu majisifu ya viongozi ambao huishia kusaliti matumaini ya wananchi. Viongozi hawa wanajisifu kwa maendeleo, sera za nchi pamoja na kipaji cha kuona mbele. Sifa hizi ni za kupumbaza wananchi ili wasitambue hila zao. Katika mshororo wa nne mtunzi anasema, "Wanadini wanaoimba kwa kupagawa" kumaanisha kuwa wananchi hawatambui kinachoendelea.

Baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2002, wananchi walitarajia kuwa maisha yao yangebadilika chini ya utawala wa Rais Mwai Kibaki. Hata hivyo matumaini yao yalisalitiwa kwa sababu mambo yalisalia kuwa vile vile.

Katika shairi ‘Ndoto Mbaya’ (uk.101) la Mogambi, mtunzi anaeleza kuhusu ndoto aliyoota kuhusu tabia za viongozi. Kwamba ni wenye ubinafsi, tamaa, wanyanyasaji na watovu wa utu.Katika ubeti wa kwanza mtunzi anasema:

*Jana niliota*
*Ndoto ya uchoyo*
*Uchoyo wa ukuu*
*Ukuu wa kuwanyanyasa wengi*
*Ndoto mbaya ya jinamizi*
*Wanaowala watu wengi wakicheka*
*Wanaokula wakilalama njaa*
*Wanawameza wakiwa hai wazimawazima.*

Katika mshororo wa tatu anasema “uchoyo wa ukuu” kwa maana kuwa wana ubinafsi wa uongozi.

Kwamba waajiona ndio tu wanaofaa kuongoza. Hata hivyo, ubinafsi huu wao ni wa kunyanyasa wananchi na kuwadhulumu. Akisisitiza tamaa ya viongozi hao mtunzi anasema, “Wanaowala watu wengi wakicheka” kumaanisha wanawanyanyasa huku wakiwadhihaki. Katika mshororo wa sita mshairi anaeleza tamaa iliyopindukia. Anasema, “Wanaokula wakilalama njaa” kumaaisha kuwa hawatosheki kamwe. Katika mshororo wa mwisho anasema kuwa wanawameza wakiwa hai. Hii ni tamaa, udhalimu na ukatili wa hali ya juu.

Hali hii inalingana na mawazo ya Ajulu (1998). Anasema kuwa, tukio la Kenya linawakilisha hali ambapo tabaka la viongozi liliamua kusalia uongozini kwa kila namna. Maelezo haya yanaonyesha wazi hulka ya viongozi wa Kenya; hasa viongozi wa kisiasa ambao wamejaa tamaa ya uongozi na ubinafsi.

### 2.2.2 Miktadha ya kijamii

Baadhi ya mashairi yanayoibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko, yametungwa katika miktadha ya kijamii. Miktadha hii inahusisha mambo kama vile, maradhi, utabaka, elimu, ukengeushi na ndoa za mapema.

#### 2.2.2.1 Utabaka

Utabaka ni hali ya kutolingana katika makundi ya kijamii. Kausi (2022) anasema kuwa, utabaka ni hali ya wahusika kuwa na hadhi na madaraja tofauti katika jamii kutokana na misingi ya kiuchumi na kisiasa. Madaraja haya yameshuhudiwa nchini Kenya kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na hata baada ya ukoloni. Kutolingana kwa nafasi kati ya makundi ya kijamii kumebakia kuwa jambo sumbufu katika maisha nchini Kenya leo hii (Njoroge, 2014). Ni katika muktadha huu wa utabaka ambapo baadhi ya watunzi katika *Diwani ya Karne Mpya* wametungia mashairi yao. Katika shairi 'Tazama' (uk.25) mtunzi anasema:

*Tazama utaona,*
*Maskini wanoishi katika dhiki za karne*
*Fukara wanodidimia katika kinamasi cha dhuluma*
*Fakiri wanogugunwa mili na michonge wa tabaka*
*Wakiwa wanokufa njaa kwa kukosa cha kujilia*

*Tazama kisha utaona,*
*Vitambi vinavyotetemeshwa na uto wa nyama*
*Shingo zinazoshabihiana na mibuyu ya pwani*
*Mili iliyonenepeana tamthili ya kiboko*
*Vinywa vinavyokula na kusaza kwa wingi*

Ubeti wa kwanza unasawiri hali ya kimaskini ya tabaka moja na ubeti wa pili unaweka wazi hali ya kitajiri ya tabaka jingine. Tabaka la kimaskini linasawiriwa kama linalokumbwa na dhiki tele. Katika ubeti wa kwanza mshororo wa nne mtunzi anasema, "Fakiri wanogugunwa mili" kumaanisha kuwa maskini wamekonda. Hawana afya. Aidha, maskini hao wanakufa kwa sababu hawana chakula. Kwa upande mwingine, tabaka la matajiri linasawiriwa kama liloshiba na lenye miili mikubwa kama kiboko. Pia matajiri hawa wanakula na kusaza. Beti hizi zinaweka wazi pengo kubwa liliko kati ya matabaka mawili. Akishadidia hoja hii, Njoroge (2014) anasema, kutolingana kwa nafasi ya makundi ya kijami kumebakia kuwa jambo sumbufu katika maisha nchini Kenya. Beti hizi ziadhihirisha kuwalicha ya kupata uhuru, migawanyiko ya kitabaka inaendela kushuhudiwa. Aidha, maisha ya wananchi wengi hayajaboreka.

Pia katika shairi 'Kilio cha Afrika' (uk.36) la Alamini Mazrui, muktadha wa utabaka unajitokeza. Katika ubeti wa nne mtunzi anasema:

*Engani kiza kilojitandika*
*tabaka zilo dhahiri*
*Afrika ikipepesuka*
*kwa pepe zilovinjari*

Katika ubeti huu, mtunzi anatuchorea taswira ya tabaka zilizomo Afrika. Katika mshororo wa kwanza anasema, "Engani kiza kilojitandika." Ametumia "kiza" kumaanisha hali mbaya iliyotawala. Hali yenyewe ni ya utabaka ambao unadhihirika wazi katika bara la Afrika. Anasema, "tabaka zilo dhahiri," kumaanisha kuwa suala la utabaka linaonekana wazi barani Afrika. Utabaka huu umesababisha maafa barani Afrika. Katika mshororo wa

tatu mtunzi anasema, “Afrika ikipepesuka” kwa maana kuwa Afrika inayumbayumba. Yaani mambo yameharibika.

Muktadha huu wa utabaka pia unadhihirika katika shairi ‘Ulimwengu tofauti’ (uk.116) la Timothy M. Arege. Anasema:

*Sebuleni niliketi*
*Mapema moja jioni*
*Nikaanza kumbo kuupiga*
*Mlima wa ugali*

*Mboga na nyama nikatowelea*
*Kabla ya maziwa mafunda kupiga*
*Na maji kuteremsha, koo kusafisha*

*Nilipozinduka nilikuta changu kisaduku*
*Macho kikiwa, habari kinamwaya*
*Ndipo nikaona wenzangu wananchi*
*Mizizi wakila na matunda mwitu*
*Vyote wakivisaka kwa taabu*

Beti hizi zinatuchorea picha ya wananchi katika tabaka mbili. Kuna wale wanaokula vinono kama vile mboga, ugali na maziwa. Kwa upande mwingine kuna wananchi ambao wanakula mizizi na matunda mwitu. Katika ubeti wa tatu anasema, “Nilipozinduka nilikuta changu kisanduku,” kwa maana kuwa, kando na kuwa na chakula cha kutosha, matajiri wanapata muda wa kupumzika. Pia wanamiliki vyombo vya kujistarehesha kama vile runinga (kisanduku). Hali hii ni kinyume na ilivyo kwa maskini ambao hawana chakula na kile duni wapatacho, wanakipata kwa tabu. Ni shairi ambalo linaweka wazi pengo la kitabaka lililoko katika jamii. Pengo hili ni kubwa kiasi inaonekana kana kwamba matabaka haya yamo katika ulimwengu tofauti. Yaani, kila moja limo katika ulimwengu tofauti na jingine.

Mtunzi katika ubeti wa mwisho anaendelea kusema:

*Nikashangaa tulivyoishi*
*Chini ya bendera moja*
*lakini tukiwa mbalimbali*
*Katika limwengu tofauti*
*kama ardhi na mbingu.*

Katika ubeti huu mtunzi anashadidia mwanya mkubwa wa kitabaka ulioko katika jamii, kiasi kwamba anaulinganisha na ule wa umbali wa ardhi na mbingu. Kwa mujibu wa Makala ya World Bank (2007), utabaka ungali tatizo nchini Kenya. Katika mwaka wa 2003, ilielekezwa kuwa karibu asilimia hamsini na sita ya familia nchini Kenya ziliishi maisha ya kimaskini. Hii ni idadi kubwa sana ya wananchi walio katika tabaka la maskini ikiliganishwa na tabaka la matajiri.

Katika shairi, 'Hofu za binadamu' (uk.130) la Kinene wa Mutiso, mtunzi anagusia suala la utabaka katika ubeti wa kwanza. Anasema:

*Hofu za wanyonge, ni nguvu za matajiri*
*Ambazo zinawaponda, wanapotaka usawa*

Ni ubeti unaoweka wazi namna matajiri wanavyoendelea kuweka mpaka kati yao na maskini. Katika ubeti huu, mtunzi anaonyesha namna matajiri huwakandamiza maskini watakapo haki yao ya usawa. Hivyo, maskini huishia kuishi katika hali ya woga na hili huwapa matajiri nguvu zaidi

### 2.2.2.3 Ndoa za Mapema

Kwa miaka kadhaa, serikali ya Kenya pamoja na washika dau wengine, imekuwa ikipiga vita ndoa za mapema hasa miongoni mwa wasichana wadogo walio chini ya miaka kumi na minane. Baadhi ya wanaounga mkono ndoa hizi si kwamba hawajui ni kinyume cha

sheria bali ni mapuuza tu. Kwa mfano, kulingana na ripoti ya UNICEF (2017) takribani asilimia 85 ya wasichana na wanawake wa asili ya Maasai, 55 ya Somali, 89 ya Samburu, 59 ya Pokot na 90 ya Rendile walioshirikishwa katika utafiti, walikiri kuwa walifahamu kuwa ndoa za mapema ni kinyume kwa mujibu wa sheria ya Kenya. Ndoa hizi za mapema huathiri maisha yao kama vile kuacha masomo na hata kutotimiza ndoto zao maishani.

Katika shairi 'Siolewi' (uk. 78) la Douglas Mutua, mtunzi anasawiri suala la ndoa za mapema, nafsineni ambaye ni msichana wa shule, analalamikia kuozwa angali masomoni.

Mtunzi anasema:

*Nina habari kamili, naozwa hali nasoma,*
*Nalia sili silali, nakerwa na hino njama*
*Elimu kwangu halali, ndoa sitamani mama*
*Ninasoma siolewi!*

*Naihitaji elimu, japo mie msichana*
*Elimu nguzo muhimu, na yenye kubwa dhamana*
*Kwani kosa gani humu, kuzaliwa msichana?*
*Ninasoma siolewi!*

Beti hizi zinadhihirisha jamii ambayo inamsawiri mtoto wa kike kama chombo cha kuozwa huku matakwa yake yakipuuzwa. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza, anasema kuwa analia na kukerwa na hiyo njama ya kumuoza. Hii ni dhahiri kuwa anaozwa kinyume na mapenzi yake. Katika ubeti wa pili mshororo wa tatu anaendelea kueleza kuhemewa iwapo ni kosa kwake kuzaliwa msichana kwani jamii haithamini hata masomo yake. Katika mshororo wa tatu anasema, "Kwani kosa gani humu, kuzaliwa msichana?" Ni dhahiri kuwa analazimishwa kuolewa kwa kuwa inaonekana kuwa msichana hana thamani nyingine ila kuozwa.

#### 2.2.2.4 Matumizi Ya Dawa Za Kulevya

Suala la ulevi na matumizi ya dawa za kulevya limekuwa miongoni mwa matatizo sugu ya kijamii nchini Kenya hasa katika karne ya ishirini na ishirini na moja. Kulingana na ripoti ya NACADA (2007), matumizi ya dawa za kulevya ni mojawapo ya matatizo sugu ya kijamii nchini Kenya. Baadhi ya watunzi katika *Diwani ya Karne Mpya* walichochewa na hali hii na hivyo kuitungia mashairi. Katika shairi 'Mihadarati shuleni' (uk39) la Douglas Mutua, mtunzi anaeleza kuhusu matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana shuleni. Anasema:

*Taasisi zachafuka, hazikaliki jamani!*
*Moto mui unawaka, doria ashike nani?*
*Taifa lafadhaika, wana wawa maluuni*
*Mihadarati shuleni, yachangia machafuko.*

Ubeti huu unaweka wazi hali ya kutia wasiwasi kutokana na matumizi ya mihadarati shuleni ambayo imechangia machafuko katika jamii. Katika mshororo wa tatu, mtunzi anasema, "Taifa lafadhaika, wana wawa maluuni." Mshororo huu unadhihirisha kuwa wanaotumia mihadarati hii ni watu wa umri mdogo. Akishadidia hili, Manoti (2012) anasema kuwa mtego wa ulevi hauna ubaguzi kati ya wasomi na wasio wasomi, tajiri na maskini. Unawanasa wote kwa pamoja huku wasomi wakiuzamia zaidi. Hii ina maana kuwa, kiwango kikubwa cha wanaotumia dawa za kulevya ni wanaolewa madhara yake. Kwa hivyo, hata vijana walio shueni ni miongoni mwao.

Mtunzi anaendelea kusema:

*Uvamizi washafanya, walanguzi wa shuleni*
*kama jeshi la tekenya, linavamia wayoni*
*Silo lao 'kiwakanya, hawajali asilani*
*Mihadarati shuleni, yachangia machafuko*

Katika ubeti huu, mtunzi anaeleza kuhusu madhara ya matumzi ya mihadarati shuleni. Mojawapo ya madhara ya matumizi ya mihadarati ni uvamizi ambao unafanywa na walanguzi. Mtunzi anafananisha uvamizi huo na jeshi la tekenya wanaovamia wayoni. Kwa kawaida jeshi la tekenya livamiapo wayoni husababisha uchungu na kero. Zaidi, hukosesha amani.

Katika shairi 'Nashangaa Ikhuwani' (uk.115) la Muchui bin Chui, mtunzi anaeleza kisa cha kijana aliyefanikiwa kupata elimu na hatimaye kupata ajira yenye mapato mazuri. Hata hivyo, aliishia kujiingiza katika uraibu wa ulevi ambao ulimkengeusha. Katika ubeti wa mwisho wa shairi hili, mtunzi anasema:

*Kimwana muota ndoto, amesahau nyumbani*
*Anaitwa moto moto, hashindiki vilabuni*
*Hata siku za Sabato, hashughuliki fulani*
*Nashangaa ikhuwani,*

Ubeti huu unaonyesha namna ulevi umeathiri kijana aliyeonekana kufaulu maishani. Ulevi umechangia kufa kwa ndoto, kusahau nyumbani pamoja na siku ya Sabato, suala ambalo ni la kusikitisha.

### 2.2.2.5 Maradhi

Alipochukua uongozi mwaka wa 1963, Rais mwanzilishi wa Taifa la Kenya, Jomo Kenyatta, aliahidi kuwa angepiga vita adui watatu wa maendelo ya taifa wakati huo. Maadui hawa ni njaa, ujinga na maradhi. Ndiposa akaanzisha filosofia ya Harambee

ambapo mradi mmoja uliohimizwa na filosofia hii ulikuwa ni ujenzi wa hospitali. Filosofia ya Harambee iliungwa mkono na Rais Daniel Arap Moi aliyechukua uongozi mwaka wa 1978 hadi 2002 baada ya kifo cha Mzee Jomo Kenyatta. Alisema kuwa angefuata nyayo za Mzee. Hivyo basi, akaanzisha Filosofia ya Nyayo. Hata hivyo, miaka kadhaa baada ya uhuru maadui hawa hasa maradhi wanahangaisha wananchi. Ni katika muktadha huu ambapo watunzi kama vile Ken walibora katika shairi "Kesho Yangu" (u.k 41) wamezungumzia suala la maradhi yanayotishia maisha yake.

Anasema:

*Ukimwi nduguze wako, Ebola na Malaria*
*Kichomi na sekeneko, mno wajifaragua*
*Maadamu wangaliko, vipi kesho kuwazia*
*Kesho si ndugu yangu mwandani.*

Kwa mujibu wa ubeti huu, ni dhahiri kuwa nafsineni amekata tamaa ya kuishi kutokana na maradhi kama vile Ukimwi, Ebola, Malaria, Kichomi na sekeneko ambayo yanamzingira.

Haya yanaungwa mkono na ripoti ya utafiti wa Kingondu na Nordberg (2007) kuhusu magonjwa ya kuambukiza. Kutokana na utafiti wao, ugonjwa wa Ebola uliwaua watu mia mbili katika mpaka wa Uganda na Congo mwaka wa 2000. Aidha, uwezekano wa kuendelea kuishi kwa waathiriwa wa kichomi ni asilimia hamsini pekee. Kuhusu sekeneko, kufikia mwaka wa 1999 ugonjwa huu ulikuwa umeambukizwa watu milioni kumi na mbili ulimwenguni huku asilimia hamsini wakiwa kutoka mataifa yanaoyoendelea. Vilevile, utafiti wao unaonyesha kuwa ugonjwa wa Malaria huambukiza watu milioni 300 hadi milioni 500 kila mwaka ulimwenguni huku asilimia tisini wakiwa

kutoka mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara. Bila shaka nchi ya Kenya ni miongoni mwa mataifa haya. Ndiposa mtunzi wa shairi "Kesho Yangu" ambaye ni Mkenya (Ken Walibora) anadhihirisha wasiwasi kuhusu magonjwa haya katika shairi lake.

Katika shairi, 'Mkesha wa mwaka mpya' (uk. 69) la Paul Nabiswa, mtunzi anataja ugonjwa wa Ukimwi kama ugonjwa ambao ni janga katika taifa na kwamba linatisha.

Katika ubeti wa sita mtunzi anasema:

*Tarakimu zaonyesha, na ukimwi umezagaa*
*Ni mvua inanyesha, na kwa taifa ni baa*
*Ama kweli linatisha, ndiposa tunanyamaa*

Katika ubeti huu, mtunzi anafananisha kusambaa kwa ugonjwa wa Ukimwi na mvua inayonyesha. Hii ni kuonyesha namna ugonjwa huu unavyosambaa kwa kasi. Akishadidi hili, Ndwiga (2013) anasema, inakisiwa kwamba watu wazima elfu sitini na tano na watoto elfu ishirini na tano huambukizwa virusi vya ukimwi kila mwaka nchini Kenya huku watu zaidi ya elfu mia moja na hamsini wakifa kutokana na ugonjwa wa ukimwi kila mwaka nchini Kenya.

Takwimu hizi zinadhihirisha idadi kubwa sana ya Wakenya wanaougua na ile ya wanaoaga kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Idadi hii inatisha kama asemavyo mtunzi katika katika ubeti wa sita mshororo wa tatu, "Ama kweli linatisha". Katika ubeti wa tano mtunzi anaeleza kuwa kisababishi cha ugonjwa huu ni uzinifu wa mabinti na maghulamu hasa katika sherehe za siku ya mkesha wa mwaka mpya.

Kando na Ukimwi na maradhi mengine yaliyotajwa katika shairi 'Kesho yangu'. Katika shairi 'Mchochole' (uk.35) la Ahmed Darwesh, mtunzi anataja maradhi ambayo yanamhangaisha mtu ambaye ni maskini. Anasema:

*Maradhi tete kwa tele, huwa kwake uzoevu*
*Mara alia upele, mara alia na mbavu*
*Matibabu kupatile, bila pesa hana nguvu*

Mtunzi anataja magonjwa yamkumbayo maskini kama upele na kuumwa na mbavu. Katika mshororo wa tatu anasema, "Matibabu kupatile, bila pesa hana nguvu." Hapa mtunzi mtunzi anadhihirisha masikitiko yake kutokana na hali hii. Kwamba, ni vigumu kwa maskini kupata matiabu ya maradhi yamkumbayo

**2.2.2.6 Ubaguzi**

Ubaguzi ni tatizo ambalo limekuwepo hata tangu enzi za kabla ya ukoloni. Mayieka (2015) anasema kuwa ubaguzi ni hali ya upendeleo katika kuhudumia watu. Upendeleo huu unapofanywa kwa misingi ya rangi ya mtu, basi ni ubaguzi wa rangi. Katika shairi 'Watuonavyo' (uk.119) la Paul Nabiswa, mtunzi anagusia suala la ubaguzi wa rangi. Katika ubeti wa sita anasema:

*Msemo wa ngozi ngumi, ni nyinyi mliobuni,*
*Hata ikawalazimu, kulitia vitabuni*
*Kwenu hiyo ni hukumu, ya shina na mizizini*
*Mwatutenga kwa karamu, tadhani tuna tauni*

Katika ubeti huu, mtunzi analalamikia namna Waafrika wanavyotengwa na Wazungu. Kisa na maana ni ngozi yao. Katika shairi 'Kijiji cha Mauji' (uk.121) la K.W. Wamitila, mtunzi anagusia suala la ubaguzi. Anaeleza namna mataifa yaliyoendelea yanavyobagua mataifa yanayoendelea kwa misingi ya kiuchumi. Anasema:

*Tukiishi kwa dharau, na kwingi kubaguana*
*Tukaitana bahau, na huku twasukumana*
*Kunyang'anyana pilau, viwiko tukivunjana*
*Tuwe bado kijijini, kijiji cha aina gani.*

*Tukigeuzwa kasuku, kusifu kila uthori*
*Ndipo tupewe mwiku, kwa kuwa tu mafakiri*
*"Wengine wametupiku, kwa kuwa tu mafakiri!"*
*Tukubali haya kweli, kijiji chetu kimoja?*

Katika beti hizi, mtunzi anaonyesha kutoelewa kuwa ni vipi waseme kuwa ulimwengu ni kijiji kimoja ilhali kuna wale ambao wanawabagua wengine. Ubaguzi huu unafanywa kwa misingi ya kiuchumi. Aidha, mataifa maskini yanalazimika kusifu yaliyoendelea ili wapewe msaada. Msaada wenyewe ni wa bidhaa duni. Mtunzi anasema. "Ndipo tupewe mwiku, kwa kuwa tu mafakiri." Anamaanisha kuwa sababu yao kusifu uovu wa mataifa yaliyoendelea ni ili wapewe mabaki. Mataifa yanaoendelea yanapewa mabaki kwa kuwa wao ni maskini.

Katika shairi 'Kila mpenda haramu' (uk.62) la Muchai Bin Chui, mtunzi anagusia suala la ubaguzi wa kimamlaka. Anasawiri viongozi ambao wamepewa mamlaka ya kuongoza wengine na kuwaajiri lakini kwa kuwa wanapenda haramu, wafanyalo ni kudhulumu umma. Katika ubeti wa tano mshororo wa kwanza na wa pili anasema:

*Namba nanyi mlo wima, mliopewa jukumu*
*Mlioajiri umma, kupenda kutudhulumu*

Mtunzi anaonyesha viongozi wanaodhulumu wengine wasio na uwezo kama wao.

Katika shairi 'Siolewi' (u,k.78) la Douglas Mutua, mtunzi anasawiri ubaguzi wa kijinsia ambapo mtoto wa kike anaachishwa masomo ili aozwe ilihali wa kiume anaachwa kuendelea na masomo.Inazingatiwa kuwa masomo ya mvulana ni afadhali kuliko ya

msichana. Katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza, nafsineni ambaye ni msichana anasema, “Nahitaji elimu japo mie msichana” kuonyesha kuwa anajitetea katika jamii ambayo inambagua kwa misingi ya kijinsia. Katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza anasema, “Dhana kwamba mvulana, akisoma afadhali. “Kauli hii inaonyesha kuwa jamii inathamini elimu ya mtoto wa kiume na kuipuuza ile ya mtoto wa kike.

Hivyo,ni dhahiri kuwa mashairi haya yalitungwa katika muktadha wa ubaguzi; ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kiuchumi na ubaguzi wa kijinsia.

#### 2.2.2.7 Ukengeushi

Ukengeushi ni mabadiliko katika tabia ya mtu ambayo huenda kinyume na inavyotarajiwa. Mayieka (2015) anasema kuwa mabadiliko haya yanaweza kuwa ya kimaadili au kijamii. Anaendelea kueleza kuwa ukengeushi unadhihirika namna vijana wanavyojianika mitandaoni wakiwa wamevaa nguo zinazofichua uchi wao. Huu ni usasa ambao ni kinyume na utamaduni wa Kiafrika ambao husisitiza maadili. Akishadidia hili, Manoti (2012) anasema kuwa ukengeushi umeletwa na elimu ya wakoloni. Waafrika walikuwa na elimu yao na tamaduni zao. Hivyo basi ukengeushi umeathiri utamaduni wa Afrika. Baadhi ya watunzi katika *Diwani ya Karne Mpya* wametunga mashairi yao katika muktadha huu wa ukengeushi. Kwa mfano, shairi “Ngoma za Leo” (uk.97) la Timothy Arege. Katika shairi hili, mtunzi anaonyesha namna ambavyo ngoma za siku hizi zinavyokera kiasi cha kutoza machozi kwa sababu zimekosa makini na zinatia kiwewe.

Anasema:

*Hizi za leo zimekosa makini*
*Na kiwewe zinatia.*
*Kwa kila avutiwaye na mahadhi yake*
*Kila mpigo una siri*
*Kila mdundo una chambo*
*Kila mvuto una mtego*
*Kila mwondoko una telezi*

*Wengi hawajitosi tena ukumbuni*
*Kwa kuzichelea ngoma za leo*
*Wanasema: zinataka makini kuzivalia njuga*
*Maana, hawaziamini tena.*

Katika beti hizi, mtunzi anaonyesha shaka kuhusu ngoma za leo ambazo si kama za zamani. Mtunzi anasema kuwa ngoma za siku hizi zimeficha maovu. Mtunzi nasema, “kila mwondoko una telezi,” kwa maana kuwa, kila mwondoko umepujuka. Yaani, umepotoka kimaadili. Mtunzi anaendelea kusema kuwa, mtu anahitaji kuwa mwangalifu kabla ya kujitoma katika ngoma hizo.

Katika shairi.’Mavazi’ (uk.52) la Douglas Mutua, mtunzi anonyesha jinsi wanawake wamebadili namna wavaavyo na kuanza kuvaa mavazi yenye aibu kiasi kwamba viumbe wengine wameshangaa. Huu ni ukengeushi kwa sababu kulingana na tamaduni za Afrika, kuna mavazi ambayo mwanamke hafai kuyavaa hasa ya aibu. Katika ubeti wa pili mtunzi anasema:

*Samaki wanalalama, maziwani*
*Na nyuni wameachama, wa angani*
*Mahuluki wazizima, ardhini*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

Mtunzi ametumia chuku kusisitiza namna mavazi avaayo mwanamke hayaendani na tamaduni za jamii kiasi kwamba kila kiumbe ameshangazwa na hali hii. Katika ubeti wa

sita mshororo wa kwanza mtunzi anasema, "Vingine zitatuhama, tamaduni," kwa maana kuwa tusipovaa mavazi yenye heshima basi tutapoteza utamaduni hasa wa Afrika. Tamaduni za Kiafrika ni tofauti na zile za kigeni. Hivyo, asiyezingatia tamaduni izo huwa amekengeuka. Ni dhahiri kuwa, mtunzi wa shairi hili alichochewa na muktadha wa ukengeushi hasa kuhusu suala la mavazi ambayo hayendani na tamaduni za Kiafrika.

Akieleza kuhusu ukengeushi, Wafula (2015) anasema kuwa mtu hukosa kubainisha maisha yake yanakoelekea na hukosa kutambua kwamba mwenyewe anafaa kufasili matendo yake na uhusiano wake na watu. Aidha, mtu hujitenga na familia, jamii na mazingira. Hali hii inabainika katika shairi 'Nashangaa Ikhuwani' (uk.115) la Muchui bin Chui. Katika ubei wa tano anasema:

*Kimwana muota ndoto, amesahau nyumbani*
*Anaitwa moto moto, hashindiki vilabuni*
*Hata siku za Sabato, hashughuliki Fulani*

Mishororo hii inasawiri kijana ambaye ameenda kinyume na matarajio ya wanajamii kwa kupoteza mwelekeo wa maisha yake. Amesahau kwao na kuingilia ulevi pamoja na kuasi dini. Haya yote ni baada ya kupata elimu ya kigeni kama inavyoelezwa katika ubeti wa tatu. Mtunzi anasema:

*Akavisoma vidato, asikwae abadani*
*Kizungu akajuweto, Kidachi na Kijapani*
*Mwana akapata joto, hashindiki asilani.*

Elimu ya kigeni imesawiriwa kama chanzo cha ukengeushi. Ukengeushi unaelekea kuharibu maisha ya kijana ambaye wazazi wake walijitolea kumpa hiyo elimu ili asiwe mpumbavu. Mtunzi katika mshororo wa tatu ubeti wa pili anasema, "sije kuwa kipeto,

mpumbavu duniani.”  Ni muktadha huu wa ukengeushi uliochochea mtunzi wa shairi hili kusawiri chanzo cha ukengeushi.

### 2.2.3 Miktadha ya kiuchumi

Miktadha ya kiuchumi iliyobainika inahusu masuala ya: Umaskini, ubepari na dhuluma za kibepari.

#### 2.2.3.1 Umaskini

Umaskini ni hali ya kukosa vitu vya kimsingi au mali. Akieleza kuhusu dhana ya umaskini Osango (2015) anasema umaskini ni hali ya kutomudu kujipatia mahitaji mbalimbali ya kila siku kwa kiwango kinachoridhisha. Hali hii inaweza kujitokeza kwa namna nyingi kama vile ukosefu wa mavazi, makaazi, chakula na mambo mengine ya kimsingi. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia mwaka wa 2005, asilimia 19.7 ya Wakenya waliishi kwa dola 1.25 kwa siku au hata kidogo zaidi na kiwango cha asilimia 5.9 waliishi chini ya kiwango cha umaskini wa taifa. Baadhi ya mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* yamechora taswira ya hali hii ya umaskini nchini Kenya.

Katika shairi ‘Tazama’ (uk.25) la K. W Wamitila, mtunzi anaeleza kuhusu hali ya umaskini na matatizo yanayowakumba maskini. Katika ubeti wa kwanza mtunzi anasema:

*Tazama utaona,*
*Maskini wanaoishi katika dhiki za karne*
*Fukara wanaodidimia katika kinamasi cha dhuluma*
*Fakiri wanaogugunwa mili na michonge ya tabaka*
*Wakiwa wanokufa njaa kwa kukosa cha kujililia*
*Maskini wanoteswa kwa kuililia auni*
*Umma unaolia kwa kuikosa nafuu,*
*Kwa kupakosa pa kulala*
*Kwa kukikosa cha kuvaa*
*Kwa kuyakosa matibabu*
Kwa kuyakosa maisha

.

Kulingana na ubeti huu, maskini wamekumbwa na hali duni inayosawiriwa na vigezo kama vile, kukosa pa kulala, kukosa cha kuvaa, kukosa matibabu na kukosa maisha, ambako ni vifo. Taswira inayochorwa katika ubeti huu ni ya kukata tamaa. Hali hii inashadidiwa na ripoti ya Umoja wa Mataifa (2010). Kwa mujibu wa ripoti hii, umaskini na njaa ni changamoto kubwa nchini Kenya kama ilivyo kwa mataifa mengine. Aidha, huduma muhimu kama malazi, chakula na mavazi bado ni dhiki na wengi wakishindwa kumudu hata milo miwili kwa siku.

Katika shairi la ‘Mchochole’ (uk.35) la Ahmed Darwesh, mtunzi anazungumzia kuhusu masaibu ya mchochole yaani maskini. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza, mtunzi anasema kuwa mchochole amezongwa na matatizo kibao. Matatizo haya kama anavyoyaangazia katika shairi hili ni, kufungwa gerezani, njaa, malipo duni afanyapo kibarua, kukosa pesa za kugharamia masomo ya mwana wake pamoja na maradhi tele.

Anasema:

*Magerezani hufungwa, uhuni yeye anao*
*Mwenye njaa ametengwa kutengwa na washibao*

*Mchochole asemapo, atafuta kibarua*
*Mara chache apatapo, kilipacho sawasawa*
*Madogo huwa malipo kwa chakula kununua*

*Mchochole hana pesa malipokugharamia*
*Mwana aende Mombasa, kupata teknolojia*

*Mara nyingi mchochole, hukumbwa na maonevu*
*Maradhi tele kwa tele, huwa kwake uzoevu*

Kutokana na maelezo katika beti hizi, ni dhahiri kuwa maskini amekumbwa na matatizo chungu nzima; hasa tangu kupata uhuru. Matatizo haya ni pamoja na kufungwa, kulipwa malipo duni, kukosa pesa za kulipia elimu ya mtoto, maonevu na magonjwa chugu nzima. Katika ubeti wa mwisho wa shairi hili mtunzi anasema, "Mgawie yake keki, ya matunda ya uhuru." Hili linashadidia kuwa matatizo anayopitia mchochole ni baada ya nchi kupata uhuru. Ni kinaya kwamba badala ya uhuru kuleta natija, umewazidishia mashaka wanyonge.

Roodeny (1973) anasema kuwa, barani Afrika kiasi cha chakula kwa kila mtu kimekuwa kikienda chini katika miaka ya hivi karibuni. Hali hii inadhihirika katika shairi 'Limwengu tofauti' (uk. 116) la Timothy Arege.Anasema:

*Ndipo nikaona wenzangu wananchi*
*Mizizi wakila na matunda mwitu.*
*Vyote wakivisaka kwa taabu.*

Ubeti huu unasawiri hali ya umaskini ambayo wananchi wanaipitia. Kwa mfano, wanakula mizizi na matunda mwitu ambayo pia si rahisi kuyapata. Hii ni ishara ya hali ya umaskini uliokithiri.

#### 2.2.3.2 Ubepari na Dhuluma za Kibepari

Kwa mujibu wa Kamusi Teule ya Kiswahili (2019) ubepari ni mfumo wa kiuchumi ambao mtu anaruhusiwa kuchuma kiasi cha mali kutegemea uwezo wake. Hata hivyo, katika mfumo huu wenye uwezo au mamlaka zaidi huishia kukadamamiza walio katika tabaka la chini ili kujinufaisha wenyewe. Ni mfumo ambao umeshuhudiwa nchini Kenya hata baada ya kuondoka kwa wakoloni. Manoti (2012) anaeleza dhuluma kama maonevu, matendo yasiyo ya haki, ukatili, kudharauliwa, kuvunjiwa heshima na hata kupigwa. Dhuluma za kibepari basi ni dhuluma zinazoendelezwa na mabepari katika njia zao za kuchuma mali. Kausi (2021) anasema Waafrika waliochukua hatamu ya uongozi kutoka kwa mkoloni waliendeleza mbinu zile zile zilizokuwa za kibepari. Baadhi ya mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* yanathibitisha hili.

Katika shairi "Kibaruwa" (Uk.93) la Abdilatiff Abdalla, mtunzi anaangazia masaibu ambayo kibaruwa anapitia chini ya mwajiri wake. Kibarua analalamikia kurauka mapema kuzitema mbuga na kukwea minazi pamoja na kubebebshwa mizigo lakini apatacho ni malipo duni.

Mtunzi anasema:

> *Viulize: Ni nani araukaye na mapema kuzitema mbuga na kuzilaza?*
> *Viulize: Ni nani akweaye minazi tangu kuchapo hadi lingiapo giza?*
> *Viulize: Ni nani abebeshwaye mizigo hadi maungo yakageuka shaza?*
> *Halafuye hana faida moja apatayo wala malipo yanayotosheleza-*
> *Isipokuwa kusundungwa na kutupiwa matambara na vyakula vilivyooza?*
> *Viulize: Ni nani huyo ni nani!*

Ubeti huu unadhihirisha mfumo wa kibepari na dhuluma ambazo zinatumika kuuendeleza. Kwa mfano mtunzi anaeleza namna kibaruwa hubebeshwa mizigo kiasi kuwa maungo yake hugeuka shaza lakini apatacho ni malipo duni, matambara na vyakula vilivyooza. Hii ni kumaanisha kuwa mwajiri wake hana utu, wala hajali haki ya kibaruwa muradi yeye (mwajiri) anapata faida.

Ubepari unadhihirika pia katika shairi 'Kijiji cha Mauji' (uk.121) la K.W. Wamitila.

Anasema:

*Bidhaa za jalalani, barani tukitupiwa*
*Na mazao ya shambani, sisi tukilanguliwa*
*Uthori us'o kifani, kwao tukilaumiwa*
*Vipi isemwe ikawa, tumo kijiji kimoja?*

*Na sayansi kuchezewa tuwe sisi ni vifaa*
*Kila ovu kufamyiwa, huku nasi twanyamaa*
*Iwe tunasaidiwa, tuepukane na baa*
*Nani asemaye ikawa, twaishi sote pamoja.*

Beti hizi zinadhihirisha namna utegemezi wa nchi za Afrika umepelekea Waafrika kunyanyaswa na mataifa yaliyoendelea. Mfano, Waafrika wanapewa bidhaa zisizofaa pamoja na kuibiwa mazao yao. Aidha, mtunzi anaeleza namna Waafrika wanavyotumika kama vifaa vya majaribio ya kisayansi na kama malipo wanapewa misaada ati wanasaidiwa. Kapiyo na wenzake (2011) wakishadidia hili, wanasema mataifa ya Ulimwengu wa Tatu yanatumika kama vipanya vya maabara kujaribia vyakula vinavyotengenezwa kupitia mabadiliko ya msimbojeni; jambo ambalo linaongeza mzigo wa msaada wa kigeni wa chakula. Mbinu hizi ni za kibepari zinazonuia kuendelea kukadamiza mataifa yanayoendelea Kenya ikiwamo.

Katika shairi 'Jikanye' (uk.68) la K.W. Wamitila, mtunzi anaangazia suala la ubepari. Katika ubeti wa kwanza anasema:

*Juta*
*Lia na wana wako waliotwaliwa na mwinyi*
*Lilia na wale wenghine waliofia vitani*
*Angua kilio kwa wengine waliofanywa mashine*
*Sikitikia na hao waliodhalilishwa jana*
*Omboleza na wengine walioteswa na nduguyo*

Ubeti huu unasawiri hali ya kutumikishwa kwa lengo la kujifaidi. Kwa mujibu wa Kamusi Teule ya Kiswahili (2019) Mwinyi ni mwenye navyo. Hivyo, ubeti huu unasawiri namna wenye navyo au matajiri wanavyotumikisha wasionavyo au wasio na uwezo kwa lengo la kujinufaisha wao tu. Katika mshororo wa nne anasema, "Angua kilio kwa wengine waliofanywa mashine." Kauli hii inamaanisha kuwa walilazimika kufanya kazi kupita uwezo wa binadamu. Huu ni mfumo wa kibepari unaoendeleza ukadamizaji na unyama dhidi ya binadamu mwingine. Ndiposa katika mshororo wa mwisho mtunzi anasema, "Omboleza na wengine walioteswa na nduguyo" kumaanisha kuwa mfumo huu haukuendelezwa na wakoloni tu bali hata Wakenya wenyewe wanauendeleza dhidi ya Wakenya wenzao baada ya uhuru.

## 2.5 Kiishilio

Sura hii ilibainisha kuwa baadhi ya mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* yalichochewa na miktadha ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Ilibainika kuwa katika vipindi vya uchaguzi na siasa, wanasiasa hutumia mbinu za udanganyifu na unafiki katika kuendeleza kampeni zao. Wanasiasa hao wanapopata uongozi, huwasaliti wananchi kwa kuungana kuwanyanyasa. Imebainika pia ukoloni mamboleo ni suala ambalo lingali linaathiri

mataifa yanayoendelea kama vile Kenya. Aidha, ukoloni mamboleo hauendelezwi na maiataifa yaliyoendelea tu bali hata viongozi wa Kiafrika waliochukua nyadhifa baada ya ukoloni. Utafiti pia ulibainisha kwamba baadhi ya watunzi kama vile Abdilatiff Abdalla na Alamini Mazrui walitunga mashairi yao wakiwa gerezani hasa baada ya kupinga serikali.

Sura hii pia ilibainisha kuwa kuna matabaka mawili ambayo ni tabaka na matajiri na tabaka la maskini. Tabaka la matajiri linaishi katika maisha ya kuridhika na kustarehe. Kwa upande mwingine, maskini wamekumbwa na matatizo chungu nzima. Ilibainika kuwa ndoa za mapema zinaathiri mtoto wa kike kwa kuwa anaonekana kama chombo cha kuleta mali kupitia mahari. Aidha, wanaoendeleza ndoa hizi wanaelewa fika kuwa ni kinyume na sheria. Dawa za kulevya pia zinawaathiri wananchi hasa watoto wa shule ambao wanaishia kuwa wahalifu. Ilibainika pia licha ya Rais Jomo Kenyatta kuahidi kupiga vita maradhi, maradhi mbalimbali yangali yanawasumbua wanchi. Ubaguzi pia ni suala jingine ambalo lilibainika katika sura hii. Aina mbalimbali za ubaguzi kama vile, ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa kimamlaka na ubaguzi wa kiuchumi zilishughulikiwa.

Sura hii pia ilishughulikia miktadha ya kiuchumi. Ilibainika kuwa hata baada ya kupata uhuru, umaskini ungali unawatatiza wananchi nchini Kenya. Maskini wanakumbwa na matatizo mengi kama vile njaa, magonjwa, ukosefu wa pesa za matumizi ya kimsingi na uonevu. Ilibainika pia kuwa ubepari a dhuluma za kibepari zinaendelezwa katika mataifa yanayoendelea Kenya ikiwamo.

Sura inayofuata ilishughulikia harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Mbinu mbalimbali za kuendeleza harakati za kuibadilisha jamii zilibainishwa kikamilifu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA KUJENGA JAMII YENYE MABADILIKO KATIKA DIWANI YA KARNE MPYA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii iliangazia mbinu za kujenga jamii yenye mabadiliko katika *Diwani ya Karne Mpya*. Mbinu hizi ndizo zinazosawiri harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Kwa mujibu wa Uhistoria Mpya, fasihi huwa haitokani na ombwe tupu. Hii ni kwa sababu, mtunzi huathiriwa na mazingira yake. Sura hii iliongozwa na mhimili wa nadharia ya Uhistoria Mpya kuwa, kusudi la mwandishi wa fasihi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria ya kazi inayohakikiwa pamoja na jamii husika. Mhimili huu ulisaidia katika kubainisha harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko pamoja na mbinu zilizotumika kuendeleza harakati hizo.

## 3.1 Kuhimiza Kumbukumbu za Historia

Katika Shairi “Kumekucha” (uk.24) la Abdlatif Abdalla, mtunzi anahimiza wananchi kutosahau walikotoka. Kwamba wakumbuke waliojitolea kumwaga damu yao ili kupata ukombozi wa uongozi. Mtunzi anawakumbusha kuwa walikabiliwa na hali ngumu katika shughuli ya ukombozi. Kwa hivyo, wasilale wakapotelewa na fahamu. Katika mishororo hii teule mtunzi anasema:

*Kungakucha! Daima tuwe kuwaza, tutokako kukumbuka ni muhimu*
*Kungakucha! Tukumbuke walonwesheza, mti wa ukombozi kwa zao damu*
*Kungakucha! Tusianze kubwagaza, ilotukabili ni kazi ngumu*
*Kungakucha! Tusirudi kujilaza, tukalala na kupotewa fahamu*
*Kungakucha! Lisije kutupumbaza, juwa likatuwiya mbuwaji sumu*

Katika mishororo hii, mtunzi anahimiza na kusisitiza kumbukumbu za historia miongoni mwa wananchi. Historia hii ni kuhusu changamoto walizozipitia ili kujikomboa kutokana na utawala wa kidhalimu. Katika mshororo wa pili anasema, "Tukumbuke walonwesheza, mti wa ukombozi kwa zao damu." Hapa, mtunzi anawahamasisha wanajamii kukumbuka dhiki ambazo wapigania uhuru walipitia. Mojawawapo ya dhiki hizo ni kupoteza maisha. Katika mshororo wa tatu anasema, "ilotukabili ni kazi ngumu," kuwasisitizia wananchi kuwa shughuli ya ukombozi haikuwa lele mama. Katika mshororo wa tano anasema, "Lisije kutupumbaza, juwa likatuwia mbuwaji sumu. "Hapa mtunzi anawazindua wananchi dhidi ya kupumbazwa na hali mpya ya baada ya ukombozi. Aidha, anawatahadharisha kuwa kusahau na kupumbazwa na hali mpya kunaweza kukawaletea hasara.

Katika ubeti wa mwisho, mshororo wa mwisho wa shairi hili, mtunzi anasema, "Tujihadhari na giza, kwani laweza rudi kutuhujumu." Hapa mtunzi anatahadharisha wanajamii kuhusu utawala wa hapo awali. Ametumia neno, "giza" kumaanisha utawala wa kidhalimu. Kwa kuhimiza kumbukumbu za historia, mtunzi ananuia kujenga jamii tofauti na ile ya awali. Jamii bora isiyo na dhuluma za kiutawala zilizoshuhudiwa katika utawala uliotangulia. Aidha, jamii isiyo na vifo kutokana na vita.

Katika shairi ‘Amani’ (uk.118) la Kineene Mutiso, mtunzi anachochea hamu ya kumbukumbu za harakati za kupigania uhuru. Katika ubeti wa kwanza anasema:

*Uhuru pia amani*
*Usifikiri ni zawadi*
*Ambayo imepeanwa*
*Pasipo mikwaruzano*

Katika ubeti huu, mtunzi anawahamasisha wanajamii kutopuuza harakati za kupigania uhuru. Anawakumbusha kuwa harakati za kupigania uhuru zilikuwa ngumu. Kwa mfano, anasema kuwa hazikutolewa kama zawadi. Aidha, anasisitiza kwamba kulikuwa na mapambano makali. Kwa hivyo, mtunzi anahimiza kumbukumbu za historia ya mapambano ya uhuru.

### 3.2 Kuhimiza Umakinifu wa Wananchi

Katika shairi “Msitu ni ule ule” (uk.29) la Omar Babu, mtunzi anahimiza umakinifu wa wananchi hasa wakati wa kampeni za uchaguzi wa viongozi wa nchi. Anawazindua kuhusu namna viongozi hujipendekeza kwa wananchi. Wakishapigiwa kura, viongozi hao huendeleza uongozi ule ule uliokuwa unaendelezwa na viongozi wa awali. Ndiposa anakariri maneno kuwa “fisi ni wale wale” kumaanisha kuwa tabia za viongozi ni zinafanana. Akishadidia hili, Ajulu (1998) anasema kuwa kutokana na matendo yao ya kisiasa kwa miaka saba ambayo imepita, ni dhahiri kuwa viongozi wa upinzani hawana tofauti kubwa na wale wa KANU ambacho hakika ndicho shina ambalo vyama vyote vimeibuka. Katika ubeti wa nne, mtunzi anasema:

*Sikuye wapapurane, maguvu waamilile*
*Muda wasisemezane, ja mahasimu wa kale*
*Wakae wasikizane, warejee pale pale*
*Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale*

Katika mshororo wa kwanza mtunzi anasema, "Sikuye wapapurane, maguvu waamilile". Kumaanisha kuwa viongozi hutumia propaganda za kuleta chuki miongoni mwao na hata wananchi. Katika mshororo wa tatu anasema, "wakae wasikizane, warejee pale pale" kumanisha kuwa viongozi hutumia hila za kilaghai na unafiki kuwapumbaza wananchi. Katika ubeti wa tano mtunzi anasema:

*Uwadhani watengane, wadumu hivyo milele*
*Ghafula waungane, ubaki kuliya ole!*
*Maadui wapatane, watakapokaa wale,*
*Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!*

Katika ubeti huu, mtunzi anaonyesha kuwa baaada ya viongozi kuwalevya wananchi na itikadi potovu, wao huungana na kuwadhulumu wananchi. Hatima yake ni majuto kwa wananchi. Ni dhahiri kuwa mtunzi anawatahadharisha wananchi dhidi ya siasa mbaya za viongozi. Aidha, anawahimiza kuwa makini ili wasinaswe katika mtego wa viongozi laghai wenye hila mbovu. Kwa hivyo, wawe macho!

Katika shairi 'Ndoto Mbaya' (uk.101) la Hezron Mogambi, mtunzi anawahimiza wananchi wachague viongozi wazuri. Aidha, anawaonyesha namna ambavyo kutomakinika kunawapelekea kuchagua viongozi dhalimu. Analiganisha viongozi hao na jinamizi.Mtunzi anasema:

*Ndoto mbaya ya jinamizi*
*Wanaowala watu wengi wakicheka*
*Wanaokula wakilalama njaa*
*Wanawameza wakiwa hai wazimawazima!*

Katika mshororo wa pili mtunzi anasema, "wanaowala watu wengi wakicheka." Hapa mtunzi anonyesha hulka za viongozi. Kwamba ni wadhalimu, katili na wenye dhihaka. Aidha mshororo wa tatu unaeleza hila wanazotumia viongozi ili kuwakandamiza wananchi. Mtunzi anasema, "Wanaokula wakilalama njaa" kumaanisha kuwa, viongozi wanajaribu kuonyesha wananchi kuwa nao wanakumbwa na matatizo kama yao.Kwa hivyo, wote ni sawa. Jambo ambalo mwananchi hajui kuwa ni udanganyifu. Katika ubeti wa pili, mtunzi anasema:

*Juzi niliota ndoto mbaya pia*
*Ndoto yenye mazingaombwe*
*Wanaowala wakiwacheka na kuwapigia makofi*
*Makofi ya kusifu wale wanaowatafuna*

Katika ubeti huu, mtunzi anatumia neno 'mazigaombwe' kumaanisha mambo ya ajabu yanayotendwa na viongozi. Katika mshororo wa tatu anasema, "Wanaowala wakiwacheka na kuwapigia makofi" kumaanihsha kumaansha kuwa wananchi wamepumbazwa kiasi hawafahamu kuwa wanadhulumiwa. Katika mshororo wa nne anasema, "Makofi ya kusifu wale wanaowatafuna." Hiki ni kinaya wananchi kusifu vingozi ambao wanawadhulumu na kuwakandamiza. Katika mshororo wa mwisho mtunzi anasema, "Kusifu kwa uchungu wa kutojua kufahamu".

Kwa ujumla katika beti hizi, mtunzi anahimiza umakinifu wa wananchi kuweza kutambua unafiki wa viongozi. Anafanya hivi kwa kushutumu hali yao wa kutomakinika. Pia anawazindua dhidi ya hila zao potovu, pamoja na kuwaonyesha madhara ya kutokuwa

makini. Akishadidia hili, Njenga (2021) ansema kuwa kubadilisha viongozi pekee hakitoshi. Kwa hivyo, ni muhumu ni muhumimu kuwa na mabadiliko ya kisingi miongoni mwa wanajamii ili kukabiliana na tatizo la uongozi. Wanajamii hawafai kujitolea kuchagua viongozi tu bali wajitolee kumakinikia hulka za viongozi wanaowachagua.

### 3.3 Kuhimiza Umoja, Ushirikiano, Bidii na Uzalendo

Katika shairi "Tujenge nti wanati "(uk.30) la Muchui Bin Chui, mtunzi anahamasisha wanajamii kuhusu umoja, ushirikiano, bidii na uzalendo. Aidha, anasisitiza wajibu wa wananchi katika ujenzi wa nchi. Katika kibwagizo, anawasisitizia kuwa ajengaye nchi ni mwananchi na mwananchi yuyo huyo ndiye avunjaye nchi. Aidha, mtunzi anadhamiria kuwajuza wananchi kuhusu haki zao. Kwa mfano, anawahimiza kuwa wana haki ya kutoa wazo thabiti katika harakati za ujenzi wa nchi. Katika kuhimiza uzalendo, mtunzi anasema kuwa apendaye nchi yake ni yule ambaye hukataa kuisaliti nchi yake. Pia mtunzi anawahimiza wananchi kuweka kando tofauti za vyama na badala yake wawe na umoja na bidii katika ujenzi wa nchi. Aidha, anawatahadharisha wananchi dhidi ya kuchagua viongozi ambao nia yao ni kwenda bungeni kuiba. Katika ubeti wa pili, anasema:

*Kila raia wa nti, anayo haki ya nti*
*Kutoa wazo thabiti, kushiriki harakati*
*Ili msingi wa nti, upate kujithibiti*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

Katika mshororo wa pili anasema, "Kutoa wazo thabiti, kushiriki harakati." Kauli hii inasisitiza ushirikianao pamoja na wajibu wa wananchi katika ujenzi wa nchi. Katika ubeti wa tatu, mtunzi anasema:

*Mzalendo madhubuti, ni yule mpenda nti*
*Akakataa unyeti, serikali kusaliti*
*Asikubali katiti, kutoa siri za nti*

Katika ubeti huu, mtunzi anahimiza uzalendo miongoni mwa wananchi. Katika mshororo wa tatu anasema, "Asikubali katiti, kutoa siri za nti." Sifa mojawapo ya uzalendo ni kutosaliti nchi na wananchi wenzake. Kwa hivyo, mwananchi hafai kamwe kutoa siri zozote za nchi yake. Katika ubeti wa tatu mtunzi anahimiza wananchi kuwa na bidii katika ujenzi wa nchi. Anasema:

*Haya shime wananti, tujumuike umati*
*Tusirefuseh uteti, viama kuweka kati*
*Msingi wetu ni hati, tufanye kazi kwa dhati*

Katika mshororo wa tatu anasema, "Msingi wetu ni hati, tufanye kazi kwa dhati." Hivyo, mtunzi anahimiza bidii katika utenda kazi kwa lengo la ujenzi wa nchi. Aidha, mtunzi anahimiza wananchi kuweka kando tofauti zao; hasa za vyama ili waweze kujenga nchi. Katika ubeti wa nne, mtunzi anasema:

*Tusikubali wateti, ambao nia ni viti*
*Bungeni kwenda manoti, nakunyakua ploti*
*Na huku nyuma mauti, kutukamua matiti*

Katika ubeti huu, mtunzi anawatahadharisha wananchi dhidi ya kuchagua viongozi wabinafsi, wezi, katili na wanyonyaji. Katika shairi "Sisi Ikiwa si Mimi" (Uk 32) la Omar Babu, mtunzi anahimiza umoja na ushirikiano katika kutenda mambo. Anasema kuwa akiwa peke yake hana usemi. Pia anasema kuwa hasikiki kwa kuwa hana ujasiri wa kusema lolote hadharani. Aidha, anasisitiza kuwa ikiwa wataungana na kuwa kundi moja, lengo lao litatimia.

Katika ubeti wa kwanza, mtunzi anawahimiza wenzake wajiunge naye kwa peke yake hana uwezo. Anasema:

*Mimi peke yangu ndimi, niso ma change ugani*
*Sina uwezo sisemi, ningamba afwate nani?*
*Nikiuzwa siungami, kanama sina sinani*
*Sisi ikiwa si mimi, tuna satuwa kutenda!*

Katika ubeti huu, mtunzi anaonyesha udhaifu wake kuwa peke yake hana uwezo na hivyo kuwahimiza wenzake kujiunga naye hili wapate uwezo wa kutenda. Katika ubeti wa tatu anasema:

*Kauli haisimami, niitoapo kinywani,*
*Elewa ukiwa nami, naye angiye kundini*
*Mbiji yetu haizami, itaoleya majini*
*Sisi ikiwa si mimi, tuna satuwa kutenda*

Ubeti huu unasisitiza suala la umoja na ushirikiano. Kuwa wote wakiwa kundini basi mbiji yao haitazama. Kwa maana kuwa shughuli yao haitakwama.

Mbinu hizi za ujenzi wa jamii, zinapiga mwangwi katika Filosofia ya Harambee iliyohimizwa na Rais mwanzilishi wa Taifa la Kenya, Hayati Jomo Kenyatta pamoja na ya Nyayo iliyohimizwa na Rais wa pili wa Taifa la Kenya, Hayati Daniel Arap Moi. Kulingana na Shirika la Kenya Literature Bureau (2019), sifa kuu za Filosofia ya Nyayo zilikuwa ni: umoja, hiari ya mtu kufanya kazi kwa dhati, uamuzi, ushirikiano na kusudi la jambo. Haya yanajitokeza katika beti ambazo zimejadiliwa hapo juu. Kapiyo na wenzake (2011) wanasema kuwa Filosofia ya Nyayo ilihimiza Wakenya kushikilia ukweli katika shughuli zao, kuonyesha imani zao katika matendo, pamoja na kupinga vigezo vyote ambavyo huibua ufisadi na maovu mengine ya kijamii. Sifa hizi za Filosofia

ya Nyayo, zinabainika katika beti za shairi, “Tujenge nti wanati”. Ni shairi ambalo, wito wake mkuu ni kuonyesha kwamba, jukumu la kujenga nchi ni la wananchi.

**3.4 Kuhimiza Ushirikiano Katika Kupiga Vita Matumizi ya Mihadarati**

Katika shairi “Mihadarati shuleni” (Uk.39) la Douglas Mutua, mtunzi anahamasisha washikadau kama vile serikali na wanajamii kuchukua hatua dhidi ya mihadarati shuleni. Mihadarati kama ambavyo ameeleza mtunzi, imeleta madhara kadhaa kama vile michafuko, uvamizi na ni chanzo cha uhayawani na kwamba wanaolewa wanaishia kuwa majuha. Harakati ya kuibadili jamii inaibuka mtunzi anaposema:

*Changamoto natupia, serikali kilingeni,*
*Ni mrefu wa sheria, mkono wake nadhani*
*Azimio zingatia, kusukumiza mbaroni*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

Mtunzi anahimiza serikali kuwatia mbaroni walanguzi wa mihadarati shuleni. Katika mshororo wa pili, mtunzi anasema, “Ni mrefu wa sheria, mkono wake nadhani,” kumaanisha kuwa, serikali ina uwezo wa kupiga kupiga vita matumizi ya mihadarati. Kwa hivyo,ni wajibu wa serikali kuchukua hatua. Aidha, mtunzi anawahimiza wanajamii kujukumika na kupiga vita dawa za kulevya kwa sababu wanaozitumia wako mijini na hata viijijini. Katika ubeti wa mwisho anasema:

*Jamii ina jukumu, mijini na vijijini*
*Wahasiriwa wa humu, dawa hizi tupingeni*
*Serikali haimudu, pasi kondo faraghani*

Katika ubeti huu, mtunzi anasisitiza wajibu wa wanajamii katika vita dhidi ya mihadarati. Aidha, anaishutumu serikali kwa ufisadi. Katika mshororo wa tatu anasema, “Serikali haimudu, pasi kondo faraghani.” Ni kinaya kuwa kuwa serikali inayostahili kumaliza

mihadarati shuleni, ni fisadi. Kwa hivyo, mtunzi anawahimiza washikadau wote kujukumika katika kumaliza mihadarati. Aidha, anawazindua kuhusu na madhara yake.

### 3.5 Kuonya Viongozi Dhidi ya Dharau

Katika shairi "Muwerevu hajinyoi" (Uk.47) la Abdilatif Abdalla, mtunzi anawaonya viongozi ambao wanajiona wenye nguvu kwa kuwa wameleweshwa na utajiri na mamalaka na hivyo kuwadharau maskini. Anawaeleza kwamba kuwa na mali kusiwadanganye kwa sababu huenda siku ikafika wakajipata taabani na hapo wakahitaji msaada. Katika ubeti wa pili anasema:

*Tangu ukite kwa kitu,'megeuka mpumbavu*
*Kattu kuthamini mtu, ambaye kwamba mtovu*
*Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu?*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

Katika mshororo wa kwanza, mtunzi anasema, "tangu ukite kwa kitu." Mtunzi ametumia neno 'kitu' kwa maana ya mamlaka. Katika ubeti huu, mtunzi anawakejeli viongozi ambao baada ya kupata mamlaka, wamekuwa wenye mapuuza, dharau na wasiotaka kuambiwa ukweli. Aidha, anawasuta kwa kujiona kuwa hawahitaji kukosolewa. Katika ubeti wa nne, anasema:

*Kupata kusikughuri, ukidhani muwerevu*
*Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu*
*Iko siku itajiri, ukjikute mwenye wavu*

Katika ubeti huu, mtunzi anatahadharisha kuwa kiburi ni cha muda mchache. Pia anawakumbusha kuwa ipo siku watahitaji msaada. Kwa jinsi hii, anawazindua viongozi kujua ukweli.

Katika shairi ‘Kwenda mbio sio kupata’ (uk.58) la Omar Babu, mtunzi anawatahadharisha matajiri kuwa kupata huwa majaliwa; kuna wakati tajiri huwa maskini. Kwa kufanya hivi, mtunzi analenga kukumbusha walionavyo kufahamu kuwa hawana tofauti na wasionavyo. Katika kibwagizo, mtunzi anakariri, “kwenda mbio si kupata, riziki ni majaliwa.” Kwa kusema hili, mtunzi analenga kuhimiza walionavyo kuheshimu wasionavyo kwa sababu huenda nao wakajipata hawana. Pia anawashauri kuhusu ulazima wa mabadiliko maishani.

Katika shairi, “ Mtu na utu” (uk. 45) la Muchui Bin Chui, mtunzi anawakejeli viongozi na matajiri wenye tabia ya kuwadharau wengine. Anasema:

*Ninaposema kiutu, si kwenda kimatumatu*
*Wenye fahari na vitu, kuona watu si watu*
*Mali na mtu si kitu, upungukiwapo utu*

Katika mshororo wa pili, ametumina maneno ‘fahari’ na ‘vitu’ kumaanisha wenye vyeo na mali. Anawahimiza kuwa na utu japo wana mali. Hii ni kwa sababu, utu una dhamani kubwa kuliko utajiri na vyeo.

### 3.6 Kuhimiza Uvaaji wa Mavazi ya Heshima

Katika shairi “Mavazi” (Uk.52) la Douglas Mutua, mtunzi anawashauri kina mama kuvaa mavazi ya heshima. Anaendelea kusema kuwa mavazi wavaayo kina mama yanachochea maovu kama vile ubakaji. Aidha, mtunzi anawashauri kubadili na kuanza kuvaa mavazi yenye heshima. Anawaonya kuwa wasipobadili, utamaduni wa bara la Afrika utapotea.

Katika beti mbili za mwisho mtunzi anasema:

*Vingine zitatuhama, tamaduni*
*Bara letu litazama, utumwani*
*Wapi tutaposimama, duniani?*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Ni mama mwenye hekima, na razini*
*Mvaa mavazi mema, hadharani*

Katika ubeti wa kwanza, mtunzi anaonyesha athari za kutodumisha tamaduni. Kwamba bara la Afrika litaingia utumwani pamoja na kujitwika aibu. Anasisitiza kuwa, ili kuheshimiwa ni sharti kina mama wavae mavazi yenye heshima. Kwa jumla, shairi hili linatoa wito wa kudumisha utamaduni wa bara la Afrika. Hasa zinazodumisha heshima kama vile mavazi ya Kiafrika. Msichana anachukuliwa kukosa adabu kwa wakubwa wake ama jamii kwa jumla kwa kuvaa vazi fupi na hata nguo inayombana sana (Ndung'u (2024). Kwa hivyo, mavazi ni suala linalothaminiwa katika jamii za Afrika kwa kuwa ni sehemu ya utamduni.

### 3.7 Kuhimiza Maskini Kutia Bidii

Katika shairi, 'Kwenda mbio sio kufika', (uk.58) la Omar Babu, mtunzi anamtia maskini moyo kuwa iwapo ataweka jitihada si huenda akfanikiwa. Katika beti za kwanza mbili mtunzi anasema:

*Haliwi lisilokuwa, lililo lako huchata*
*Mambo yamekadiriwa, ya ukwasi na ukata*
*Mja kujitititimuwa, si ajabu akadata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki ni majaaliwa*

*Mafungu yamegawiwa, gaolo halitopita*
*Mara mtu hwangukiwa, jaza kitita katika*
*Mwengine hupungukiwa, tajiri awe mkata*

Mtunzi anaonyesha kuwa mpaji riziki ni Mungu. Kwa hivyo, anawazindua maskini kuhusu wajibu wao wa kutia bidii. Pia anawakumbusha matajiri kuwa hali hubadilika na tajiri akawa maskini. Katika ubeti wa pili mshororo wa tatu anasema, "Mwenginewe hupungukiwa, tajiri awe mkata," kumaanisha kuwa hali hubadilka. Kando na kuhimiza bidii, mtunzi anashutumu kulaza damu na kuendeleza umaskini.

### 3.8 Kuwasuta Mabepari

Katika shairi 'Kila mpenda haramu' (uk.62) la Muchai Bin Chui, mtunzi anawasuta na kuwakemea wapendao kula haramu kwa kutumia mbinu za hila kujinufaisha wenyewe. Njia hizi huwa ni za kuwadhalilisha na kuwadhulumu wale ambao huwa ni wenye uwezo mdogo. Tazama beti hizi teule:

*Heri utwae rukwama, utambe hadi Watamu*
*Yakunyauke matama, kwa kuiiga baragumu,*
*Kuliko uwe kadama, wadhalili binadamu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

*Namba nanyi mlo wima, mliopewa jukumu*
*Mlioajiri umma, kupenda kutudhulumu*
*Kuna siku ya kiyama, ameipanga Rahimu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

Katika shairi hili, mtunzi anawakumbusha wanaodhulumu wengine hasa viongozi kuwa siku ya kiama itakapofika, nakama itawasibu. Ametumia neno 'nakama' kumaanisha

adhabu kubwa itakayowakumba viongozi dhalimu. Kwa hili, anawazindua na kuwahimiza warekebishe dhidi ya vitendo vyao vya udhalimu na ubepari. Aidha, anawatahadharisha kuhusu adhabu ambayo hukumba watendao maovu.

**3.9 Kukashifu Ndoa za Mapema**

Katika shairi 'Siolewi' (uk.78) la Douglas Mutua, mtunzi anapinga dhana kuwa kuelimisha mvulana ni bora kuliko msichana. Anakashifu mzazi anayetaka kuachisha msichana masomo ili amuoze mapema. Mtunzi anasema:

*Naihitaji elimu, japo mie msichana*
*Elimu nguzo muhimu, na yenye kubwa dhamana*

*Kwani kosa gani humu, kuzaliwa msichana?*
*Ninasoma siolewi!*

*Dhana kwamba mvulana, akisoma afadhali*
*Mashiko kamwe haina, ni bure ukatili*

*Mahari hayatokimu, elimu ghala la nyaka,*
*Ninasoma siolewi!*

Katika beti hizi, mtunzi anahimiza elimu kwa watoto wa jinsia ya kike kama ilivyo kwa jinsia ya kiume. Zaidi, anawashutumu wanaaondeleza ndoa za mapema kwa watoto wa jinsia ya kike. Anawakumbusha kuwa, katika ulimwengu wa sasa watoto wote wanafaa kuelimishwa. Pia wote wana haki sawa. Katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza anasema, "Mahari hayatokimu, elimu ghala la nyaka," kwa maana kuwa elimu ina faida kubwa kuliko mahari. Aidha, faida ya kuelimisha msichana ni kubwa na hushuhudiwa kwa miaka mingi.

### 3.10 Kukashifu Ukoloni Mamboleo na Ubaguzi wa Kimataifa

Katika shairi 'Kijiji cha mauji' (uk.121) la K. W Wamitila, mtunzi anapinga kauli kuwa mataifa yote ni kijiji kimoja. Aidha, anakerwa na namna ambavyo mataifa yanaoendelea yanadhalilishwa na yaliyoendelea ili kupata misaada. Mataifa yaliyoendelea yanatupia yanayoendelea bidhaa duni pamoja na kuwaibia mazao yao ya mashambani. Mtunzi pia anasawiri namna mataifa yaliyoendelea yanavyolazimisha yanayoendelea kuyasifu na kukubali kuwa wao ni maskini ili wapate msaada. Kwa mfano, anasema:

*Tukigeuzwa kasuku, kusifu kila uthori*
*Ndipo tupewe mwiku, kwa kuwa tu mafakiri*
*"Wengine wametupiku, hili lazima tukiri!"*

Ni kutokana na masuala kama haya ya ukoloni mamboleo ambayo yanamfanya mtunzi kubaini kuwa ni unafiki mataifa hayo kudai kuwa sote twaishi kijiji kimoja.

### 3.11 Kuhimiza Tahadhari Dhidi ya Ukimwi

Katika shairi "Kuteleza siku hizi' (uk.56) la Dougla Mutua, mtunzi ametumia jazanda katika shairi hili kuhimiza umma kujitahadharisha na ugonjwa wa ukimwi ambao anaufananisha na wingu jeusi. Katika ubeti wa kwanza anasema:

*Wingu jeusi latoka, kusi hadi kaskazi*
*Mashariki ladondoka, magharibi si ajizi*
*Mno tuna shaka shaka, twatapa ja sisimizi*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.*

Katika ubeti huu, mtunzi anatoa taswira ya namna ugonjwa wa Ukimwi unavyotamba kwa kasi pade zote za dunia. Aidha, anaonyesha namna ugonjwa wa Ukimwi unavyowatia watu wasiwasi. Anafananisha ugonjwa huu na 'wingu jeusi' kumaanisha maafa yanayosabishwa na ugonjwa huu. Hali hii inashadidiwa na ripoti ya UNAIDS

(2006). Kwa mujibu wa ripoti hii, ugonjwa wa Ukimwi umeenea kutoka maeneo machache yaliyokuwa yameathiriwa mpaka takribani kila nchi ulimwenguni. Kwa miaka ishirini na mitano tu tangu kuzuka kwa ugonjwa huu, watu milioni 65 wameambukizwa huku milioni 25 wakiaga. Hii ni idadi ya kutisha! Kwa hivyo, mtunzi anazindua wanajamii kuhusu hatari za ugonjwa wa Ukimwi. Pia anawatahadharisha dhidi ya kujiingiza katika anasa ambazo huenda zikapelekea maangamizi yao. Ndiposa katika mshororo wa mwisho anasema kuwa, "Siku hizi kuteleza, hakikia ni kuanguka." Kwa maana kuwa kutotahadhari dhidi ya Ukimwi kunasababisha maafa.

Katika ubeti wa pili, mtunzi anatoa taswira ya namna ugonjwa huu unavyoangamiza hata wajionao wajuzi. Anasema:

*Roho zinatifilika, kuwahiliki mahiri*
*Wanaochovya gharika, starehe ya Dhahiri*

Ni dhahiri kuwa mtunzi anawashutumu wanaojiingiza katika anasa na hatimaye kujisababishia maangamizi. Katika ubeti wa tano, mtunzi anaonya kuwa ugonjwa wa Ukimwi haubagui. Anasema:

*Nafaka ashashumbisha, dungudungu simuoni*
*Majibwa anagurisha, hawanusuriki nyani*
*Ya mbwa chunga maisha, nyani kaidi ta'bani*

Katika ubeti huu, mtunzi anawahimiza wanajamii kutahadhari kwa kuwa Ukimwi haubagui. Anatumia jazanda kama vile nafaka, dungudungu, majibwa na nyani. Kumaanisha kuwa ugonjwa wa Ukimwi haubagui yeyote. Katika ubeti wa tano, mtunzi anwazindua wanajamii kuhusu kutopumbazwa na uzuri wa wanawake au wanaume. Anawafananisha na maua. Kwa kawaida maua hupendeza. Aidha, anatahadharisha kuwa

mengi ya maua hayo yana sumu. Kwa maana kuwa badhi wa wanawake au wanaume hao wazuri wana Ukimwi. Mtunzi anasema:

*Kokote kuna mauwa, ela mengi yana sumu*
*Yosayosa yanauwa, anayenusa hadumu*
*Bora jangwa kutengewa, kuepuka chungu tamu*

Ni dhahiri kuwa, mtunzi anawahimiza wanajamii kujikinga na Ukimwi. Njia moja ya kujikinga ni kujiepusha na mapenzi ya kiholela ambayo huenda yakaleta hasara.

### 3*.12 Kuhimiza Haki na Usawa wa Kijinsia*

Baadhi ya mashairi katika *Diwani ya Karne* Mpya yanazindua jamii kuhusu kudumisha usawa wa kijinsia. Katika shairi "Siolewi" (uk.78) la Douglas Mutua, mtunzi anahimiza usawa wa kijinsia katika jamii. Katika ubeti wa pili anasema: "Nahitaji elimu, japo mie msichana." Kumaanisha kuwa kama vile mvulana apewavyo elimu, hata naye msichana anahitaji elimu. Katika ubeti wa nne anasema:

*Wapo wake mahashumu, wasomi nana pulika*
*Wahimili kuzikimu, aila zao hakika*

Katika ubeti huu, mtunzi anwajuza wanajamii kuhusu umuhimu wa mtoto wa kike. Aidha, anawazindua kuwa kinyume na mila zielekezavyo, elimu ya mtoto wa kike inamsaidia kuikimu familia yake. Katika ubeti wa sita mshororo wa tatu anasema, "Kuoza mwenye elimu, huwa kuu taaadhima." Kwa hili, mtunzi anawajuza wanajamii kuwa, kuna heshima kubwa kuoza msichana mwenye elimu. Mtunzi pia anashutumu wanaowanyima watoto wa kike elimu bila sababu yoyote ila kwa misingi kuwa elimu ya mtoto wa kiume ndiyo bora.

Katika shairi “Elimu adhimu” (uk.54) la Muchui Bin Chui, mtunzi anazindua kuhusu kutobagua katika kusaka elimu. Katika ubeti wa tano mshororo wa kwanza anasema, “Someni akina mama, kina baba na ghulamu.” Mshororo huu anahimiza wanajmii wote wasome bila ubaguzi wa kijinsia wala kiumri. Hili linasahdidiwa na Katiba ya Kenya (2010) ambayo inahimiza haki ya kila Mkenya. Kifungu cha 43 cha katiba kinaeleza kuhusu haki za kiuchumi na kijamii. mtu ana haki. Haki hzi ni pamoja na haki ya usalama wa kijamii na haki ya kupata elimu ya msingi bila malipo.

Katika ubeti wa sita mshororo wa kwanza mtunzi anasema, “Ndiyo njia ya salama, yafaa kila hirimu”. Kwa hivyo, anawahamasisha wanajamii kuhusu manufaa ya elimu hasa kwa jinsia zote. Hii ni kwamba, elimu ni haki ya msingi kwa kila mtu bila kuzingatia misingi yoyoye.

**3.13 Kiishilio**

Sura hii ilibainisha mbinu za kujenga jamii yenye mabadiliko. Ilibainika kuwa mbinu mbalimbali zilitumika kuendeleza harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Mbinu hizi ni pamoja na kuhimiza, kukejeli, kusuta, kuonya, kukashifu na hata kutahadharisha. Sura inayofuata ilishughulikia umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko.

## SURA YA NNE

## UMUHIMU WA HARAKATI ZA UJENZI WA JAMII YENYE MBADILIKO KATIKA JAMII YA SASA

### 4.0 Utangulizi

Kazi ya yoyote ya fasihi huwa na athari kwa msomaji. Masinde (2003) anasema kuwa fasihi ina uwezo wa kuathiri fikra na hisia za mpokeaji na hakuna mtu anayebakia vile alivyokuwa baada ya kuguswa na kazi nzuri ya sanaa. Aidha, mojawapo ya madhumuni ya fasihi ni kuzindua jamii. Sura hii ilijadili umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko hasa katika jamii ya sasa katika *Diwani ya Karne Mpya*. Sura hii iliongozwa na mihimili miwili ya Uhistoria Mpya kuwa, chimbuko la kazi ya fasihi huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi. Kwa hivyo, sura hii imechunguza umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko kama ulivyohakikiwa na kufasiliwa baada ya uchunguzi wa miktadha na mbinu za kujenga jamii yenye mabadiliko.

Mhimili wa pili ni kuwa, suala la miktadha na utamaduni wa kijamii lazima liangaliwe upya. Mhimili huu ulisaidia kueleza sababu ya kuwa na harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Hakuna kitu, mtu au hali katika maisha ya mwanadamu inayoweza kuepuka mabadiliko (Masinde na Wanyela, 2024). Mabadiliko yaliyoshughulikiwa katika sura hii ni chanya. Kwa hivyo, ndiyo umuhimu wa harakati zililizobainishwa katika sura ya pili. Aidha, umuhimu huo uligawika katika vitengo vitatu ambavyo ni uzindushi, uwajibikaji na usawa.

## 4.1 Uzindushi

Kulingana na Musembi (2008), zinduko ni kufanya mtu awe na habari kuhusu jambo fulani. Kwa hivyo, uzindushi ni hali ya kutoa mtu kutoka hali ya kutojua, kutoelewa au ujinga. Harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko zinaibua umuhimu wa kuwazindua wanajamii kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Kuelewa Unafiki wa Viongozi

Katika shairi "Mti ni Ule Ule" (uk.29) la Omar Babu, ni muhimu kuwa mtunzi anawahimiza na kuwazindua wananchi kujihadhari na hadaa za viongozi. Anaweka wazi njia za kinafiki wazitumiazo viongozi hasa wakati wa kampeni za uchaguzi ili wapate kura. Mtunzi anaweka wazi kuwa viongozi huwa hawana chuki miongoni mwao kama ambavyo hutaka mwananchi aamini. Kwamba, hujifanya wanachukiana ili kuwapumbaza wananchi na baadaye wakishachaguliwa wao huungana kupora na kujitajirisha. Katika ubeti wa mwisho mtunzi anasema:

*Uwadhani watengane, wadumu hivyo milele*
*Ghafula waungamane, ubaki kuliya ole!*
*Maadui wapatane, watakapokaa wale,*
*Kwani mwitu ni ule ule, na fisi ni wale wale.*

Katika mishororo hii, mtunzi angependa wananchi waelewa kwamba hakuna tofauti kati ya viongozi wa hapo awali na wapya. Kwa hivyo, lengo lake kuu ni kuwasaidia kuelewa hadaa za viongozi na waweze kuwachagua viongozi bora.

### 4.1.2 Kujuza Kuhusu Unafiki wa Mataifa Yaliyoendelea

Katika shairi 'Kijiji cha mauji' (uk.121) la Wamitila, mtunzi anakashifu kauli kuwa mataifa yote ni kijiji kimoja. Sababu ya kukashifu kauli hii ni kuwa mataifa yaliyoendelea

yanaendelea kuyaibia, kuyadharau na kuyabagua mataifa yanayoendelea. Katika kila mshororo wa mwisho, mtunzi anatumia swali balagha kusisitiza shaka yake kuhusu kauli ya kwamba mataifa yote ni kijiji kimoja. Anaweka wazi sababu zake kushuku kauli hii. Sababu hizi ni kama vile kudharauliwa na kubaguliwa, kutupiwa bidhaa za jalalani, kugeuzwa kasuku ili tupewe mabaki, kufanywa vifaa vya sayansi, kuibiwa, kukengeushwa akili kwa vitabu vya kijinga na binti zetu kugeuzwa bidhaa za madanguro. Umuhimu wa mawazo haya ya mtunzi, ni kwamba analenga kuweka wazi na kujuza umma kuhusu unafiki wa mataifa yalioyendelea na mbinu wanazotumia kuendeleza ukoloni mamboleo.

## 4.2 Uwajibikaji

Uwajibikaji ni hali ya kutekeleza wajibu au majukumu kulingana na matarajio ya jamii. Harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko zina umuhimi wa kuhimiza uwajibikaji wa wanajamii ili kuwezesha:

### 4.2.1 Kudumisha historia

Mojawapo ya majukumu ya fasihi ni kwamba huhifadhi historia ya jamii. Katika shairi ‘Kumekucha’ (uk.24) la Abdlatif Abdalla, umuhimu wa msingi ni kwamba mtunzi anawahimiza wananchi kutosahau walikotoka. Anafanya hivi kwa kuwachorea taswira ya maisha yalivyokuwa kabla wapate ukombozi. Aidha, anaeleza namna wapigania ukombozi walivyojitoa mhanga muradi wajikomboe. Ukombozi unaorejelewa ni wa kujinasua kwenye udhalimu wa chama tawala cha hapo awali. Anahimiza kumbukumbu hizi ili wananchi wasitamani kuwa katika hali kama hiyo tena na badala yake wajibiidishe

katika kuijenga jamii isiyo na utawala wa kidhalimu kama iliyokuwepo hapo awali. Katika mishororo hii teule, mtunzi anasema:

> *Kungakucha! Daima tuwe kuwaza, tutokako kumbukumbu ni muhimu*
> *Kungakucha! Tukumbuke walonwesheza, mti wa ukombozi kwa zao damu*
> *Kungakucha! Lisije kutupumbaza, juwa likatuwiya mbuwaji sumu*

Katika mishororo hii, anasisitiza umuhimu wa kumbukumbu za kipindi cha upiganiaji ukombozi wa utawala na hivyo kuwaomba wasipumbazwe na ukombozi ambao wameupata. Ni dhahiri kuwa, mtunzi angependa wananchi waelewe malengo ya wapiganiaji uhuru ambao kufikia sasa haujakamilika. Aidha, mtunzi angependa wananchi waenendeleze juhudi za ukombozi zilizoanzishwa na waliowatangulia.

Katika shairi "Tujenge Nti Wananti" (uk.30), mtunzi kupitia kuhimiza umoja na ushirikiano, anapiga mwangwi Filosofia ya Nyayo ambayo pia ilikuwa inapiga mwangwi Filosofia ya Harambee. Filosofia ya Nyayo ilianzishwa na Rais wa pili wa Taifa la Kenya ili kuhimiza Wakenya kuendeleza juhudi za ujenzi wa nchi zilizokuwa zimeanzishwa na Rais Jomo Kenyatta. Rais Jomo Kenyatta alikuwa ameanzisha Filosofia ya Harambee kwa lengo la kujenga nchi na hasa uchumi wa Kenya. Kuunga mkono filosofia ya mtangulizi wake, Rais Moi alitoa wito wa umoja na ushirikiano wa wanajamii kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya Taifa la Kenya. Pia katika shairi" Amani" (u.k, 118) la Kineene Mutiso, mtunzi anatoa wito wa kuhifadhi historia ya harakati za kujikomboa kutokana na utawala dhalimu. Kwa hivyo, watunzi wa mashairi haya wanasisitiza wito wa wanachi kuzindisha mapambano ili kuendeleza juhudi za watangulizi.

### 4.2.2 Kumaliza Mihadarati Shuleni

Ni muhimu kuhimiza washikadau katika sekta mbalimbali kuchukua hatua dhidi ya walanguzi wa mihadarati shuleni. Kulingana na ripoti ya NACADA (2016), kunafaa kuwa na mafundisho kuhusu dawa za kulevya, athari zake na namna ya kuepuka matumizi yake. Mtunzi wa shairi, 'Mihadarati shuleni' (uk. 39) la Douglas Mutua analenga kupiga vita madhara ya matumizi ya mihadarati katika jamii. Katika shairi hili, mtunzi anatoa wito kwa serikali kuwatia mbaroni walanguzi wa mihadarati. Pia anatoa wito kwa wanajamii kuwajibika katika vita dhidi ya mihadarati. Aidha, anawakumbusha wanajamii kutotegemea baadhi ya waliopewa hilo jukumu serikalini kwa kuwa ni wafisadi. Wito mkuu katika shairi hili ni washikadau wote kuwajibika ili kumaliza mihadarati shuleni. Aidha, ikiwa watawajibika, jamii haitashuhudia madhara yanayosababishwa na mihdarati kama vile: Wanafunzi kuwa maluuni, wazazi kupatwa na simanzi, kufanya uvamizi na wanafunzi kuishia kuwa majuha.

### 4.2.3 Kudumisha Utamaduni wa Afrika

Katika shairi 'Mavazi' (uk.52) la Douglas Mutua, ni muhimu kwamba mtunzi anahimiza kina mama kuvaa mavazi yenye heshima. Anasema kuwa mavazi yasiyo heshima yanachochea maovu kama vile ubakaji na hata kuletea bara Afrika aibu. Katika ubeti wa sita mtunzi anasema:

*Vingine zitatuhma, tamaduni,*
*Bara letu litazama, utumwani*
*Wapi tutaposimama, duniani?*
*Magaunu ya heshima, tuvaeni*

Katika ubeti huu, Mtunzi anahofu kuwa uvaaji wa mavazi yasiyo na heshima utapoteza tamaduni za Afrika. Pia kupoteza tamaduni za Afrika ni kukubali utumwa na hivyo kuwa chanzo cha aibu kwa Waafrika.

### 4.2.4 Kumaliza Udhalimu na Ubepari

Katika shairi 'Kila mpenda haramu' (uk.62) la Muchai Bin Chui, mtunzi anasuta na kuonya wapendao haramu. Anawakumbusha kuwa watapatwa na nakama kwa kupenda haramu. Anakumbusha waajiri wapendao kudhulumu umma kuwa mwisho wao u karibu. Katika ubeti wa sita anasema:

*Wakatabu watama, zatosha hizo nudhumu*
*Maadamu unga wima, usipate kwa haramu*
*Duniani tenda wema, atakulipa Karimu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

Huu ndio ubeti wa mwisho wa shairi hili. Umuhimu wake ni kwamba mtunzi anahimiza matendo mema hapa duniani kwa sababu kuna malipo kutoka kwa Mungu. Aidha, katika kibwagizo, anasisitiza kuwa adhabu ya watendao maovu itakuwa kali. Ni dhahiri kuwa, mtunzi analenga kumaliza vitendo vya kidhalimu na kibepari katika jamii.

### 4.2.5 Kupiga Vita Maradhi

Alipoingia uongozini, Rais mwanzilishi wa taifa aliahidi kupiga vita adui watatu nchini Kenya ambao ni maradhi, ujinga na njaa. Kufikia karne ya ishirini na moja, maradhi mbalimbali na hatari yameibuka; mojawapo ikiwa ni Ukimwi. Katika shairi 'Kuteleza siku hizi' (uk.56) la Douglas Mutua, ni muhimu kwamba mtunzi anahimiza umma kujitahadharisha na ugonjwa wa Ukimwi. Anaweka wazi namna ugonjwa huu ulivyo hatari. Katika ubeti wa tano mtunzi anasema:

*Nafaka ashasumbisha, dungudungu simuoni*
*Majibwa anagurisha, hawanusuriki nyani*
*Ya mbwa chunga maisha, nyani kaidi ta'bani*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka*

Katika mshororo huu, mtunzi anaeleza namna ugonjwa wa Ukimwi haubagui na hivyo kuhimiza umma kujihadhari na wasije wakaangamia. Kwa tahadhari hii, mtunzi analenga kupunguza idadi ya vifo pamoja na kutokomeza ugonjwa wa Ukimwi.

### 4.2.6 Kumaliza Uzembe na Utegemezi

Ni muhimu kwamba watunzi mbalimbali wamedhamiria kumaliza utegemezi kupitia harakati kama vile kuhimiza bidii, umoja, ushirikiano na kukashifu ukoloni mamboleo. Mojawapo ya nguzo za Filosofia ya Harambee ilikuwa ni kukemea uzembe. Kulingana na Filosofia hii, uhuru wa mwanadamu ungepatikana tu kwa kufanya kazi kwa lengo la kuwa na taifa imara. Taifa imara kwa maana ya taifa linalojisimamia bila kutegemea mataifa yaliyoendelea au wakoloni walioondoka. Katika shairi 'Kwenda mbio si kupata' (uk, 58) la Omar Babu, mtunzi anagusia suala la kukemea uzembe. Katika ubeti wa nne mshororo wa kwanza, mtunzi anasema, "Uzembe sio muruwa, ni wajibu kutafuta." Kulingana na mtunzi wa shairi hili, japo riziki ni majaaliwa, mtu pia anafaa kuwa na bidii na kuambaa uzembe. Katika shairi 'Utakula nini?' (uk.60) la Douglas Mutua, mtunzi anakemea uzembe. Anashangaa vipi binadamu atatoa wapi cha kula iwapo ataendelea kulaza damu. Katika ubeti wa sita mshororo wa pili anasema, "Kumetupambazukia, tukagure utumwani." Kupitia mshororo huu, mtunzi anaonyesha tayari hawajajitegemea. Katika ubeti wa saba anasema

*Ni heri kuriaria, chungucho kiwa mekoni,*
*Allahu takujalia, uzembe 'sipotamani*
*Neema kuzidishia, ni kazi yake Manani*
*Walaza damu daima, mwisho takula nini?*

Katika ubeti huu, mtunzi anakataza uzembe na kuhimiza binadamu kufanya chochote kile angaa Mungu atamjalia muradi ana bidii. Aidha, mtunzi anabainisha kuwa, hatimaye binadamu ataweza kujitegema kwa kula.

Katika shairi "Mwangu nakuusia" (u.k, 127), mtunzi anaonyesha umuhimu wa kufanya kazi.Katika ubeti wa pili anasema:

*Ewe muogopa kazi, nguo sijifinikile,*
*Fahamia waziwazi, hilo lilitengezwile*
*Guo Silone minyuzi, wenzio walishonele*
*Hatari kujiachile, ela kazi sakanyile*

Mtunzi anabainisha kuwa, vyote vinavyoonekana ni matokeo ya kazi. Hata nguo ambazo mzembe "muogopa kazi" ameiva ni kuwa watu wengine walifanya kazi ndiposa akaipata yeye. Anaendelea kueleza kuwa ni hatari kukaa bila kazi ya kufanya. Ni dhahiri kuwa mtunzi analenga kupiga vita uzembe ili wanajamii waweze kujitegemea pamoja na kukuza uchumi wa nchi

**4.3. Usawa**

Usawa ni hali ya kutokuwa na baguzi kwa misingi yoyote kama vile elimu, jinsia, dini, kabila , tabaka au hadhi. Harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko zina umuhimu wa kukuza usawa ili kufanikisha:

### *4.3.1 Usawa wa Kitabaka*

Katika shairi 'Muwerevu hajinyoi' (uk.47) la Abdilatif Abdalla), ni muhimu kwamba mtunzi anakashifu na kuwaonya matajiri dhidi ya kujigamba na kudharau wasionavyo. Anawakumbusha kuwa huenda siku moja wakajipata kwenye wavu na hivyo kuhitaji msaada wa hao hao wanaowadharau. Lengo lake ni kuwasaidia wajirekebishe. Aidha, mtunzi analenga kuziba mwanya wa utabaka katika jamii na hivyo kuhimiza heshima na usawa kwa wote. Katika ubeti wa tano mtunzi anasema:

Ipo siku itajiri, ujikute mwenye wavu
Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?

Katika mshororo wa kwanza, mtunzi anasema kuwa kuna siku itafika naye tajiri ajipate kwenye tatizo. Kumaanisha kuwa japo yeye ni tajiri bado anaweza kuhitaji msaada. Katika mshororo wa pili, anatumia swali balagha kusisitiza kuwa mwerevu hajinyoi. Kumaanisha kuwa hakuna awezaye kufanya kila kitu bila kuhitaji msaada wa wengine. Kwa hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa binadamu hutegemeana. Pia wote wana hadhi sawa.

Katika shairi 'Kwenda mbio sio kupata' (uk.58) la Omar Babu, ni muhimu kwamba mtunzi anawakumbusha walionavyo kuwa, hawana tofauti na wasionavyo. Hii ni kwa sababu tajiri pia huwa maskini. Katika ubeti wa pili anasema:

*Mara mtu huwangukiwa, jaza kitita kitita*
*Mwengine hupungukiwa, tajiri awe mkata*

Kwa kusema hili, mtunzi anaonyesha kuwa hakuna hali ya kudumu. Kwa hivyo, anawasaidia wanajamii kudumisha heshima na usawa bila kujali hadhi.

Katika shairi, 'Nilipokuwa tajiri' (uk.131) la Paul Nabiswa, mtunzi anachora taswira ya tajiri aliyegeuka maskini. Alipoteza kazi na majina makubwa ya heshima aliyokuwa akiitwa. Katika ubeti wa nane anasema:

*Dunia kumbe duara, mimi sasa maskini*
*Nimesalia fukara, nilipo sina sinani*
*Kope si zangu ni dira, kwa manoti na mapeni*
*Yamenikumba madhara, sijui nifanye nini?*

Katika ubeti huu, ni muhimu kuwa mtunzi anahimiza wenye mali na vyeo kuwaheshimu walio chini yao kwa kuwa vyeo na mali huisha. Mwishowe hukumbwa na majuto. Mtunzi anashadidia hili katika ubeti wa mwisho mshororo wa mwisho anaposema, "Kumbe mpanda ngazi, mwishowe yeye hushuka" kumaanisha kuwa hakuna hali ambayo hudumu.

### 4.3.2 Usawa wa kijinsia

Katika shairi 'siolewi' (uk.78) la Douglas Mutua, umuhimu wake ni kwamba mtunzi anapinga suala la kukatiza masomo ya msichana na kumuoza mapema. Aidha, mtunzi anapinga dhana kuwa elimu ya mvulana ni afadhali. Kwa hili, mtunzi anakuza usawa wa kijinsia hasa katika masomo pamoja na kupinga ndoa za mapema kwa mtoto wa kike. Katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza mtunzi anasema: "Nahitaji elimu, japo mie msichana." Katika mshororo huu mtunzi analenga kuonyesha kuwa mtoto hata awe wa jinsia ya kike, elimu kwake ni muhimu kama ilivyo katika mtoto wa kiume. Katika ubeti wa tatu anasema:

*Dhana kwamba mvulana, akisoma afadhali*
*Mashiko kamwe haina, ni bure ukatatili*

Mishororo hii inasisitiza umuhimu wa kuwapa watoto wote fursa sawa ya elimu. Pia mtunzi anawasaidia wanajamii kuelewa kuwa watoto wote ni sawa. Katika shairi 'Elimu Adhimu' (uk.54) la Muchai bin Chui, ni muhimu kwamba mtunzi anahimiza watu wote kupata elimu bila kuegemea jinsia. Katika ubeti wa tano mshororo wa kwanza anasema, "Someni akina mama, kina baba na gulamu." Mshororo huu unabainisha wazi kuwa anataka wanajamii wote kupata elimu bila kubagua jinsia yoyote. Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010), kila mtu ana haki ya kupata elimu. Usawa wa kijinsia hasa katika elimu ni suala muhimu katika jamii hasa katika maendeleo na ukuaji wa jamii.

**4.4 Kiishilio**

Sura hii ilibainisha umuhimu wa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko na kubainisha kuwa harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko zina umuhimu mkubwa hasa katika jamii ya sasa. Umuhimu huo uligawika katika vitengo vitatu ambavyo ni uzindushi, uwajibikazi na usawa. Katika vitengo hivi, umuhimu ufuatao ulibainika: kukuza usawa ili kuziba mwanya wa utabaka na wa kijinsia, kudumisha historia na kumbukumbu, kuzindua kuhusu unafiki wa mataifa yaliyoendelea pamoja na unafiki wa viongozi.

Aidha, harakati hizi pia zina umuhimu wa kumaliza maradhi, kumaliza uzembe miongoni mwa wanajamii, kumaliza udhalimu na ubepari pamoja na kuonyesha nafasi ya washikadau mbalimbali katika vita dhidi ya matumzi ya mihadarati hasa miongoni mwa vijana.

Umuhimu ulioibuliwa na harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko ni idhibati kuwa, kuna masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanahitaji kurekebishwa na kubadilishwa ili binadamu aweze kufurahia haki zake za kibinadamu. Sura inayofuata ilishughulikia hitimisho na matokeo ya utafiti.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MATOKEO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii ilishugulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi unaohusiana na mada ya utafiti huu.

### 5.1 Muhtasari

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Aidha, utafiti huu ulilenga kuchunguza miktadha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa iliyochangia harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Hatimaye, utafiti huu ulilenga kuonyesha umuhimu wa harakati za ushairi katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Mashairi yaliyochanganuliwa ni yaliyo katika *Diwani ya Karne Mpya*.

Tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia maelezo ya istilahi umuhimu, usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya utafiti. Mengine yaliyoshughulikiwa katika sura ya kwanza ni yaliyoyandikwa kuhusu mada, msingi na mihimili ya nadharia ya Uhistoria-Mpya ambayo ilitumika katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data ya utafiti huu. Halikadhalika, sura hii ilishughulikia mbinu za utafiti ambazo ni pamoja na muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli ambapo mbinu

iliyotumiwa ni ya kimakusudi, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

Sura ya pili ilishughulikia miktadha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyoibua harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Mashairi teule yalichanganuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Uhistoria-Mpya kuwa, kazi zote za kubuni zaina muktadha wa kijamii na zina mahusiano yanayoingiliana. Aidha, Kazi za kifasihi ni matokeo ya uhusiano changamano wa mwingiliano matini na wala sio kazi zinazotokana na ubunifu wa mwandishi pekee.

Sura ya tatu ilishughulikia harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Kufikia lengo hili, mbinu mbalimbali za kuleta mabadiliko katika jamii zilibainishwa. Mashairi yaliyobainisha harakati hizi yalichanganuliwa kwa kina kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya Uhistoria-Mpya kuwa kusudi la mwandishi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria, kazi ya fasihi ambayo inahakikiwa pamoja na jamii husika.

Sura ya nne ilishughulikia umuhimu wa harakati za ushairi katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Umuhimu huu ulionyesha manufaa yanayotokana na harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko kando na kuwa na jamii isiyo na changamoto za kijamii, kiuchumi za kisiasa ambazo zilibainishwa kwa kina katika sura ya pili. Mihimili ilioongoza sura hii ni kuwa, chimbuko la kazi ya fasihi huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi. Aidha, suala la muktadha wa kijamii lazima liangaliwe upya.

Sura ya tano na ya mwisho ilishughulikia utangulizi wa sura ya tano, mukhtasari wa sura tangulizi, matokeo ya utafiti, changamoto na umuhimu wa utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yalitolewa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza miktadha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa iliyochochea harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadilko. Hii ni kwa mujibu wa nadharia ya Uhistoria-mpya iliyoongoza utafiti huu. Wahakiki wa nadharia ya Uhistoria –Mpya wanatambua umuhimu wa muktadha katika kazi za fasihi. Greenblatt (1980) kwa mfano anasema kuwa watunzi huathiriwa na mazingira yao na athari hizi hujitokeza katika tungo zao. Hivyo basi, kulikuwa na haja ya kuchunguza miktadha hii pamoja na uhusiano wa kimwingiliano matini. Miktadha ya kisiasa iliyochunguzwa ni, vipindi vya uchaguzi na siasa, ukoloni mamboleo, ufungwa na uongozi mbaya.

Utafiti huu ulibainisha kuwa, vipindi vya uchaguzi na siasa nchini Kenya hutawaliwa na ulaghai, unafiki, ahadi za uongo, propaganda na hogo. Wanasiasa hutumia mbinu hizi kwa lengo la kutenganisha wafuasi wao na wapinzani. Hali hii husababisha majuto miongoni mwa wananchi baada ya wao kuchagua viongozi wafisadi na wenye tamaa ambao, lengo lao ni kujinufaisha wenyewe huku wakinyanyasa wananchi.

Vilevile, ukoloni mamboleo ni tatizo ambalo linakumba nchi zinazoendelea Kenya ikiwamo. Utafiti huu ulibaini kuwa mataifa yanayoendelea yanatawaliwa, kudharauliwa

na kunyanyaswa na yaliyoendelea. Kinaya ni kuwa, licha ya uovu huu, mataifa yaliyoendelea yanahimiza mataifa yanayoendelea kukubali kuwa ulimwengu ni kijiji kimoja. Huu ni unafiki wa hali ya juu. Ilibainika pia, ukoloni mamboleo kando na kuendelezwa na mataifa yanayondelea, viongozi wa mataifa haya, wanaendeleza ukoloni mamboleo dhidi ya wananchi wenzao.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa, baadhi ya wananchi wanaojitokeza kupinga utawala mbaya hufungwa jela na kudhulumiwa ili kunyamazishwa. Mfano ni Abdilatif Abdalla alipojitolea kupinga utawala dhalimu wa chama cha KANU. Muktadha huu wa ufungwa ulimchochea kutunga mashairi kadhaa baadhi yakichora taswira ya dhiki aliyopitia pale gerezani. Pia yalieleza sababu yake kutiwa pale gerezani.

Utafiti huu ulibainisha kuwa, baadhi ya viongozi ambao huchukua hatamu za uongozi huwa na mapuuza, ufisadi, usaliti, utawala wa kidhalimu na unyanyasaji wa wananchi waliowachagua. Hujilimbikizia mali pamoja na sifa wasizostahili

Kwa upande mwingine, miktadha ya kijamii iliyochunguzwa ni pamoja na utabaka, ndoa za mapema, matunizi ya dawa za kulevya, maradhi, ubaguzi na ukengeushi. Utafiti ulibainisha kuwa, utabaka unaendelea nchini Kenya hata baaada ya uhuru. Yaani, kungali na mwanya mkubwa kati ya matajiri na maskini. Utabaka huu kwa kiasi fulani umesababishwa na ukosefu wa usawa katika ugawaji wa mali pamoja na uongozi unaoendeleza ukoloni mamboleo. Isitoshe, matajiri huwakandamiza maskini hasa wateteapo usawa.

Ilibainika kuwa, ndoa za mapema zinaathiri watoto wa kike hasa wale ambao bado wako katika umri wa kwenda shuleni. Elimu yao inapuuzwa huku ya mtoto wa kiume ikitiliwa maanani. Huu ni ubaguzi wa kijinsia uanomkandamiza na kumtweza mtoto wa jinsia ya kike.

Matumizi ya dawa za kulevya ni muktadha mwingine wa kijamii uliyoibua harakati za kuibadilisha jamii. Dawa hizi zinatumiwa na vijana hasa walio shuleni na hatimaye kuchangia machafuko katika jamii. Kwa mfano, wanafanya uvamizi na wengine kuishia kusahau nyumbani kwao baada ya kupata ajira kisha kujiingiza kwenye ulevi.

Maradhi kama vile Ukimwi, Kichomi, Ebola na Maralia, yangali tishio katika maisha ya binadamu. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya magonjwa kama vile Ukimwi, yanasababishwa na tabia ya uzinifu miongoni mwa wanadamu. Aidha, kupta matibabu ya baadhi ya maradhi haya si rahisi hasa miongoni mwa maskini.

Ubaguzi pia uliibua harakati za kujenga jamii yenye mabadiliko. Ubaguzi huu ni wa kiuchumi, kijinsia na hata kirangi. Utafiti ulibainisha kuwa mataifa yaliyoendelea yanabagua nchi zinazoendelea kwa misingi ya kiuchumi. Mataifa haya yanyanyasa nchi hizo kwa kuchukua zipandavyo mashambani pamoja na kuzilazimisha kuyasifu ili zipate msaada. Vile vile, wazungu wanabagua Waafrika na kusema wana ngozi ngumu. Aidha, viongozi wanaendeleza ubaguzi wa kimamlaka ambapo baada ya wao kupata mamalaka, wanawadhulumu wale ambao hawana uwezo kama wao. Utafiti huu pia ulibaini kuwa baadhi ya wanajamii wanaendeleza ubaguzi wa kijinsia. Kwa mfano, mtoto wa kike

anaachishwa masomo na kulazimishwa kuolewa huku wa kiume akipewa nafasi ya kuendelea na masomo.

Muktadha mwingine ulioibua harakati za ujenzi wenye jamii yenye mabadiliko ni ukengeushi. Utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya wanajamii wanatenda matendo ambayo ni kinyume na matarajio ya kijamamii. Kwa mfano ngoma waimbazo zimekosa makini na hivyo kukera kiasi cha kutoza machozi. Aidha haziaminiki na ni pujufu. Vile vile, wanawake wameacha kuvaa mavazi ya heshima na kuanza kuvaa yenye aibu kiachi cha kulalamikiwa na viumbe kama vile samaki. Kuna baadhi ya vijana pia ambao baada ya kupata elimu ya kigeni, wanaingilia ulevi, kuasi dini pamoja na kusahau nyumbani kwao.

Utafiti huu ulibaini kuwa miktadha mbalimbali ya kiuchumi ilibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Miktadha hii ni umaskini, ubepari na dhuluma za kibepari. Utafifi ulibaini kuwa baadhi ya wanajamii wamethiriwa na umaskini kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, wanakosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, malazi, matibabu na mavazi. Vilele, wanatengwa na matajiri. Isitoshe, maskini wanakosa hata pesa za kupeleka wanao shuleni. Hali hii ilichochea harakati za kuibadilisha jamii.

Vilevile, utafiti huu ulibaini kuwa, ubepari na dhuluma za kibepari viliibua harakati za ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Ulibaini kuwa, kutokana na utegemezi wa nchi za Afrika, Waafrika wanatumika kama vipanya vya majaribio ya kisayansi na kama malipo, wanapewa misaada ambayo pia si ya kuwafaa. Aidha, nchi za kigeni zinahodhi mazao ya mashamba ya nchi za Afrika.Ubepari pia unaendelezwa na Waafrika dhidi ya Waafrika

wenzao. Kwa mfano, waajiri wanafanyiza vibarua kazi ngumu pamoja na kuwalipa malipo duni.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubainisha za harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Utafiti huu ulibaini kuwa harakati za ushari wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko hazitokani na ombwe tupu. Miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa imechangia harakati hizi. Miktadha hii ilibainishwa kwa kina katika sura ya pili ambayo ilishughulikia lengo la kwanza. Uchanganuzi wa mashairi teule ulibainisha harakati kama vile, kuhimiza kumbukumbu za kihsitoria, kuhimiza umakinifu wa wananchi hasa wakati wa kampeni za uchaguzi na siasa, kuhimiza umoja, ushirikiano, bidii na uzalendo pamoja na kuhimiza ushirikiano katika kupiga vita mihadarati.

Aidha, ili kujenga jamii yenye mabadiliko, utafiti huu ulibaini kuwa ni muhimu kuonya matajiri dhidi ya dharau hasa kudharau maskini, kuhimiza uvaaji wa mavazi ya heshima, kuhimiza maskini kutia bidii, kuwasuta na kuwaonya mabepari, kuhimiza tahadhari dhidi ya ukimwi, kuhimiza usawa wa kijinsia pamoja na kukashifu ukoloni mamboleo na ubaguzi wa kimataifa. Lengo hili lilifanikishwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Uhistoria-Mpya kuwa lengo la mwandishi wa fasihi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria, kazi ya fasihi ambayo inahakikiwa pamoja na jamii husika. Aidha, chimbuko la kazi ya fasihi huathiri uhakiki na ufasili wa matini ya kifasihi. Miktadha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kijumla, ilibainika kuwa iliathiri mawazo ya watunzi wa mashairi kwa namna ya kuchochea kauli za kuleta mabadiliko. Utifiti huu ulijikita katika jamii ya Kenya ambapo utafiti ulirejelea baadhi ya vipindi vya kihistoria nchini Kenya.

Lengo la tatu lilikuwa kuonyesha umuhimu wa harakati za ushairi katika ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Utafiti huu ulionyesha kuwa harakati hizi zina umuhimu hasa katika jamii ya sasa kwa kuwa zinasawiri manufaa ya ushairi katika jamii pamoja na kuangazia haja ya kujenga jamii adilifu. Yaani jamii isiyo na matatizo kama yaliyochimuzwa na miktadha ya kiuchumi, kisiasa na kijamii iliyobainishwa katika utafiti huu. Utafiti huu umedhihirisha kuwa harakati hizi zina umuhimu kama ifuatavyo: kuelewesha wanajamii kuhusu unafiki wa mataifa yaliyoendelea na pamoja na unafiki wa viongozi wa mataifa yayoendelea, kudumisha historia, kudumisha utamaduni mwafaka wa Afrika na kukuza uwajibikaji wa washikadau katika vita dhidi ya matumizi ya mihadarati. Umuhimu mwingine wa harakati hizi ni kumaliza udhalimu na ubepari, uzembe na utegemezi miongoni mwa wanajamii na kumaliza maradhi kama vile Ukimwi. Halikadhalika, harakati hizi zinanuia kukuza usawa wa kijinsia pamoja na kuziba mwanya wa utabaka ili kukuza usawa wa kitabaka na kijinsia. Lengo hili lilifanikishwa na mhimili kuwa suala la miktadha na utamaduni wa kijamii halina budi kuangaliwa upya.

### 5.3 Changamoto za utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto ambazo zilitatiza ukamilishaji wa shughuli nzima ya utafiti kama ilivyokuwa imekadiriwa. Moja ya changamoto hizi ni kuwa, wakati wa utafi huu mtafiti alikuwa ajirani. Kwa hivyo, ilikuwa changamoto kubwa kupata nafasi ya kusafiri kwa ajili ya maelekezo pamoja na kuomba vitabu katika matibaa ya chuo.

Changamoto nyingine ni kuingiliana kwa miktadha hasa ya kijamii na kiuchumi iliyozua utata katika uchanganuzi wa mashairi ili kupta data. Vilevile, ilikuwa kazi ngumu

kuielewa miktadha halisi iliyoangaziwa katika mashairi yaliyoteuliwa kwa ajili ya kufanikisha utafiti huu.

## 5.4 Umuhimu wa utafiti

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa, utanzu wa ushairi kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi; una jukumu kubwa katika jamii. Utanzu huu unaweza kutumika kusawiri hali halisi ya jamii pamoja na kuirekebisha jamii. Utafiti huu uliweka bayana njia mbalimbali ambazo wanajamiii wanaweza kuzitumia ili kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanaikumba jamii ya sasa.

Vilevile, utafiti huu uliweka msingi wa tafiti za awali zinazohusiana na ujenzi wa jamii yenye mabadiliko. Aidha, utafiti huu ulidhihirisha kuwa fasihi na haswa ushairi wa Kiswahili unaweza kuhakikiwa kinadharia.

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kubainsha harakati za ushairi wa Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya. Aidha, ulibainisha miktadha ya kiuchumi, kijamii na kisiasa iliyoibua harakati hizi. Mashairi yaliyochanganuliwa ni ya watunzi kutoka nchini Kenya. Utafiti zaidi wa aina hii unaweza kufanywa katika tanzu nyinginezo za fasihi. Pia, mashairi kutoka nchi nyinginezo yanaweza kutumiwa katika utafiti zaidi wa aina hii. Utafiti huu uliongozwa na Nadhari ya Uhistoria-Mpya, utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

# MAREJELEO


Foucault, M. (1997). *The Order of Things.London*: Routeledge and Kegan limited.

Cartey, W na Kilson,M.(1970).African Reader:Colonial Africa.Newy York.Random House

Christopher, A.J. (1984) Colonia Africa. New Jersey: Barne & Noble Books.

Kapiyo, et al. (2011). The Evolving World: A History and Government Course (Form 3). Nairobi: Oxford University Press

Kapiyo, et al. (2011). The Evolving World: A History and Government Course (Form 4). Nairobi: Oxford University Press.

*Kenya - Country Assistance Strategy Progress Report (English).* Washington, D.C.:WorldBankGroup. http://documents.worldbank1.org/curated/en/460 511468089365037/Kenya-Country-Assistance-Strategy-Progress-Report

Kenya Literature Bureau (2017). Secondary History and Governemt (Form Four). Nairobi.

Kimeu, A.N. (2016). *Maudhui ya Ukombozi Katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti*.Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo*.Nairobi: Phoenix Publishers.

Kiongera, K.J. (2012). *Mchango wa Vijana katika Kuketa Mabadiliko Chanya katika Tamthilia Teule za Kiswahili*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kombo, K.na Tromp, A. (2006). *Proposal and Thesis Writing. An Introduction.*Nairobi: Pauline Publishers.

Manoti, J.K. (2012). *Dhamira ya Uozo na Athari zake kwa Jamii, katika Riwaya ya Upotevu:* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Masinde, E na Wanyela, L.(2025). Mchango wa Ken Walibora Waliaula katika Maendeleo ya Taaluma na Jamii.Fasihi na Masuala Ibuka1(1): 149-160

Masinde, E. (1992). *Dhamira na mtindo katika mashairi huru*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinde, E. (2003). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya maudhui*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinde, E. (2024). Nafasi ya Ushairi katika Harakati ya Kujenga Jamii Mpya.Ukuzaji na Maendeleo ya Kiswahili.143-157

Masinde, E. (2024). Nafasi ya Ushairi wa Kiswahili katika Harakati za Ujenzi wa Jamii

Mberia,K.(2001).Bara Jingine.Marimba Publishers Ltd.

Mlacha, S. (1984).*'Riwaya za Visiwani (1970 -1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya'* katika Mulika na. ya 16. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mugambi, E.K. (1987). *Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*: Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Nasimiyu, M.C. (2016). *Athari ya Mazingira ya Kihistoria na Kijamii katika Uwasilishaji wa Maudhui ya Dhifa* (E. Kezilahabi). Tasnifu ya Shahada ya Uzamil.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ndung'u, J.M. (2019). Usawiri wa Vijana Katika Ujenzi wa Jamii Mpya Katika Riwaya Teule ya Kiswahili.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Laikipia.

Ndungo, C.(2024) . Mchango Profesa Mbaabu katika Kuelewa Utamaduni wa Waswahili. Ukuzaji na Maendeleo ya Kiswahili.55-74

Omoga, R.G. (2018). Mwananchi wa Kawaida Kama Mdhulumu wa Maslahi Yake Katika Tamthilia za Kilio cha Haki, Amezidi na Mstahiki Meya.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Orodho, A. (2005). Elements *of Education and Social Science Research Methods*.Nairobi: Masola Publishers.

Osango, D.S. (2015). *Ukombozi wa Kisiasa na Kiuchumi Katika Mkamadume*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sanja, W.L. (2012). Maudhui ya Ndoa na Dini Katika Riwaya za Kala Tufaha na Paradiso.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Thuranira, I.S. (2017) Maudhui ya Ukoloni Mamboleo katikaTamthilia Teule Za Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Wafula, C.N. (2015). Mgongano wa Utamaduni Katika Hadithi Fupi za Kiswahili.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Wafula, R.M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2007). *Diwani ya Karne Mpya*.Phoenix Publishers Ltd.Nairobi.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*.Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi : Istilahi na Nadharia* : Focus Publications.Ltd.

Wangeci, A.N. (2014). Viongozi Kama Visababishi vya Mabadiliko Katika Riwaya za Mwenda Mbatiah : Vipanya vya Maabara na Majira ya Tufani.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi

## VIAMBATISHO:

### Mashairi teule

*KUMEKUCHA*
*Abdilatif Abdalla*
*Kumekucha! Imengiya asubuhi! Kumekucha! Siku imepambazuka!*
*Kumekucha! Wote umma tufurahi, miale ya juwa sikuyamulika*
*Kumekucha! Itwambae ikirahi, na nyoyo zetu ziwe kutukunduka*
*Kumekucha! Mbingu zapiga siyahi, na ardhi nayo piya yatibwirika!*
*Kumekucha! Kwanukiya njema rihi! si ya ule uvundo wenye kunuka*
*Kumekucha! Mwishowe 'metanabahi, giza limetishika ma kutimka!*
*Kumekucha! Ni kwamba 'mekosa zihi, jogoo leo limeshindwa kuwika!*

*Kungakucha! Na juwa lingaangaza! Kungakucha! Nyoyo zingatabasamu*
*kungakucha! Sauti anagpoteza; Jogoo mambo yamgamwiya magumu*
*Kungakucha! Sauti tungazipaza, kwa shangwe siku mpy kuisalimu*
*Kungakucha! Daima tuwe kuwaza, tutokako kukumbuka ni muhimu*
*Kungakucha! Tukumbuke walonwesheza, mti wa ukombozi kwa zao damu*
*Kungakucha! Tusianze kubwagaza, iloyukabili ni kazi ngumu*
*Kungakucha! Tusirudi kujilaza, tukalala na kupotewa fahamu*
*Kungakucha! Lisije kutupumbaza, juwa likatuwiya mbuwaji sumu*
*Kungakucha! Waweza ibwa mwangaza, ikaja hasirika tena kaumu*
*Kungakucha! Tujihadhari na giza, kwani laweza rudi kutuhujumu!*

*TAZAMA*
*Tazama utaona*
*Maskini wanaoishi katika dhiki za karne*
*Fukara wanaodidimia katika kinamasi cha dhuluma*
*Fakiri wanaogugunwa mili na michonge wa tabaka*
*Wakiwa wanaokufa njaa kwa kukosa cha kujilia*
*Maskini wanaoteswa kwa kuililia auni*
*Umma unaolia kwa kuikosa nafuu*
*Kwa kupakosa pa kulala*
*Kwa kukikosa cha kuvaa*
*Kwa kuyakosa matibabu*
*Kwa kuyakosa maisha*
*Tazama kisha utaona*
*Vitambi vinavyotetemeshwa na uto wa nyama*
*Shingo zinazoshabihiana na mibuyu ya pwani*
*Mili iliyonenepeana tamthili ya kiboko*

*Vinywa vinavyokula na kusaza kwa wingi*
*Macho yasiyopenda kuona uhalisi*
*Tazama tena, kisha utaona*
*Wanasiasa wanaojisifu kwa maendeleo*
*Mawaziri wanaorejareja sifa za sera za nchi yao*
*Wanadini wanaoimba kwa kupagawa*
*Na kiongozi anyesjisifia kipaji cha kuona mbele.*

*NIGUSE*
*Nitokapo kizuizini*
*Nitamwomba yoyote mwendani*
*Aniguse*
*taratibu*
*polepole*
*lakini*
*kwa yakini*
*Niguse tena*
*Unijuze tena*
*Unifunze tena*
*maisha yalivyo*
*maisha yaonjavyo*
*ladha ilivyo*
*Nipo hapa nimekubali*
*Niguse tena tafadhali!*
*Niguse!*
*Niguse!*

*MSITU NI ULE ULE*
*Hitaraji yuungane, undugu ututawale*
*Hataka tushikamane, kama pete na kidole*
*Kumbe bwana ni dengene, wakuu wetu wawale!*
*Msitu ni ule ule, na fisi ni wale wale!*

*Waimbe waonekane, kwamba wajali watule*
*Siku nenda wambizane, ujima waulekele*
*Hoja tuheshimiane, na amani teletele*
*Ela mwitu ule ule, na fisi ni wale wale*

*Vigogo waumbuane, matayo paisi sumile*
*Na mara watukanane, wapigizane kelele*
*Eti kisa twondokane, na ya uhasama ndwele!*
*Bado mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!*

*Sikuye wapapurane, maguvu waamilile*
*Muda wasisemezane, ja mahasimu wa kale*

*Wakae wasikizane, warejee pale pale*
*Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale*

*Uwadhani, watengane, wadumu hivyo milele,*
*Ghafula waungamane, ubaki kuliya ole!*
*Maadui wapatane, watakapokaa wale,*
*Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!*

*TUJENGE NTI WANATI*
*Mimi naunga mkono, naunga wazo thabiti*
*Umoja wetu wanati, katika kujenga nti*
*Ndilo jambo madhubuti, linalofaa wanati*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

*Kila raia wa nti, anayo haki ya nti*
*Kutoa wazo thabiti, kushiriki harakati*
*Ili msingi wa nti, upate kujithibiti*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

*Mzalendo madhubuti, ni yule mpenda nti*
*Akakataa unyeti, serikali kusaliti*
*Asikiubali katiti, kutoa siri z anti*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

*Haya shime wananti, tujumuike umati*
*Tusirefushe uteti, viama kuweka kati*
*Msingi wetu ni hati, tufanye kazi kwa dhati*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

*Tusikubali wateti, ambao nia ni vitu*
*Bungeni kwenda manoti, nakunyakua ploti*
*Na huku nyuma mauti, kutukamua matiti*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.*

*Kura iwe ndio cheti, ukabila ni mauti*
*Sio kupenda manoti, kuhongwa kati kwa kati*
*Ngao iwe ni tikiti, kadi zetu tuzatiti*
*Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati*

*Rasilimali za nti, mbuga za pori na miti*
*Vifaru, ndovu na nyati, utamaduni mufti*
*Tukazie harakati, raha yetu wananti*
*Mjenga nti mwanti, mvunda nti mwanati*

*Uwe Jaluo Hakati, au Mkamba Kaiti*

*Mandi Eldoreti, au Kikuyu wa Kati*
*Umoja wetu wanati, ndio msingi thabiti*
*Mjenga nti mwanti, mvunda nti mwanati*

*KUNO KUNENA*
*Kuno kunena kwa nini, kukanikomeya kuno?*
*Kwani kunena kunani, kukashukwa kani vino?*
*Kani sio kiini, kuninuniya mno*
*Kanama nako kunena, kwaonekana ni kuwi*

*Kana na kuku kunena, kunenwa kakutakiwi*
*Kuna wanakokuona, kunena kwamba si kuwi*
*Kunena wakikuona, kukuita kawakawa*
*Kunena kana kwanuka, nikukone kukunena?*

*MCHOCHOLE*
*Mchochole amezongwa na matatizo kibao*
*Magerezani hufungwa, uhuni yeye anao*
*Mara nyengine, hunyongwa, kwa uhuni afanyao*
*Mwenye njaa ametengwa, katengwa na washibao*
*Msaidieni naye, apate jitegemea.*

*Mchochole asemapo atafuta kibarua*
*Mara chache apatapo, kilipacho sawasawa*
*Madogo huwa malipo, kwa chakula kununuwa*
*Mchochole hapo hapo, na nyongo hutumbukiwa*
*Mchochole afanyeje, kujikimu kimaisha*

*Mchochole hana pesa, malipo kugharamia*
*Mwana aende Mombasa, kupata teknolojia*
*Maisha yanamtesa, japo yuwavumilia*
*Mwisho hufanya makosa, pasi na kutarajia*
*Maisha yake gharama, huwa hajimudu katu*

*Mara nyingi mchochole, hukumbwa na maonevu*
*Maradhi tele kwa tele, huwa kwake uzoevu*
*Mara alia upele, mara alia na mbavu*
*Matibabu kuaptile, bila pesa hana nguvu*
*Maskini yuwachapwa, na kiboko cha maisha*

*Mungu Mola mbariki, mnyonge umnusuru*
*Mgawie yake keki, ya matunda ya uhuru*
*Mpatie naye haki, apate kuona nuru*
*Mwondoshee hizi dhiki, ewe Yarabi ghafuru*
*Mchochole usilie, iko siku yatakwisha.*

*KILIO CHA AFRIKA*
*Pilikeni kilio kilotawanyanika*
*kwa huzuni kikibashiri*
*hatari ilojisimika*
*na uwele kukithiri*

*Shuhuduni utu ukiumbuka*
*ukikatwa yake dhakiri*
*na beberu akitucheka*
*kwa shibe ya kutughuri*

*Tazameni miji ikinyongeka*
*kwa magugu ya ubepari*
*na madhila yakituzika*
*yapta yakijikariri*

*Engani kiza kilojitandika*
*tabaka zilo dhahiri*
*Afrika ikipepesuka*
*kwa pepe zilovinjari*

*Oneni wakati ukitimika*
*kama moto wenye mori*
*na mwisho kutufunika*
*kama wimbi la bahari.*

*MIHADARATI SHULENE*
*Taasisi zachafuka, hazikaliki jamani*
*Moto mui unawake, doria ashike nani*
*Taifa lafadhaika, wana wawa maluuni*
*Mihadarati shuleni, yachangia machafuko*

*Yachangia machafuko, mihadarati shuleni*
*Tufanye gani tambiko, atuauni Manani*
*Yanazidi maudhiko, wavyele wa simanzini*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Uvamizi washafanya, walanguzi wa shuleni*
*Kama jeshi la tekenya, linavamia wayoni*
*Silo lao 'kiwakanya, hawajali asilani*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Wazazi zenu dinari, zinapofika bwenini*
*Mtaji wa hino shari, chanzo zha uhayawani*

*Haiwi heri fahari, hela nyigi mifukoni*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Uraibu ushakita, hili lakata maini*
*Viwango vimeshapita, laning'inia la zani*
*Pakubwa sote twajuta, hini taaluma gani*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Wanolewa wanahaha, mazuri hawatambui*
*Kawatandia ujuha, hawatambui kunani*
*Na ushauri-nasaha, kwao wao haufani*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Changamoto natupia, serikali kilingeni*
*Ni mrefu wa sheria, mkono wake nadhani*
*Azimio zingatia, kusukumiza mbaroni*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko*

*Jamii ina jukumu, mijini na vijijini*
*Wahasiriwa wa humu, dawa hizi tupingeni*
*Seikali haimudu, pasi kondo faraghani*
*Mihadarati shuleni, yachangia michafuko,*

*KESHO YANGU*
*Sidhani ni kichekesho, kesho kuwepo sidhani*
*Vilivyoko ni vitisho, viwewe na visirani*
*Mimi kupe kwenye josho, la sumu iso imani*
*Kesho yangu imeshaliwa*

*Kesho yamgu imeshaliwa, isibaki hata kitwa*
*Kwamba hai nitakuwa, kesho na kesho kutwa*
*Hilo haliwezi kuwa, na wakati limepitwa*
*Na iwapi kesho yangu?*

*Sikwambii mtondoo, au ni mtondogoo*
*Ajapowika jogoo, kesho sipo mg'oo*
*Hata simu za "haloo", hazinipati "haloo"*
*Ninaituhumu kesho.*

*Kesho ninaituhumu, kwa sababu ya hasama*
*Hasama ya mahasimu, walioshana njama*
*Kutaka kunihujumu, wanizulie nakama*
*Itokapi yangu kesho?*

*Wa kwanza huyu Ukimwi, daima aniotea*

*Kwa dawa huyu hazimwi, haachi kuturingia*
*Amekuwa kama zimwi, mtu lisilomjua*
*Ati nipangie kesho?!*

*Nipange yangu matanga, au kujenga nyumba*
*Nipange kung'oa nanga, au shairi kuimba?*
*Nipangeni cha kupanga, biashara za mtumba/*
*Kesho si ukoo wangu.*

*Ukimwi nduguze wako, Ebola na Malaria*
*Kichomi na sekeneko, mno wajifaragua*
*Maadamu wanagliko, vipi kesho kuwazia?*
*Kesho si ndu yangu mwandani*

*Mimi napangia leo, maana kesho sijui*
*Usafiri nifanyao, kwenye vyombo anuwai*
*Una mikasa kibao, majanga ya kila nui*
*Salama yangu I wapi?*

*Iwapi salama yangu, huku wapo wa kijicho*
*Ngaa nipatapo changu, waingiwa mpekecho*
*Kunipikia majungu, nikikosa changu hicho*
*Waso nitakia kesho*

*Kesho waso nitakia, watele kama siafu*
*Majambazi nasinzia, tapeli na wazinifu*
*Roho yanguwapania, kunipeleka wa ufu*
*Nipewe jina" hayati"!*

*MTU NA UTU*
*Nawaita wanakwetu, mje tucheze kikwetu*
*Jongeeni nyatu nyatu, tuimbe huno utatu*
*Mjue mtu na utu, asiye utu si mtu*

*Mtu akikosa utu, kikwetu haitwi mtu*
*Tunawita mbwa mwitu, ndani ya kundi la watu*
*Lakini mwinyi na utu, hutambuliwa kiutu*

*Kwa mja mwiyi na utu, hushika hili kukutu*
*Haropoki katu katu, matusi kwake mtutu*
*Bure huitwa kurutu, akavumbikwa msutu*

*Muerevu mwenye utu, huishi ndani na watu*
*Hatukuwi utukutu, ushari na ukurutu*
*Bure huwa sokwe mtu, ama mnyama wa mwitu*

*Mtu akiitwa mtu, siye mvaa sapatu*
*Aweza akawa jitu, lenye miraba mitatu*
*Asipoheshimu watu, hupungukiwa na utu*

*Ninaposema kiutu, si kwenda kimatumatu*
*Wenye fahari na vitu, kuona watu si watu*
*mali na mtu si kitu, upungukiwapo utu*

*Kwenye mashirika yetu, kuna baadhi ya watu*
*Hawafai kuwa watu, si joka wala si chatu*
*Usafi pia ni utu, aso safi ni butu*

*Kaditama wanakwetu, naufupisha utatu*
*Tupaoishi na watu, tuzingatieni utu*
*Asiye utu ni kutu, Kimungu pia kikwetu.*

*MUWEREVU HAJINYOI*
*Mwenye nacho wajishasha, wajiona kama ndovu*
*Kitu kimekulewesha, huutambuwi uovu*
*Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

*Tangu ukite kwa kitu,'megeuka mpumbavu*
*Kattu kuthamini mtu, ambaye kwamba mtovu*
*Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

*Wangapi 'meonekana, mibakhili mishupavu*
*Waliyo wakijitoma, na mwingi usuluhivu*
*Leo hawanasi tena, wageukile maivu*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

*Kupata kusikughuri, ukidhani muwerevu*
*Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu*
*Iko siku itajiri, ujikute mwenye wavu*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

*Kila mwenye kukuonya, uiwate ndiya mbovu*
*Huchelewi kmminya, kumvunda zake mbavu*
*Fanya ambayo wafanya, bada ya mbiti ni mbivu*
*Tangu lini muwerevu, akajinyoa mwenyewe?*

*AJALI IKIDHIHIRI*

*Omar Babu (Abu Marjan)*
*Ajali ikidhihiri, wala haina cha hela,*
*Haimjui fakiri, ijapo ambe hewala,*
*Inamkumba tajiri, akabaki shelabela*

*Siku ya siku hujiri, kwa misingi ya Jaala*
*Huwatukia viburi, wasazacho ni salala,*
*Walotanua suduri, hujiondokea bila*

*Kila atendao ari, alojipa maghafala*
*Yasibu kujihadhari, kufanya sitahamala*
*Hazina tija kikiri, hatima mtu hulala*

*MAVAZI*
*Mavazi ya kina mama, sikizeni*
*Ni kigezo cha heshima, akilini*
*Katujalia Karima, kumbukeni*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Samaki wanalalama, maziwani*
*na nyuni wameachama, wa anagani*
*Mahuluki wazizima, ardhini*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Ya dhati huwa heshima, ya moyoni*
*Si kwamba iwe lazima, sheriani*
*Tubwage mbali tuhuma, kaumuni*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Ubakaji unavuma, duniani*
*Twachochea uhasama, tizameni*
*Wa jinsia daima, ukinzani*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Mnada waja wasema, twanadini?*
*Tuvaeni huko nyuma, upenuni*
*Umati utatukoma, maskini*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*Vingine zitatuhama, tamaduni*
*Bara letu litazama, utumwani*
*Wapi tutapisimama, duniani?*
*Magauni ya heshima, tuvaeni.*

*Ni mama mwenye heshima, na razini*

*Mvaa mavazi mema, hadharani*
*Langu bovu nalitema, abadani*
*Magauni ya heshima, tuvaeni*

*ELIMU ADHIMU*
*Utatukuka daima, na watu wakuheshimu*
*Upalizwe taadhima, na kuonwa maasumu*
*Katika kundi la wema, lenye watu maalumu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Kuandika na kusoma, ni jambo lilo muhimu*
*Siku hizi ni lazima, kila kiumbe timamu*
*Kila kitu kitakoma, usipopata elimu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Ukishajua kusoma, na shuleni uhitimu*
*Itafute taaluma, chuoni tena kwa hamu*
*Kazi uzijue vema, uajiriwe kwa zamu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Elimu ndio uzima, unaokutupa naumu,*
*Ndiyo njia ya salama, tena ya kutabasamu*
*Ni hazina ya daima, isiyoisha utamu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Someni akina mama, kina baba na ghulamu*
*Mtaziepuka njama, zenye madhila magumu*
*Taifa lililo wima, hutegemea elimu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Ndiyo njia ya dalama, yafaa kila hirimu*
*Ya msingi ulo mwema, wenye maisha matamu*
*Tujifunza hima hima, liwe ni letu jukumu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima*

*Wakaditama watama, wakatabahu nudhumu*
*Yatosha niloyasema, kuwambia binadamu*
*Elimu tukiipima, ujinga kwetu adimu*
*Elimu kitu adhimu, binadamu ni lazima.*

*KUTELEZA SIKU HIZI*
*Douglas Mutua*
*Wingu jeusi latoka, kusi hadi kaskazi*
*Mashariki ladondoka, magharibi si ajizi*
*Mno tuna shaka shaka, twatapa ja sisimizi*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.*

*Roho zinatifilika, kuwahiliki mahiri,*
*Wanaochovya gharika, starehe ya dahari*
*Kina cha mto kumbuka, ki tuli haki kikiri*
*Siku hizi kiuteleza, hakika ni kuanguka*

*Ukithubutu wazama, muda wa toba hupati*
*Ukichovya ni kama, kalmia iwe laity*
*Na yetu bure huruma, waama ni tashititi*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka*

*Hutelezi ukaima, naamba wazi sifumbi*
*Pulika haiwi homa, ungawa nao ujimbi*
*Sambe mzizi hatoma, nyendoze zina mlimbi*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka*

*Nafaka ashasumbusha, dungundungu simuoni*
*Majibwa anagurisha, hawanusuriki nyani*
*Ya mbwa chunga maisha, nyani kaidi ta'bani*
*Siku hizi kuanguka, hakika ni kuteleza*

*Kokote kuna mauwa, ela mengi yana sumu*
*Yosayosa yanauwa, anayenusa hadumu*
*Bora jangwa kutengewa, kuepuka chungu tamu*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka*

*Hamna kamwe shufaka, hupati wala shufaa*
*Hatima ya kuteguka, tiketi kuangamia*
*Mzuri wa kupulika, afaa kuchanjamaa*
*Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka*

*KWENDA MBIO SI KUPATA*
*Omar Babu (Abu Marajan)*
*Haliwi lisilokuwa, lililo lako huchata*
*Mambo yamekadiriwa, ya ukwasi na ukata*
*Mja kujititimuwa, si ajabu akadata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki majaaliwa*

*Mafungu yamegawiwa, gaolo halitopita,*

*mara mtu hwangukiwa, jaza kitita kitita*
*Mwengine hupungukiwa, tajiri awe mkata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki ni majaaliwa*

*Haikhalisi kutuwa, kuzengea ukasita*
*Ela shughuli elewa, ada kipato huvuta,*
*Pana siku huambuwa, tena kuna kula mwata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki ni majaaliwa*

*Uzembe sio muruwa, ni wajibu kutafuta*
*Kutwa na jaa kutuwa, guu njiani wafata*
*Lakini mtegemewa, akwondoleaye tata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki ni majaliwa*

*Bahati zimepangiwa, muweza mezichanyata*
*Kwa mgao huizowa, yako ijapo kamata*
*Kwengineko hitotwawa, huna haja kukangata*
*Kwenda mbio si kupata, riziki ni majaliwa*

*TUTAKULA NINI?*
*Umezembeazembea, tangia hapo fulani*
*Magharibi yajongea, huna kitu asilani*
*Kuno wanotegemea, kulishwa nawe mwandani*
*Walaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*Hakikaninashangaa, hujali wala hubali*
*Wanao walala njaa, hushughuliki shughuli*
*Mavazi yamechakaa, yatia kiwewe hali*
*Walaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*Uzembe umekutwa, akili ukakuteka*
*Mjini wasumbukia, nyumbani huwezi fika*
*Hupendi kupalilia, kuvuna, ntingi nafaka*
*Walaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*Ni heri kuzingatia, jukumu lako fulani*
*Kuliko kuyachelea, maisha ya duniani*
*Aushi yako walia, haupo kuwaauni*
*Walaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*Godoro walilalia, macheo hadi machweo*
*Rauka nakuusia, wakati wako ni leo*
*Ukome kubingiria,usende kwenye vikao*
*Walaza damu daima,mwisho utakula nini?*

*Kumekucha angalia, shughuli gani gizani*
*Kumetupambazukia, tukagure utumwani*
*Hali huku wadandia, chombo kiso usukani*
*Walaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*ni heri kuriaria, chungucho kiwa mekoni*
*Allahu tukujalia, uzembe,'sipotamani*
*Neema kuzidishia, ni kzi yake Manani*
*Walaaza damu daima, mwisho utakula nini?*

*KILA MPENDA HARAMU*
*Heri utwae rukwama, utambe hadi Watamu*
*Yakunyauke matama, kwa kupiga baragumu,*
*Kuliko uwe kadama, wadhalili binadamu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

*Heri na uwe yatima, huli haramu ya tamu*
*Na uwe tena adhima, japo huwahi adimu*
*Kuliko nyama ya kima, kesho wende jehanamu*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

*Heri unyimwe heshima, uitwe mwenda wazimu*
*Kula ule manyama, na kuitwa maalimu,*
*Na kesho mbele ya umma, uzikwe wende kuzimu,*
*Kila mpenda haramu, itamsibu nakama*

*Heri unyimwe heshima, utukanike bahimu*
*Kuliko uwe u wima, na mali ya kulazimu*
*Kesho ukose salama, ikikupata hukumu,*
*Kila mpenda haramu, ingamsibu nakama*

*Namba nanyi mlo wima, mliopewa jukumu*
*Mlioajiri umma, kupenda kutudhulumu*
*Kuna siku ya kiyama, ameipanga Rahimu*
*Kila mpenda haramu, ingamsibu nakama*

*Wakatabu watama, zatosha hizo nudhumu,*
*Maadamu unga wima, usipate kwa haramu*
*Duniani tenda wema, atakulipa Karimu*
*Kila mpenda haramu, ingamsibu nakama*

*JIKANYE*

*Juta*
*Lia na wana wako waliotwaliwa na mwinyi*
*Lilia na wale wengine waliofia vitani*
*Angua kilio kwa wengine waliofanywa mashine*
*Sikitika na hao waliodhalilishwa jana*
*Omboleza na wengine walioteswa na nduguyo*

*Cheka*
*Ucheke ujinga wako wa kumwamini jamabazi*
*Ucheke ujuha wako wa kumhongera malanguzi*
*Ucheke ubwege wako wa kumtunuku pwaguzi*
*Ucheke upumbe wako wa kumzawidi mwizi*

*Kemea*
*Suta yako yaliyokurubuni mchana*
*Kengemeka akili yako iliyotattwa na fumbo*
*Subukia na kinywa chako kilichomsifu dhulumati*
*Kanya na sikio lako lililouzibia ukweli*
*Subu na pua yako isiyonusa hata uozo*
*Jikanye*
*Usimwite kaini mja wa kutajika*
*Usimsifu mwokozi kumbe pwaguzi*
*Usimtukuze hakiri kumbe chakari*
*Usiseme tena, hili ni wingu la kupita!*

*MKESHA WA MWAKA MPYA*

*Mkesha wa mwaka mpya, ndiyo mada ya shairi*
*Ninayosema si mapya, ni dhahiri siyo siri*
*Mambo tunayoyafanya, napania kukariri*
*Pole pole tutamenya, hata wenye makasiri*

*Majumba ya tafrija, hujaa watu sisisi*
*Tena huzuka vioja, kama kutenda matusi*
*Sitasahau kutaja, burudani huwa kasi*
*Mabingwa hupiga mbinja, kujishaha jukwaani*

*Takriban kanisa, zote huwa na ibada*
*Wengine huwa na misa, na maombi ya ziada*
*Waja pia hutakasa, kanisa walizound*
*Sakafu watu hutesa, kwa miguu wakidunda*

*Pia hubeba ahadi, za uongo na ukweli*

*Watu huwa mashahidi, wa kuzitenda fadhili*
*Wengi hutaka, ushindi, wa kuitwa afadhali*
*Na wachache huwabidi, kuungana ufidhuli*

*Ni siku ya uzinifu, kwa mabinti na gulamu*
*Tena kweli bainifu, huzaa wanaharamu*
*Hizi kazi za siafu, hatimaye huwa sumu*
*Wachache hujinyarafu, kwa hili lililodumu*

*Tarakimu zaonyesha, na ukimwi huzagaa*
*Ni mvua inanyesha, na kwa taifa ni baa*
*Ama kweli linatisha, ndiposa tunanyamaa*
*Muhimu kubadilisha, kujitenga na balaa*

*Ni siku yenye mitego, kama vile kupigana*
*Wasotumia ubongo, hata visu hudungana*
*Wezi huvunja milango, wasivyopanda kuvuna*
*Hapa hamna uongo, ni nususi ninanena*

*Wamilikio mabaa, hupata fedha si haba*
*Mapema hujiandaa, kwa vinywaji vya kukaba*
*Kwa hiyo si fadhaa, ni faida wanumba*
*Wanaume huzubaa, waonapo makahaba*

*Usingizi hutoweka, kutokana na kelele*
*Keshoye ukiamka, wavamiwa na malale*
*Wabaki ukiteseka, kana kwamba una ndwele*
*Ama ukimakamaka,'kiumauma vidole*

*Kaditama wa tamati, karibu kwa mwaka mpya*
*Acheni yale tititi, yadhuruyo zenu afya*
*Msibaki katikati, kutojua la kufanya*
*Nimefanya utafiti, awali ya kukuonya*

*SIOLEWI*
*Nina habari kamili, naozwa hali nasoma*
*Nalia sili silali, nakerwa na hino njama*
*Elimu kwangu halali, ndoa sitamani mama*
*Ninasoma siolewi!*

*Ninahitaji alimu, japo mie msichana*
*Elimu nguzo muhimu, na yenye kubwa dhamana,*
*Kwani kosa gani humu, kuzaliwa msichana*
*Ninasoma siolewi!*

*Dhana kwamba mvulana, akisoma afadhali*
*Mashiko kamwe haina, ni bure ukatatili*
*Kuoa na kuoana, kwangu sasa kubwa feli*
*Ninasoma siolewi!*

*Wapo wake mahashumu, wasomi nana pulika*
*Wahimili kuzikimu, aila zao hakika*
*Mahari hayatokimu, elimu ghala la nyaka*
*Ninasoma siolewi!*

*Nina mawazo fahamu, japo ubwabwa shingoni*
*Wazazi nitalaumu, endapo sendi shuleni*
*Kisomo kunidhulumu, sema kwa sababu gani?*
*Ninasoma siolewi!*

*Wa nikaha utatimu, muda niozwe mzima*
*Ela sasa ni haramu, elimu yangu kuzima*
*Kuoza mwenye elimu, huwa kuu taadhima*
*Ninasoma siolewi!*

*KIBARUWA*
*Kwenye shamba hilo kubwa asilani hakunyi mvuwa!*
*Ni kwa mitilizi ya jasho langu ndiyo hunweshezwa*
*Kwenye shamba hilo kubwa sasa imeshaiva kahawa*
*Na bunize ni matone ya damu yangu niliyotowa*
*Ndipo mt ukatipuza!*

*Buni hiyo itakaangwa buni hiyo itapondwapondwa*
*Buni hiyo itasagwa na buni hiyo itafyondwa fyondwa*
*Bali itabaki nyeusi kama ngozi yangu Kibaruwa*

*Waulize ndege kwa nyimbo nyanana watutumbuizao*
*Iulize na mito kwa furaha maji itiririkapo*
*Uulize na upepo mkali kwa ghadhabu uvumao-*

*Viulize: Ni nani araukaye na mapema kuzitema mbuga na kuzilaza?*
*Viulize: Ni nani akweaye minazi tangu kuchapo hadi lingiapo giza?*
*Viulize: Ni nani abebeshwaye mizigo hadi maungo yakageuka shaza?*
*Halafuye hana faida moja papatayo wala malipo yanayotosheleza-*
*Isipokuwa kusundugwa na kutupiwa matambara na vyakula vilivyooza?*
*Viulize: Ni nani huyo ni nani!*

*Viluliza: Ni nani ayalimaye mashamba na kuyapaliliya?*

*Na mimea kochokocho ikajaa kwa uzito ikajinamiya?*
*Hatimaye nani atajirikaye mali yakammiminikiya*
*Akaota na kitambi kama mja mzito wa miezi tisiya*
*Na akaongeza magari na wanawake kutoka na kuingiya?*
*Viulize: Ni nani huyo ni nani!*
*Na hao ndege kwa nyimbo nyanana watutumbuizao*
*Nayo hiyo ito kwa furaha maji itiririkao*
*Na huo upepo mkali wenye ghadhabu uvumao*
*Vyote hivyo vitatu vitakujibu kwa umoja wao:*
*"Ni Kibaruwa Manamba ndiye mtendaji hayo!"*

*NGOMA ZA LEO*
*Sikiliza hiyo mirindimo*
*Ya ngoma za leo*
*Ngoma za siku hizi*

*Ngoma hizi zizidipo milio*
*Machozi hututoa na furaha kutunyima*
*Za zamani zilitunyima machozi*
*na furaha zikatutia*
*Tulicheza lakini*

*Hizi za leo zimekosa makini*
*Na kiwewe zinatia.*
*Kwa kila avutiwaye na mahadhi yake*
*Kila mpigo una siri*
*Kila mdundo una chambo*
*Kila mvuto una mtego*
*Kila mwondoko una telezi*

*Wengi hawajitosi tena ukumbini*
*Kwa kuzichelea ngoma za leo*
*Wanasema: zinataka makini kuzivalia njuga*
*Maana, hawaziamini tena.*

*Hizi ndizo ngoma za leo*
*Ziwatumbuizao nusu vichaa*
*Vichaa wenyewe zawachenga*
*Wakabaki kurukaruka bila kupatana nazo*
*Na wenye zao timamu*
*Kazi yake inawazidi*
*Wakabaki machozi kuyapangusa*
*Hata tu kwa zao kumbukumbu*

*NDOTO MBAYA*
*Jana niliota*
*Ndoto ya uchoyo*
*Uchoyo wa ukuu*
*Ukuu wa kuwanyanyasa wengi*
*Ndoto mbaya ya jinamizi*
*Wanaowala watu wengi wakicheka*
*Wanaokula wakilalama njaa*
*Wanawameza wakiwa hai wazimawazima!*

*Juzi niliota ndoto mbaya pia*
*Ndoto yenye mazingaombwe*
*Wanaowala wakiwacheka na kuwapiga makofi*
*Makofi ya kusifu wale wanaowatafuna*
*Kusifu kwa uchungu wa kutojua kufahamu*
*Makali yanayozima uhai wa wengi!*

*Leo naota ndoto*
*Ndoto ya mchana*
*Mchana wenye giza*
*Ndoto mbaya iliyojaa mazimwi*
*Mazimwi wenye kuwahangaisha wengi*
*Kwa ahadi za Uongo zisizokwisha!*

*Usiku naogopa kuota tena*
*Ndoto mbaya za 'kaa vivyo hivyo'*
*Ndoto yenye kujaa giza mbele*
*Giza linalotisha maisha ya kizazi!*

*Je, kesho nitaota?*
*Noto yenye uhai wa kifo*
*Ndoto ya matumanini yanayoyeyuka*
*Kuyeyushwa kwa juha la mchana*
*Mchana wenye giza totoro?*
*Nauliza!*

*LIMWENGU TOFAUTI*
*Sebuleni niliketi*
*Mapema moja jioni*
*Nikaanza kumbo kuupiga*
*Mlima wa ugali.*

*Mboga nyama nikautowelea*
*Kabla ya maziwa mafunda kupiga*

*Na maji kuteremsha, koo kusafisha.*

*Pembeni niliketi*
*Nikipumua kwa shida*
*Na kushindwa kujinyanyua.*
*Taratibu askari wakaninyemelea*
*Na bakunja kunipiga.*

*Nilipozinduka nilikuta changu kisanduku*
*Macho kikiwa, habari kinamwaya*
*Ndipo nikaona wenzangu wananchi*
*Mizizi wakila na matunda mwitu.*
*Vyote wakivisaka kwa taabu.*

*Katika mazingira hayo ya sarabi*
*Miili yao ilikuwa taabu kuibeba*
*Kwa unyonge wa njaa.*
*Nikashanga tulivyoishi*
*Chini ya bendera moja*
*Lakini tukiwa mbalimbali*
*Katika limwengu tofauti*
*Kama ardhi na mbingu*

*AMANI*
*Uhuru pia amani*
*Usifikiri ni zawadi*
*Ambayo inapeanwa*
*Pasipo mikwaruzano*

*Kama wataka hakiyo*
*Sharti uwe tayari*
*Kupotea roho yako*
*Pamoja na ya mwingine*

*Uhuru jai ni la faru*
*Ambalo kulifikia,*
*Sharti uwe jasiri*
*Jasiri aso kifani.*

*WATUONAVYO!*
*Ninadokezapo, na kupokezapokeza,*
*Japo ni ya kuchukiza, nawaomba kusikiza*
*Weupe wajitukuza, na ubwana kutangaza,*
*Hakika wametuweza, uchokozi wamekuza*

*Kush na kizao chake, kwa wazungu na tiara*
*Kitoa mawazo yake, kwao pia ni hasara*
*Waume kwa wanawake, uzungunguni ni madhara*
*Lilaniwa kipekee, wazungu ndo wenye nira*

*Taswira ya huku kwetu, kwao bara jeusi*
*Waongeza utukutu, kudai yetu meusi*
*Waona tunayo kutu, nyingi kupita kiasi*
*Ama kwetu kila kitu, ni nduli kama kisasi.*

*Sisi tunaishi jana, nanyi mnaishi kesho*
*Mwasema sisi ni jana, nanyi ni nyuki wa mwisho*
*Kwa wazee na vijana, bado mwatutoa jasho*
*Twaogopa kubishana, kwani mwatoa vitisho*

*Mmetutia unyama, kusema sisi tumbili*
*Siku nyingi mmesema, sisi hatuna akili*
*Mwatuchukulia kama, hatuwezi uwakili*
*Ndiposa ninawauma, kwa matatu na mawili*

*Msemo wa ngozi ngumu, ni nyinyi mliobuni*
*Hata ikawalazimu, kulitia vitabuni*
*Kwenu hiyo ni hukumu, ya shina na mizizini*
*Mwatutenga kwa haramu, tadhani tuna tauni*

*Na hati za usafiri, ni vikwazo chungu tele*
*Hata waweza fikira, mbinguni ndiyo kilele*
*Kumbe tu ni Marekani, palipojaa kelele*
*Ingawa hatuwapingi, kuja kwetu tangu kale*

*Vitu ni vyetu Wakenya, mwasema mlivumbua*
*Mfano Mlima Kenya, mwaimba mlitambua*
*Porojo mkizifanya, mwadhani mwatuzindua*
*Mwazidi kutukanganya, kwa anga za kusumbua*

*Mungu siyo Athmani, na hakwendi msalani*
*Tukutane kiamanni, kujibu ya duniani*
*Tuchunguzwe kwa makini, tangu tukiwa tumboni*
*Wenye makosa moyoni, tatekezwa motoni*

*Basi hizo ni kurasa, za vitabu vya wazungu*
*Kufungua zinatesa, tena kwa mengi machungu*
*Kama huo ni usasa, ni heri nikale chungu*

*Baada ya hiyo misa, mimi ninakwenda zangu.*

*KIJIJI CHA MAUJI*
*Kina jambo lanikera, kila siku m'nasema*
*Moyo unayo hasira, kinywa kinalalama*
*Midomo imenifura, nywele zinanitetema*
*Leo natoa kalmia, mnipe yenu fasiri*

*Kwa muda nimefikiri, na nywele nikazikuna*
*Nikawa natafakari, mawazo kila namna*
*Mwisho ikawa sufuri, jawabu sikuliona*
*Ulimwengu ni kijiji, lakini cha jinsi gani?*

*Kijiji huishi ndugu, jamaa na marafiki*
*Wakakaa kwa udugu, na mapatano mithaki*
*Kwa wema sio vurugu, pasiwe na uzandiki*
*Kisemwacho yahe hiki, naona kina dosari*

*Takishi kwa dharau, na kwingi kubaguana*
*Tukaitana bahau, na huku twasukumana*
*Kunyang'nyana pilau, viwiko tukivunjana*
*Kuwe bado kijijini, kijiji cha aina gani?*

*Bidhaa za jalalani, barani tukitupiwa*
*Na mazao ya shambani, sisi tukilanguliwa*
*Uthori us'o kifani, kwao tukilaumiwa*
*Vipi isemwe ikawa, tumo kijiji kimoja?*

*Tumbo kafungwa mkaja, miguu kutiwa pingu*
*Miili ikaleleja, tukiabudu miungu*
*Tukisema haleluja, tukiwa katika chungu*
*Wapi inakubalika, pamoja sisi twaishi?*

*Tukigeuzwa kasuku, kusifu kila uthori*
*Ndipo tupwe mwiku, kwa kuwa tu mafakiri*
*"Wengine wametupiku, hili lazima tukiri"*
*Tukubali haya kweli, kijiji chetu kimoja?*

*Na sayensi kuchezewa, tuwe sisi ni vifaa*
*Kila ovu kufanyiwa, huku nasi twanyamaa*
*Iwe tunasaidiwa, tuepukane na baa*
*Nani asemaye ikawa, ywaishi sote pamoja?*

*Sisi kugeuzwa paia, kupigwa huku na huku*
*Masogi kutupakia, mchana kisha usiku*

*Vyetu wakituibia,"ni lanuni za utuku!"*
*Kushika tama daima, twaishi kweli pamoja?*

*Akili kukengesushwa, kwa vitabu vya kijinga*
*Mapiswa tukifundishwa, ukweli kuuboronga*
*Mengine kulazimishwa, ndipo tupate faranga*
*Lini inakubalika, chetu kijiji kimoja*
*Binti zetu kugeuzwa, bidhaa za madanguro*
*Wazee nao kup'uzwa, wabaki kwnye ugoro*
*Vijana hukengeushwa, wahariji kiwatoro*
*Anayekubali nani, kwamba kijiji kisawa?*

*Kila jambo kuamuliwa, na mijitu ajinabi*
*Ja watoto kukemewa, tutashikwa na kibibi*
*Kisa mikopo kupewa, tuwe twaona kivumbi*
*Iweje kulumba sie, kuwa twaishi pamoja?*

*MWANANGU NAKUUSIA*
*Amka uliyelala, hayile sasa kuchile*
*Bumburuka halahala, uvivu siwendekele*
*Chagua nguo kuvala, nuru njema uyonele.*
*Daima uraukile, nambele kutangulia*

*Ewe muogopa kazi, nguo sijifinikile,*
*Fahamia waziwazi, hilo litengezwile,*
*Guo Silone minyuzi, wenzio walishonele*
*Hatari kujiachile, ela kazi sakanyile.*

*Ilimu unayosoma, mwanafunzi nisikile*
*Jaribu kuwa na hima, yote uifahamile,*
*Kwani kila nikipima, maisha haya si yale*
*Lako ni kumakinile, mwanafunzi kusomele*

*Maisha ni jisu gutu, nyama halichinjwile*
*Namba na uwe mwenetu, keleti ujituzile*
*Ogopa na uche satu, anasa sizimbambile*
*Poa vitu sipapile, dunia ina salala*

*Rauka siwe mbishi, ushindani teletele*
*Sahau wako uzushi, ijara kusubirile*
*Tena kunena siishi, ni doto siiotele*
*Ulele nakwammshile, mipango kupangilia*

*Vurugu katu sipende, sikio lako tegile*
*Wangu mwana sinivunde, kwa haya nilokwambile*

*Ya tamu ja peremende, mwishowe waja juwile*
*Zaidi siendi mbele, kalamu naangushile*

*HOFU ZA BINADAMU*
*Hofu za wanyonge, ni nguvu za matajiri*
*Ambazo zinawaponda, wanapotaka usawa*

*Hofu za watawala, ni kupoteza uhuru,*
*Wa kutawala kwa mbavu, pamoja na utukufu*

*Hofu za mwanamke, mwanamke wa sasa*
*Ni kutumiwa ja rungu, daima kuwekwa nyuma*

*Hofu za mcha Mungu, ni maisha ya baadaye*
*Maana hana hakika, ndio aogopa kifo*

*Na hofu zao wasomi, ni kwamba wako baidi*
*Na wale wateteao, ambao si sawa nao*

*NILIPOKUWA TAJIRI*
*Dunia ina wambeya, wengi kupia kifani*
*Kama hujaizoeya, utabaki machozini*
*Kwa muda ukitembeya, utapokea maoni*
*Japo ukiieleya, hutabaki ushenzini*

*Nilikuwa na afisi, pamoja na wahazili*
*Kazi lifanywa kwa kasi, halafu wakanakili*
*Nilipokuwa na kesi, niliajiri wakili*
*Nilitusi matopasi, hadhi zao sikujali*

*Ni mimi niliyekwenda, kwa gari hata na ndege*
*Wala sikupanda punda, ili sifa niijenge*
*Utajiri kunitanda, ni dhana iliyo funge*
*Lakini liponidinda, walininyang'anya mwenge.*

*Vyakula vilisheheni, nikavifanyia kwata*
*Watu walinilaani, na wengine kunisuta*
*Niliitwa maluuni, kwa pumzi za kuteta*
*Tangia hapo zamani, nimebakia kujuta*

*Pombe nayo sikufichi, nilikunywa kwa vishindo*
*Kwa nguo pia na uchi, nilimeza kwa mtindo*
*Niliketi kwa makochi, kwa wingi wa madoido*
*Lilijaa langu pochi, hela kulipia tembo.*

*Linitka usuhuba, warembo wa kiamboni*
*Nilitekwa na mahaba, nikawa siwezekani*
*Ya halali na kuiba, yote nilikuwa ndani*
*Sio miji sio shamba, niliwika kwa utani*

*Na wapwa waliniita, kwa heshima si kwa jina*
*Mjomba liliwanata, bali siyo la Muchina,*
*Ukoo limetameta, na kujawa na thamana*
*Sawa wanasitasita, manake kaziyo sina*

*Ninaomba msamaha, aidha kwa nguvu zote*
*Nilidhani ni mzaha, nilipofanya popote*
*Sasa ninazo fedheha, katika mtima wote*
*Ninabaki nimehaha, siku zote nikiwaza*

*Kumbe mpandaji ngazi, mwishowe yeye hushuka*
*Nilipandishiwa kikazi, kisha nikateremka*
*Vizazi hadi vizazi, vijaribu kuj'okoa*
*Ninawaomba wazazi, m'nombee kwa Rabuka.*

*MOYO IWA NA SUBIRA*
*Usiliye moyo wangu,'siliye nyamaza*
*Usijitie matungu,'siliye 'tajiumiza*
*Huno ndiwo ulimwengu, muna yasiyopendeza*
*Kwa hiyo moyo nyamaza, zidi kuwa na subira*

*Yafute matozi yako, moyo sijiungulishe*
*Usijipe sikitiko, moyo usijikondeshe*
*Ituze nafusi yako, teka ujifurahishe*
*Hilino lisikuwashe, zidi kuwa na subira*

*Moyo nyamaa kuliya, matozi yako yaweke*
*Usizidi kuyamwaya, yaweke yatundizike*
*Matoziyo niwekeya, nifapo yatiririke*
*Huu si wakati wake, zidi kuwa na subira*

*Usiwe kama mkiwa, moyo wangu tangamka*
*Kwani mnyonge ukawa, na matama kujishika?*
*Ng'ara mfano wa juwa, uwate kuhuzunika*
*Sijiuwe kwa mashaka, zidi kuwa na subira*

*Mbona wazidi kuliya, K'wanza kuomboleza?*
*Ni ya nini yote haya? Hebu moyo nieleza*
*Haruma nakuoneya, uliyapo waniliza*
*Moyo nakusisitiza, zidi kuwa na subira*

*Utajiumiza mbavu, kuliya ukitosita*
*Utashikwa na chechevu, na homa utaipata*
*Upate na maumivu, langu ukitofuwata*
*Nyamaa matozi futa, zidi kuwa na subira*

*Dunia ni mdawari, hili moyo lifahamu*
*Na kuyapata mazuri, pasi mabaya vigumu*
*Kwa hiyi moyo subiri, tungu igeuze tamu*
*Usijiuwe kwa hamu, zidi kuwa na subira*

*Moyo kwamba halikuwa ulilolitarajiya*
*Lisikupe kuingiwa, na simanzi na kuliya*
*Hivyo ndivyo mambo huwa, ni kama lumbwi duniya*
*Shika n'nalokwambiya, zidi kuwa na subira*

*Hebu tupa jito lako, ukuangaliye nyuma*
*Kutizame utokako, moyo kwangaliye vyema*
*Utokako na wendako, kupi kwenye nyingi pima?*
*Usianguke simama, zidi kuwa na subira*

*Huku kwako mtihani, moyo wangu jitahidi*
*Yatuze yako makini, uwe mtuvu baridi*
*Faulu nikutahamini, nikutuze na zawadi*
*Hii nakupa ahadi, zidi kuwa na subira*

*Haya ni mafunzo kwako, funzika moyo funzika*
*Tabu na misukomisuko, si mwishowe kukufika*
*Katika uhai wako, hutaweza kuy'epuka*
*Muda yakikudirika, zidi kuwa na subira*

*Huwezi kuligeuza, lililotekeya kuwa*
*Kwa hivyo moyo nyamaza, uwate kujisumbuwa*
*Ufaalo kufanyiza, omba uwe na afuwa*
*Hakuna nyingine dawa, zidi kuwa na subira*

*Halikuwa ni la kuwa, si kama yale yawayo*
*Na yale ambayo huwa, huwa ni ya kuwa hayo*
*Na hili kwa kutokuwa, pengine ni heri hiyo*
*Basi tuwa ewe moyo, zidi kuwa na subira*

## Kibali cha NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **211301**

Date of Issue: **12/September/2024**

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Miss.. Martha MARTHA Gaceri of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Meru on the topic: HARAKATI ZA USHAIRI WA KISWAHILI KATIKA UJENZI WA JAMII YENYE MABADILIKO for the period ending : 12/September/2025.**

License No: **NACOSTI/P/24/39882**

**211301**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commission for Science, Technology and Innovation